# Nipashe

Jumatano Julai 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581733

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

**Adaiwa** kumng'oa meno matatu mke wake kisa Sh. 200 UKURASA 2



**Uamuzi** wa kesi ya Kabendera na Vodacom waiva UKURASA 5



**Korti** ya Rufani kuamua hatima watu kushtakiwa katika mahakama zisizo na hadhi UKURASA 5


Nipashe MWANZA TOLEO MAALUM

Sifa 10 za Mwanza, zikinyambuliwa na RC kulikoni kinara nyuma ya Dar

UKURASA 9

## IKITHIBITIKA...

# RC kufungwa gerezani maisha

• **Ni** anayeshtakiwa kumwingilia kinyume cha maumbile binti wa miaka 21... *Endelea uk. 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda (aliyevaa kofia), akiongozwa na makachelo wa polisi, kuingia katika Mahakama ya Mkoa wa Mwanza jana, kabla ya kusomewa shtaka la kulawiti binti ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu mkoani Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Rais wa zamani TLS apinga jina la Mwabukusi kukatwa

UKURASA 3



## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**SHULE YAKABILIWA UPUNGUFU, UCHAKAVU MATUNDU YA VYOO**

UKURASA WA 24

**YANGA YAANZIA 'GYM' IKIMTANGAZA ANDAMBWILE**

KIKOSI cha Yanga jana kimeanza rasmi maandalizi ya mashindano msimu ujao, huku klabu hiyo ikitamba kutwaa taji la kwanza nchini Afrika Kusini kwenye mich-



# Aliyekuwa Meya wa Ubungo aibua mapya mgogoro wa Simu 2000

UKURASA 2

**MICHEZO** KUNDI LA PILI SIMBA KUONDOKA LEO UK.24

**MAONI,** UK.6

# Aliyekuwa RC Simiyu kizimbani shtaka la ulawiti

. Ikithibitika, kifungo cha maisha au miaka 30 gerezani

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mwanza na kusomewa shtaka la kulawiti.

Kesi hiyo ya jinai namba 1883 ya mwaka 2024, ilifikishwa jana mahakamani huko mbele ya Hakimu Mfawidhi Mkuu Erick Marley.

Upande wa Mashtaka unawakilishwa na Waendesha Mashtaka wa Serikali, Martha Mtiti na Magreth Mwaseba, Dk. Nawanda akidaiwa kutenda kosa hilo Juni 2 mwaka huu.

Akisoma shtaka hilo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali Magreth Mweseba alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu namba 154(1(a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, marejeo ya mwaka 2022.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, kifungu hicho kinaelekeza: "Mtu yeyote ambaye anamwingilia mtu yeyote kinyume cha maumbile, atakuwa ametenda kosa, na atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha na wakati mwingine kifungo kisichopungua miaka 30."

Mweseba alidai mahakamani huko kuwa mshtakiwa Dk. Nawanda, mkazi wa Nyamata, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, anashtakiwa kwa kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile binti mwenye umri wa miaka 21 (jina tunahifadhi).

Alidai kuwa Dk. Nawanda alitenda kosa hilo katika eneo la maegesho ya magari lililoko Rock City Mall, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mshtakiwa Dk. Nawanda alikana kutenda kosa hilo. Mwendesha Mashtaka Mwaseba alidaiwa mahakamani huko kuwa upelelezi wa shauri hilo umeshakamilika, hivyo akaomba tarehe kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Wakili wa Utetezi wa Dk. Nawanda, Constantine Mutalemwa, aliomba mahakama hiyo kumwachia mteja wake kwa dhamana kwa kuwa kosa hilo linadhaminika.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote, Hakimu Marley alisema dhamana iko wazi endapo mshtakiwa huyo akikidhi masharti ya kuwa na wadhamini wawili; mmoja awe mtumishi wa umma na mwingine wa sekta binafsi na raia wa Tanzania mwenye utambulisho rasmi pamoja na bondi ya mali isiyohamishika yenye thamani isiyopungua Sh. milioni tano.

Mshtakiwa huyo alitimiza masharti hayo na kuachiwa kwa dhamana. Shauri hilo liliahirishwa hadi Julai 16 mwaka huu kwa ajili ya mshtakiwa huyo kusomewa maelezo ya awali na kesi kuanza kusikilizwa.

Kabla ya kuahirisha shauri hilo, Hakimu Marley alisema dhamana hiyo itakoma endapo mshtakiwa atavunja sharti lolote la mahakama ikiwamo kutofika mahakamani.

## Adaiwa kumng'oa meno mkewe kisa Sh. 200

**Na Ambrose Wantaigwa,** MARA

JESHI la Polisi mkoani Mara linamshikilia mkazi mmoja wa Kijiji cha Nyakatende wilayani Musoma, Musa Abdallah kwa tuhuma za kumn'goa meno matatu mke wake kwa kutumia 'pliers' kwa kile kilichoelezwa ni ugomvi wa Sh. 200.

Inadaiwa mtuhumiwa huyo ambaye ni mganga wa kienyeji alitenda ukatili huo baada ya mke wake huyo kutumia fedha hizo, zilizotokana na mauzo ya mahindi kununua mahitaji ya mtoto wao mdogo bila idhini yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Salum Morcase, alithibitisha tukio hilo akisema mtuhumiwa huyo akisaidiana na mke wake mwingine ambaye bado hajatiwa nguvuni walimkamata mke mdogo wakamlaza chini na kisha mume wake akamn'goa meno matatu.

"Mtuhumiwa huyo akisaidiana na mke wake wa pili walimshika mama huyo na kumlaza chini huku wakiwa wamemshikilia ambapo kwa kutumia pliers aliweza kutenda ukatili huo na kumsababishia maumivu makali," alisema.

Kamanda Morcase alisema hata hivyo, baada ya kutenda ukatili huo mtuhumiwa huyo ambaye yuko mikononi mwa polisi alimfungia ndani ya nyumba hadi taarifa kutoka wasamaria wema zilipofika polisi.

"Kwa sasa tunamshikilia kwa ajili ya mahojiano na uchunguzi ili hatua sahihi zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kumfikisha mahakamani kutokana na makosa yanayomkabili ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa polisi aliwatahadharisha wananchi kutumia njia sahihi za usuluhishi wakati wa migogoro, ikiwamo ya ndoa na kuepuka kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa hatua hizo husababisha uvunjifu wa sheria.


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**Dev Recoveries Limited** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (T) LTD,** tutauza kwa minada ya hadhara nyumba zifuatazo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe/siku ya tangazo hili.

Nyumba namba moja(1) imewekwa rehani kudhamini mikopo uliyotolewa na benki ya ICBTL kwa Bahadur Dewji Hassham na nyumba namba mbili(2 inamilikiwa na International Commercial Bank Tanzania Limited.Nyumba hizi mbili(2) zimeorotheshwa kwenye jedwali hapa chini.

Pia, Tangazo hili la minada ya hadhara, ni notisi ya siku kumi na nne(14) kwa mkopaji /wadhamini wa mkopo.

**MCHANGANUO WA NYUMBA ZITAKAZOUZWA**

| NO | JINA LA MKOPAJI/MDHAMINI | TAARIFA ZA NYUMBA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | BAHADUR DEWJI HASSHAM (Mkopaji na Mmiliki) | Nyumba ya makazi iliyopo jingo la Uhuru height,Barabara ya Bibi titi, Apartment 'F', gorofa ya 17 yenye hati nambari: 38083/85, kitalu' na. 63/27, MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 30/07/2024 kuanzia saa 05:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko nyumba. |
| 2 | INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK TANZANIA LIMITED(Mmiliki) | Nyumba ya makazi iliyopo jingo la Uhuru height, Barabara ya Bibi titi, Apartment F, gorofa ya 14 yenye hati nambari: 38083/30, kitalu' na. 63/27, MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 30/07/2024 kuanzia saa 05:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko nyumba. |

**Wanunuzi wote wenye nia na uwezo,mnakaribishwa kuja kukagua nyumba kwa vigezo na masharti yafuatayo:**

**VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA;**

1. Mali/Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 kutokea siku ya mnada.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa na mnada utarudiwa kwa tarehe nyingine.
4. Gharama za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji "Eviction" na nyinginezo, zitakuwa juu ya Mnunuzi.
5. Ukaguzi wa dhamana unaweza kufanywa na wanunuzi, siku yoyote kuanzia siku ya tangazo hili kati ya saa tatu asubuhi na saa kumi na moja jioni.
6. Kwa taarifa zaidi,wasiliana na Dev Recoveries Limited kupitia simu: **+255788438640/+255712390460**


# Meya wa zamani Ubungo aibua mapya Simu 2000

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob, ameibuka na kutetea wafanyabiashara wa Soko la Simu 2000 wilayani humo baada ya kuibuka madai kuwa eneo hilo umepewa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ili ujenge karakana.

Amesema kama manispaa hiyo imechukua uamuzi wa kugawa eneo hilo kwa DART, atarudisha wafanyabiashara hao eneo la Ubungo Mataa walikokuwa wanafanya shughuli zao kabla ya kuhamia eneo hilo.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X, Boniface aliandika jana kuwa Manispaa ya Kinondoni ilinunua eneo hilo lililokuwa na ekari tano kutoka kwa Shirika la Posta Tanzania wakati akiwa diwani mwaka (2010-2015) kwa madhumuni ya kuweka miradi ya uwekezaji ili kukuza mapato ya halmashauri.

Jacob alidai kuwa baada ya kununua eneo hilo, ikaligawa kwa matumizi ya stendi ya daladala, choo cha umma na soko la mazao na biashaara ndogo mwaka 2013 na kugawa vizimba vya soko kwa watu wasiostahili.

Alisema jambo hilo lilisababisha soko hilo kutokuwa na shughuli yoyote ya maendeleo kwa miaka miwili kwa kuwa waliopewa vizimba sokoni hapo siyo wafanyabiashara.

Alisema mwaka 2016, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, walianza utaratibu wa kuondoa machinga hao Ubungo Mataa na kuwapeleka maeneo rasmi bila mafanikio.

"Walipigwa mabomu, wakaharibu mali, wakafunguliwa kesi lakini machinga Ubungo Mataa hawakuondoka barabarani," alisema.

Alisema Mei Mosi, 2016, akiwa mstahiki meya na diwani wa manispaa hiyo, alifika eneo la Ubungo Mataa bila polisi na askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) na kuongea na wafanyabiashara hao na kuwaomba awapeleke eneo la Simu 2000.

"Niliwaambia kwa kuwa madiwani na watu wengine walipewa vizimba sokoni na maeneo nje ya soko wameshindwa kufanya soko lichangamke, basi kila mfanyabiashara wa Ubungo aende aingie pale sokoni Simu 2000, atakapochagua kukaa ndiyo pa kwake.

"Baada ya hotuba hiyo nilikwenda kwa maandamano mimi na wafanyabiashara wa Ubungo Mataa, tukaingia sokoni Simu 2000 kila mtu akakimbilia sehemu aliyoona inafaa," alisimulia.

Jacob alisema watu waliopita Ubungo Mataa siku hiyo walishangaa kukuta kukiwa safi na machinga wote walikubali kwenda soko la Simu 2000.

Alisema baada ya kugawanywa halmashauri, Ubungo iliwaomba wa Kinondoni wawachie Stendi ya Mawasiliano na soko hilo, na wao wakawaachia stendi na soko la Makumbusho na mali zingine waligawana kwa hisa za asilimia 60 Kinondoni na 40 Ubungo.

Alisema anashangazwa na uamuzi wa Baraza la Madiwani Ubungo la Julai 2024 kuamua kugawa eneo hilo muhimu na la kimkakati kwa mapato ya halmashauri na kutaka iwe karakana ya mabasi ya mwendokasi.

Alisema uamuzi uliochukuliwa bila kuwashirikisha wafanyabiashara hao utaliua soko hilo na kupoteza mapato ya halmashauri.

"Wanavunja soko wakati huu kukiwa na miundombinu ya zaidi ya Sh. billioni moja ambayo iliboresha mazingira ya soko la Simu 2000 kama ujenzi wa fensi, ujenzi wa mabanda ya soko, ujenzi wa choo sokoni, ujenzi wa vizimba, umeme na maji," alisema.

Alipoulizwa kuhusu uamuzi wa Baraza la Madiwani , Meya wa Ubungo, Affary Juma Nyaigesha, alithibitisha baraza hilo limepitisha uamuzi wa kukabidhi DART eneo hilo, lakini haina maana ya kuwa wafanyabiashara hao wataondolewa.

Alisema katika awamu hii ya utawala uliojaa uhuru na haki serikali haiwezi kuondoa wajasiriamali ambao wanategemea eneo hilo kujipatia kipato.

Juzi asubuhi machinga wa eneo hilo waligoma na kuziba barabara kuzuia magari kuingia katika kituo cha mabasi, wakilalamikia uamuzi wa manispaa hiyo kuipa DART eneo hilo ili kujenga karakana ya mabasi ya mwendokasi.

Wakati wakiendelea na mgomo huo, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko, kwa ajili ya kuzungumza nao walikataa na kumtaka aondoke kwa madai kuwa hawana imani naye.

Baadaye alifika Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila na kuwataka wafungue biashara zao kwa kuwa atakwenda kufanya kikao na DART, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Manispaa ya Ubungo kisha atawaletea mrejesho Julai 13, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Rais wa zamani TLS apinga jina la Mwabukusi kukatwa

Na Restuta James

UAMUZI wa Kamati ya Rufani ya Uchaguzi (EAC) kumwengua Wakili Boniface Mwabukusi, aliyekuwa akiwania urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), umemwibua aliyewahi kukalia kiti hicho, Wakili Francis Stola, akiupinga na kusema ni haramu huku akihoji muda wa hukumu hiyo.

Katika andiko lake, Stola amesema uamuzi wa kamati hiyo ya TLS iliyobatilisha Kamati ya Uchaguzi ya chama hicho, ambayo ilimpitisha Mwabukusi kuwa miongoni mwa wagombea, uko kinyume cha mamlaka yake.

Kwa mujibu wa EAC, Wakili Mwabukusi ameenguliwa kwa maslahi ya umma kwa madai ya utovu wa nidhamu.

Katika andiko hilo, Stola anasema kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha kanuni za TLS za mwaka 2022, EAC haina nguvu ya kubatilisha uamuzi wa Kamati ya Uchaguzi wa chama hicho iliyomwidhinisha Mwabukusi.

"Kwa hiyo, kwa hali ilivyo leo, kamwe Mwabukusi hatofuzu kugombea nafasi ya Rais wa TLS kwa sababu EAC imempa adhabu isiyo na kikomo.

Kama hii (urais), ni nafasi nzuri kwake, ni lini katika maisha yake atarejeshewa sifa za kustahili kugombea nafasi ya Rais wa TLS siku zijazo? Ni mahakama ipi itakayomsafisha? Je, hii ni hukumu ya maisha? Jibu ni ndiyo. Je, hii ndiyo ilikuwa nia ya kamati hii? Hapana!" anasema.

Stola anasema uamuzi wa kamati ya rufani umempa Mwabukusi adhabu mara mbili kwa kuwa alishaadhibiwa kwa kupewa onyo.

"Kwahiyo, ni makosa kumwadhibu mara mbili kwa kosa lilelile. EAC haikuzingatia hoja ya Kamati ya Uchaguzi iliyoeleza kwamba kumwengua Mwabukusi kwa kosa la utovu wa nidhamu ni kumwadhibu mara mbili.

"Na je, ni taasisi ipi na sababu zipi zitatolewa kwa siku zijazo kwamba sasa Mwabukusi ameshatumikia adhabu yake na kwamba yuko safi kuwania urais wa TLS? Na ikiwa sababu hiyo itakuwapo siku za usoni, basi kwanini isitolewe sasa? EAC imekosea katika hoja na sheria. Huu ndio msimamo wangu wa sasa," Stola anasema.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwabukusi alisema aliweka nia ya kuwania urais wa TLS ili akifanye chama hicho kiwajibike kwa umma na kwa wanachama wake.

"Kama ningechaguliwa kuwa rais wa TLS ningeifanya iwajibike kwa umma na kwa wanachama. Kwa sasa haiwajibiki ndio maana masuala yote ya umma unaona chama kiko kimya," alisema.

Wakili hiyo alisema kuenguliwa kwake ni kinyume cha kanuni kwa kuwa kosa la nidhamu alilotuhumiwa nalo alishapewa onyo Mei mwaka huu, adhabu ambayo alisema inajitosheleza.

Baada ya Mwabukusi kuenguliwa, wagombea wanaochuana kuwania urais wa TLS ni Kapteni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda na Sweetbert Nkuba.

# Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

Na Halfani Chusi



MTOTO Barack Majijeh (13) amepotea tangu Julai 5 mwaka huu wakati akirejea nyumbani Mtaa wa Maweni Kata ya Mji Mwema Wilaya ya Kigamboni Dar es Salaam kutoka shuleni.

Kwa mujibu wa mama yake, Mariam Majijeh, mwanawe huyo (pichani) anasoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Abdu Jumbe, wilayani Kigamboni.

Mama huyo aliiambia Nipashe jana kuwa siku hiyo, mwanawe hakurudi nyumbani na hajapatikana mpaka jana, ikiwa ni siku ya tano tangu kupotea kwake na hawajui kilichomsibu.

Alisema tayari ameshafanya jitihada za kumtafuta katika hospitali na vituo vya polisi bila mafanikio, akifafanua kuwa wakati anaondoka nyumbanii alivaa fulana yenye rangi ya bluu, suruali (damu ya mzee) na raba nyeupe.

Alisema waliposhindwa kumpata, walitoa taarifa Kituo cha Polisi Kigamboni na kupewa namba ya shauri (RB): KGM/RB/217/24.

Mama huyo aliomba Watanzania na yeyote atakayemwona mwanawe, apige simu namba 0715803235 au 0617903235.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Mahakama Rufani kuamua hatima watu kushtakiwa korti wasizostahili

**Na Kulwa Mzee**

MAWAKILI katika shauri la kupinga vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinavyoruhusu washtakiwa kufikishwa kwenye mahakama za chini wamepingana kwa hoja, upande wa mrufani ukidai Mahakama Kuu ilikosea huku upande wa serikali ukidai mahakama hiyo ilikuwa sahihi kutupilia mbali shauri hilo.

Hayo yalijiri jana katika Mahakama ya Rufani mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji Sam Rumanyika, Jaji Augustine Mwarija na Jaji Lameck Mlacha wakati shauri hilo lilipokuwa linasikilizwa.

Mrufani katika shauri hilo namba 165 la mwaka 2021 ni Wakili Onesmo Olengurumwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Rufani hiyo inatokana na uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Masjala ya Dar es Salaam uliotolewa mwaka 2020, ukitupilia mbali kesi hiyo kwa madai kwamba aina ya maombi na kiini cha msingi katika maombi hayo tayari kilikwishaamuliwa katika mashauri ya awali.

Shauri hilo lilikuwa linapinga vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinavyoruhusu washtakiwa kushtakiwa kwenye mahakama za chini ambazo hazina mamlaka ya kusikiliza kesi hizo.

Mwombaji alilalamikia vifungu namba 178, 243, 244, 245, 246, 247, 248, 249, 250, 256, 257,258 na 259 vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kwa madai kuwa vinakiuka Katiba na haki za binadamu, akitolea mfano haki ya kusikilizwa kwa usawa mbele ya sheria na zingine ambazo zipo katika Ibara ya 13 1)(2) na (6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Mrufani, akiwakilishwa na Wakili Mwandamizi Mpale Mpoki, akisaidiana na Wakili Daimu Halfani, aliwasilisha hoja mbili.

Katika hoja ya kwanza, alidai Mahakama Kuu ilikosea kutupilia mbali kesi hiyo kwa kigezo kuwa kiini na aina ya kesi hiyo ilikwishaamuliwa katika kesi ya Galeba. Kesi ya Galeba ilipinga vifungu viwili tu wakati kesi ya Olengurumwa inapinga vifungu 13 vya CPA.

Hoja ya pili inadaiwa kwamba jopo la majaji wa Mahakama Kuu lilikosea kumpangia jaji mmoja kati yao ili kusikiliza pingamizi lililosababisha kesi hiyo kutupwa kinyume cha utaratibu ambapo ilitakiwa Jaji Kiongozi ndiye apange jaji mmoja kwa ajili ya kusikiliza pingamizi.

Wakili Mpoki aliendelea kudai kwamba vigezo vya msingi vilivyotajwa kwenye kifungu cha 9 na ufafanuzi wa aya ya 6 ya kifungu hicho cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai havikuthibitishwa na mawakili wa serikali.

Alidai utaratibu uliotumika na mahakama baada ya mapingamizi kuibuliwa wakati ambao majaji watatu wa mahakama hiyo wameshaketi kusikilizwa msingi wa shauri, haukuwa sahihi.

Wakili wa Serikali Narindwa Sekimanga, akijibu, alipinga hoja za mrufani na kusema kwamba uamuzi wa Mahakama Kuu ulikuwa sahihi kwa sababu msingi wa vifungu viwili katika kesi ya Galeba ni wa watu kushtakiwa katika mahakama ambazo hazina mamlaka ya kusikiliza kesi, hivyo hata kesi ya Olengurumwa msingi wake ni huo japokuwa ina vifungu vingi.

Kutokana na kudai hayo, Jaji Mwarija alihoji endapo kuna sheria au kanuni inayoruhusu majaji watatu waliopangiwa kesi kujipangia mmoja kati yao kusikiliza pingamizi, Wakili Narindwa alidai kuwa hakuna sheria wala kanuni inayosema hivyo.

Shauri hilo liliahirishwa hadi tarehe nyingine itakayopangwa kwa ajili ya kusomewa uamuzi.

# Uamuzi kesi ya Kabendera, Vodacom waiva

**Na Kulwa Mzee**



Wakili Peter Madeleka anayemwakilisha Mwandishi wa Habari Erick Kabendera (hayupo pichani), akitoka Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, kuwasilisha maombi katika kesi ya mteja wake ya kuidai kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania fidia ya Sh. bilioni 28 kwa madai ilifanikisha kutekwa kwake mwaka 2017. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam, inatarajia Agosti 21, mwaka huu kutoa uamuzi kama kesi ya madai iliyofunguliwa na mwanahabari, Erick Kabendera akiomba mahakama iamuru kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom imlipe Sh. bilioni 28 kwa madai ya kufanikisha kutekwa kwake, kama iko mahakamani kihalali au itupwe.

Uamuzi huo ulifikiwa jana mbele ya Jaji Salma Maghimbi, wakati shauri hilo lilipokuwa linatajwa.

Akimwakilisha Kabendera, Wakili Peter Madereka alidai walalamikiwa Vodacom kupitia Wakili wao, Gasper Nyika, waliwapa majibu ya madai dhidi yao jana pamoja na kusudio la kupinga madai yaliyoko mahakamani.

"Mheshimiwa Jaji kuna notisi ya pingamizi, tunaomba kabla ya kuendelea na shauri la msingi tupewe utaratibu wa kusikiliza pingamizi na kwa upande wetu tunaomba lisikilizwe kwa maandishi," alidai Wakili Madereka.

Wakili Nyika alidai wamewasilisha majibu ya utetezi pamoja na pingamizi, wanakubali pingamizi walilowasilisha lisikilizwe kwa njia ya maandishi.

Jaji Maghimbi baada ya kusikiliza maombi hayo aliamuru upande wa wajibu maombi kuwasilisha hoja za pingamizi Julai 23, mwaka huu.

Aidha, aliamuru mwombaji ajibu pingamizi hilo Agosti 6, kama kuna hoja za nyongeza ziwasilishwe Agosti 13 na mahakama itatoa uamuzi kama shauri hilo liko mahakamani kihalali au Agosti 21, mwaka huu.

Vodacom kupitia Wakili Nyika wanapinga shauri hilo kusikilizwa kwa madai kesi ilifunguliwa nje ya muda kisheria, wanaomba itupwe.

Katika kesi ya msingi Kabendera anaoimba mahakama hiyo iamuru kampuni hiyo imlipe fidia ya Dola za Marekani milioni 10 (Sh bilioni 28), akiituhumu kuwa ndio iliyofanikisha kukamatwa kwake na askari polisi, tukio analoliita kutekwa na kisha kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi, mwaka 2019.

Anadai kutokana na matukio hayo amepata madhara ya kiuchumi na yasiyo ya kiuchumi, kijamii, maumivu ya kiakili na kimaono, hasara ya kutokufurahia maisha hasara ya maendeleo binafsi na hadhi yake katika jamii na kutoaminiwa kitaaluma.

Kabendera anataka kampuni hiyo imlipe kiasi hicho cha fedha, Dola za Marekani milioni 10 kama fidia ya hasara halisi na riba kwa kiwango cha mahakama kuanzia tarehe ya hukumu mpaka kumaliza malipo yote.

Pia, anataka alipwe fidia ya hasara ya jumla kadri mahakama itakavyotathmini, gharama za kesi na nafuu nyingine kadri mahakama itakavyona inafaa.

Hati ya madai katika kesi hiyo Kabendera imeeleza matukio yaliyojiri katika simu yake kabla ya tukio la kukamatwa kwake, kuwa ilianza kupoteza mawasiliano na kumfanya ashindwe kupata huduma.

Pia, amedai juhudi alizofanya kujua chanzo cha hali hiyo kwa kufanya mawasiliano na mwakilishi wa huduma kwa wateja na hata kutembelea ofisi za kampuni hiyo, lakini hakupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Katika hati ya madai anadai Julai 27, 2019, saa 9:00 Alasiri alipoiwasha simu yake ambayo alikuwa ameizima tangu jana yake usiku na ndipo alipobaini haikuwa na mtandao.

Alidai, mwakilishi wa huduma kwa wateja wa Vodacom alimweleza kuwa namba yake ya simu ya Vodacom (+255767456796) ilikuwa na changamoto za kiufundi ambayo ilimhitaji kutoa taarifa katika kituo cha huduma kwa wateja cha karibu kilichopo Tegeta.

Kabendera alimtaka mwakilishi huyo kueleza tatizo ni nini kabla ya kwenda kituoni, lakini mwakilishi huyo alikataa akidai kuwa ni suala nyeti ambalo linamtaka aende binafsi kituoni hapo.

Alidai badala yake walimshauri atembelee ofisi zao zilizoko Mlimani City asubuhi, hata hivyo saa 9:00 alasiri siku hiyo hiyo ya Julai 29, 2019 ghafla simu yake ilianza kufanya kazi, kisha alipopigiwa simu na mwakilishi wa Vodacom ambaye alimtaka (Kabendera) amwelezee tatizo lake na baada ya kumwelezea kwa takribani dakika tatu, alikata simu akiahidi kumpigia baadaye kidogo.

Alidai baada ya dakika tatu Kabendera alipokea simu iliyopigwa kutoka huduma kwa wateja Vodacom na kubaini kuwa ilikuwa ni sauti ya mwanamume, ambaye alimtaka Kabendera aeleze mahali alikokuwa na kwamba simu hiyo ilikuwa ikikwaruza kama vile ilikuwa inarekodiwa.

Anadai kabla ya simu hiyo kukatwa mteja alimsikia huyo aliyempigia simu hiyo akinong'ona kuwa alikuwa nyumbani kwake.

Kwa mujibu wa hati hiyo, maelezo hayo yalimshtua Kabendera na akakimbia sehemu ya juu ya nyumba yake ambako aliweza kuona magari kadhaa ambayo hakuyafahamu, karibu ya nyumba yake.

Aidha, lilitokea gari lingine aina ya Toyota Alphard liliegeshwa mbele ya magari hayo upande wa kulia mwa nyumba yake, halafu wakashuka watu wanne ambao walijitambulisha kuwa maofisa wa polisi, lakini walikataa kutoa utambulisho. Walimpiga pingu kumshikilia kizuizini kwa siku mbili.

Hati hiyo inaendelea kueleza kuwa wakati wa mahojiano, maofisa wa polisi walifika katika chumba cha mahojiano wakiwa na karatasi zilizochapishwa kutoka katika kompyuta (printout) za akaunti za fedha ya simu na namba za simu alizokuwa amezipiga kwa mwaka mzima.

Walimhoji lengo la kila muamala alioufanya kwa mwaka mzima nyuma na pia uhusiano wake na watu aliokuwa amewasiliana nao miaka kadhaa.

Kabendera analalamika kuwa polisi na serikali walitoa taarifa kadhaa zenye mgogoro kwa umma kuhusiana na 'kutekwa' kwake na kwamba walimtuhumu kwa kutokuwa raia na kumkashifu Rais (wa wakati huo) John Magufuli.

Anadai alishtakiwa mahakamani kwa makosa ya utakatishaji fedha, uhujumu uchumi na ukwepaji kodi na matokeo yake walimuweka chini ya ulinzi mkali katika mahabusu ya Gereza la Segerea.

Anadai kuwa akiwa mahabusu, mama yake, Verdiana Mujwahuzi, alifariki dunia na hakuruhusiwa kuhudhuria mazishi yake na kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa na tatizo la kiafya.

Anadai katika hati ya madai kuwa kutokana na hali hiyo aliamua kukiri makosa na kulipa fidia ya Sh. milioni 273 ili atoke mahabusu na kwamba baada ya kuachiliwa marafiki na familia yake walimweleza kuwa walipigiwa simu na polisi wakiwaonya kutokumtembelea mahabusu na kwamba vinginevyo wangepata hatari.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyabiashara watengewe maeneo ya uhakika wa kudumu

**WAFANYABIASHARA** wadogo au wamachinga wanaouza bidhaa mbalimbali mijini na kwenye majiji ni waathirika wa majanga mengi.

Mosi, moto unaoteketeza mali zao, kadhalika kuhamishwa mara kwa mara kwenye maeneo waliyohamishiwa.

Adha wanazokumbana nazo ni wakati mwingine kupata vipigo na kupoteza mali zao wakati wanapokaidi kuhama maeneo hayo. Katika matukio hayo kuna wengine waliopoteza maisha katika heka heka hizo.

Ni kutokana na mali zao kuteketea, kuibwa, kubomolewa maduka na vibanda na masuala yanayofanana na hayo katika masoko mbalimbali nchini.

Inaumiza kuona mtu aliyejitahidi kutafuta mtaji kwa shida na baadaye anapofungua biashara yake na kuanza kutengemaa anatakiwa kuondoka na wakati mwingine kwa kuvunjiwa vibanda vyao.

Wamachinga wa soko la Simu 2000 au kituo cha mabasi cha Mawasiliano kilichoko Ubungo Dar es Salaam, hoja yao ni kuwa walihamishiwa hapo na kuhakikishiwa hawatabugudhiwa.

Taarifa za kuwahamisha kutoka kituoni hapo kwa maelezo kuwa soko hilo limetolewa kwa kampuni ya mabasi yaendayo kasi ili kujenga karakana, zimewafanya kuzua sintofahamu hiyo.

Tumewasikia wafanyabiashara hao wakisema wanataka kusikilizwa na kuamuliwa hatima yao ili ieleweke.

Wamachinga wa Simu 2000, wanasikika wakisema wamekaa katika eneo hilo baada ya kuhamishwa kutoka maeneo mengine wakiambiwa kuwa kituo cha Mawasiliano kitakuwa cha kudumu.

Ni wazi kuwa wanaofaidika na masoko Dar es Salaam ni wafanyabiashara mbalimbali kutoka Tanzania nzima, wanaoleta bidhaa zao mijini kwenye mahitaji makubwa.

Ni uchumi wa nchi na pia ni maisha ya Watanzania.

Soko la Simu 2000 ni mali ya serikali na wafanyabiashara hao wanatakiwa kusikiliza na kuheshimu serikali ambayo ndiyo inayosimamia ardhi kwa maendeleo ya taifa.

Lakini ni lazima pia kuangalia hatima ya wamachinga hao ambao wamejiajiri ili kumudu maisha yao.

Serikali imeahidi kukaa nao Jumamosi ni jambo jema, lakini kuja na ufumbuzi wa kudumu wa masoko ya wamachinga kwenye majiji na miji ndicho kitu muhimu zaidi.

Wamachinga wafahamu wanakwenda wapi kufanya biashara zao, kwa utaratibu wa kumudu maisha yao.

Wafanyabiashara hao wanalalamika kwamba hawakupewa notisi na kwamba wamesikia kuhusu uhamisho wao kwenye mitandao na kutaka haki itendeke.

Masuala yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja kama ajira yaangaliwe kwa umakini mkubwa.

Tunajua soko la Mawasiliano au Simu 2000 ni sehemu watu walipojiajiri ndiko uliko mkate wao wa kila siku, ingekuwa vyema wakashirikishwa kwenye kufikia maamuzi badala ya kuyasikia mitandaoni.

Tunajua lengo la serikali ni jema la uamuzi wa kukabiliana na foleni na kurahisisha usafiri Dar es Salaam, maamuzi hayo yanahitaji kuyatafakari na kushirikisha pande zote tena ziridhike ili kuepusha taharuki.

Serikali ina maeneo mengi na pia ina uwezo wa kuweka kitega uchumi popote hivyo si vibaya ikatafakari kupeleka karakana hiyo eneo lisilo na wafanyabiashara ili kuepusha migogoro.

Baadhi ya sehemu ni Kimara Temboni ambako ipo sehemu iliyofungiwa inayohifadhi magari mabovu, ikisimamiwa na Wakala wa Taifa wa Barabara -TANROADS.

Tunawasihi wafanyabiashara hao kusikilizwa na kuwasiliana na serikali ili kuwa na mchakato wenye amani unaowanufaisha pia ukilinda maslahi ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Dokta Omar shujaa wetu mpenda amani

Na Sabato Kasika

**MAONESHO** ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam, Sabasaba yanayofanyika Julai kila mwaka, hayawezi kumalizika bila kurejea kumbukizi za Makamu wa Rais wa awamu ya tatu, Dk. Omar Ali Juma.

Aliaga dunia Julai 4, 2001 wakati wa maonesho hayo yakiendelea, hadi leo anakumbukwa kwa kufanikisha uwepo wa uchaguzi wa vyama vingi ambao alikuwa mgombea mwenza wa Benjamin Mkapa mwaka 1995.

Alifariki wakati serikali ya awamu ya pili ikiwa kwenye muhula wa pili baada ya kuchaguliwa tena kwenye uchaguzi mkuu wa 2000.

Miaka 23 iliyopita wakati wa maonesho ya Sabasaba kiongozi huyo alifariki dunia, saa chache baada ya kutoka kwenye viwanja vya maonesho Kilwa Road.

Julai 4 mwaka 2001 kabla ya kufariki dunia kiongozi huyo alitembelea mabanda mbalimbali katika maonyesho hayo, lakini muda mfupi baada ya kurejea nyumbani Oyster bay, habari za kifo chake zilisikika.

Tukio hilo liliwaacha Watanzania katika majonzi, huku wengine wakiwa hawaamini taarifa za kifo chake, hasa wale waliomshuhudia akitembelea mabanda mbalimbali kwenye viwanja vya Sabasaba.

Lakini, huo ndiyo ukawa mwisho wa miaka 60 ya safari ya Dk. Omar Ali Juma, hapa duniani, ambaye alizaliwa Juni 26 mwaka 1941 na kufariki dunia Julai 4 mwaka 2001.

Wakati huu wa kumbukumbu ya kifo chake, ni vyema pia kukumbusha na kuelezea machache kuhusu kiongozi huyo ambaye alidumu katika nafasi hiyo miaka sita.

Huyo ndiye alikuwa mgombea mwenza wa kwanza katika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi uliofanyika 1995 na kuunda serikali ya awamu ya tatu ya Rais Benjamin Mkapa.

Baada ya uchaguzi huo, Dk. Omar Ali Juma, akawa Makamu wa Rais wa kwanza ambaye marekebisho ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalianzia kwake.

Marekebisho hayo yalikuja wakati nchi inajiandaa kufanya uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa ambapo mapendekezo ya marekebisho yalitokana na ushauri wa Tume ya Jaji Bomani.

Tume hiyo ilipendekeza kuwapo mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano ambaye anakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweka pembeni utaratibu kuwa Rais wa Zanzibar anakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Kuanzia hapo hadi sasa, Rais wa Jamhuri ya Muungano na wa Zanzibar wanakuwa na mgombea mwenza ambaye ndiye Makamu wa Rais.

Unapozungumzia urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi, si rahisi kusahau jina la kiongozi shupavu Dk. Omar, kwa sababu unamgusa katika maeneo mbalimbali kuanzia marekebisho ya katiba.

Ni wa kwanza kuwa mgombea mwenza na hatimaye kushika nafasi ya Makamu wa Rais akianzia kwenye mfumo wa vyama vingi, ambavyo yeye na Mkapa walikuwa wahusika wakuu.

Wakati akiwatumikia Watanzania Dk. Omar Ali Juma, anayesifika kwa upole na unyenyekevu, mambo mbalimbali yalijitokeza kwenye uwanja wa siasa za vyama vingi na kuibu mgogoro wa CCM na CUF kisiwani Pemba.

Akishirikiana na Mkapa hawakukaa kimya ili walisimamia na kukutana mezani ambako vyama CCM na CUF vilitiliana saini muafaka wa maridhiano Juni 9, 1999 na kudhamiria kwa makusudi kutekeleza walichokubaliana na chini ya mpatanishi Jumuiya ya Madola.

Makamu wa Rais ofisi yake ilipewa jukumu rasmi la kutunza na kusimamia mazingira, akawa kiongozi anayeliongoza taifa kulinda mazingira kupambana na uharibifu na uchafuzi wa kila aina.

Atakumbukwa kwa kuanzisha kampeni maalum ya kitaifa ya

kupanda miti milioni kila mwaka, kampeni waliyoianza mwanzoni mwa 1999.

Dk. Omar Ali Juma pia alipiga vita umaskini na uharibifu wa mazingira, hayo yalikuwa ni miongoni mwa mambo yaliyomkera huku akiamini kuwa umaskini una pacha ambaye ni uharibifu wa mazingira, na kwamba mama yao ni ujinga.

Yapo mengi yanayomgusa kiongozi huyo, lakini kubwa zaidi likiwa ni la Makamu wa Rais wa kwanza kuhudumu katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, chini ya utaratibu wa kuwa na mgombea mwenza.

HABARI KITAIFA

# Shule yakabiliwa upungufu, uchakavu matundu ya vyoo

**Na Jumbe Ismailly,** MANYONI

SHULE ya Sekondari Kilimatinde, wilayani Manyoni, mkoani Singida inakabiliwa na uhaba wa matundu 15 ya vyoo vya wanafunzi na mawili ya walimu.

Vilevile, zaidi ya wanafunzi wa kike 200 wanaoishi bwenini, wanakosa mahali pa kuhifadhi na kuteketeza taulo za kike.

Mkuu wa shule hiyo, Jenifer James alisema kuna wanafunzi 493, wakiwamo wavulana 229 na ina uhitaji wa matundu ya vyoo 25, yakiwamo 10 ya wavulana.

“Tuna changamoto ya matundu ya vyoo, tuna matundu manne kwa upande wa wavulana na matundu sita kwa upande wa wasichana, lakini tunatakiwa tuwe na matundu 10 ya wavulana na matundu 15 ya wasichana, hivyo tuna upungufu wa matundu sita kwa wavulana na tisa kwa wasichana,” alisema.

Mwalimu huyo alisema kuwa kutokana na janga la ugonjwa wa kipindupindu lililopo kwa hivi sasa, wanahitaji matundu ya vyoo kulingana na idadi ya watoto walionao.

Pia shule hiyo yenye walimu 14 wakiwamo wanaume tisa inahitaji matundu ya vyoo manne, yaliyopo ni mawili.

“Walimu pia tuna changamoto ya vyoo vyetu vimechakaa ni vya muda mrefu na tuna tundu moja kwa upande wa walimu wa kiume na tundu moja kwa upande wa walimu wa kike pia havitoshi, lakini vile vile ni vya muda mrefu na vimechakaa,” alisisitiza Jenifer.

Aliiomba serikali kusaidia uboreshaji wa miundombinu ya vyoo ili waishi katika hali ya usalama na shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi viweze kwenda salama.

Mwakilishi wa wanafunzi hao, Juliana George, alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa matundu ya vyoo, na kwamba kwenye mabeni kuna wanafunzi 52 wanaotumia matundu matatu.

Aidha, alisema changamoto nyingine ni kukosekana sehemu ya kuhifadhia taulo za kike za wanafunzi zaidi ya 200 na mashimo ya kuchomea taulo za kike hali inayowalazimu kukusanya tu na kuchoma kwenye mashimo ya kawaida ya taka.

“Tunasubiriana wakati mwingine kama kipindi hiki cha baridi tunakwenda haja ndogo mara kwa mara hata kule bwenini hivyo hivyo. Tunaiomba serikali itusaidie kwenye hili,” alisema.

Akizungumzia changamoto hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Anastazia Tutuba, alithibitisha changamoto hizo na kwamba wamejipanga kuziondoa kwa kadri bajeti zinavyoruhusu.

# Vijiji 45 vyawekwa mipango matumizi ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** UVINZA



NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda amesema vijiji 45 kati ya 61 wilayani Uvinza, mkoani Kigoma vimewekwa mipango ya matumizi ya ardhi.

Pinda aliyasema hayo juzi wilayani Uvinza katika siku ya kwanza ya ziara ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpanga mkoani Kigoma.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, Mji wa Uvinza kwa sasa unakua kwa kasi na wizara yake kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo iliamua kuviwekea vijiji vya wilaya hiyo katika mipango ya matumizi ya ardhi ili kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile kilimo na ufugaji.

“Uamuzi wa kuviwekea mipango ya matumizi ya ardhi vijiji 45 katika Wilaya ya Uvinza ni njia sahihi ya kupunguza mgongano wa matumizi ya ardhi na zoezi litaendelea katika vijiji vilivyobakia 16 ambavyo viko katika mpango kazi,” alisema Pinda.

Naibu Waziri Pinda alisema mgogoro baina ya wananchi wa Kijiji cha Mpeta na Ranchi ya NARCO, ulisababishwa na wananchi wa kijiji hicho kutoridhika na hekta 2,500 walizopatiwa kutoka kipande cha ranchi ambapo kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Ardhi tayari serikali imesikia kilio cha wananchi hao na kuwapatia hekta nyingine 5,240 ili kutosheleza mahitaji.

Hata hivyo, Pinda aliagiza Mkuu wa Wilaya ya Uvinza pamoja na mkurugenzi wa halmashauri kukaa na viongozi wengine wa wilaya hiyo kuhakikisha hekta zilizotolewa zinagawiwa kwa wananchi kwa lengo la kukidhi mahitaji.

Akizungumzia mgogoro baina ya Wilaya ya Kasulu na Uvinza kuhusiana na kitalu cha uwindaji alichopatiwa mwekezaji, Pinda alimweleza Makamu wa Rais kuwa kitalu alichopewa mwekezaji, ramani yake ina upungufu, hivyo ameielekeza ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kigoma itakutana na halmashauri za wilaya husika ili kupata tafsiri sahihi ya ramani kwa lengo kutafuta suluhu ya mgogoro huo.

Makamu wa Rais, Dk. Mpango alianza ziara yake mkoani Kigoma juzi. Pamoja na mambo mengine, amekagua miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya umeme na barabara.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 2.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 3. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2.SALUM JUMA MARWA 3.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.MBEZI MANYEMA 2.KIGOGO KATI 3.KINZUDI GOBA | 17/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 18/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | MBM MOTORCYCLE SPARES | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 101, KITALU "47", HATI NAMBA 52425 | PETER SIMON MSANZYA | KIJITONYAMA -DAR ES SALAAM | 19/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 300-SNGLR, KIWANJA NAMBA 794 &796 KITALU 'A' CHAPWA TUNDUMA | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | CHAPWA TUNDUMA | 19/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 19/07/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 18/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 18/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 17/07/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 18/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.SABA SABA MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 16/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 17/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 20/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI | 21/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | HELENA ANTONY HALENGO | NYUMBA | MARIA ANTHONI SKAWEWE | ILEMI | 21/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | NYUMBA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | TEMBELA | 17/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHARLES SIMON MALOMELE | NYUMBA | CHARLES SIMON MALOMELE | NDACHI-DODOMA | 18/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI- MSAKUZI | 26/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ELIZABETH SHAURI ULOMI | GARI (TOYOTA ALPHARD T 559 DWV) | ELIZABETH SHAURI ULOMI | POSTA HOUSE-ILALA | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | YASINTA CLEMENT SANGA | 1.NYUMBA 2.KIWANJA | 1. JOYCE BOAZ KOYA 2. YASINTA CLEMENT SANGA | 1.PUGU 2.MAGOLE MZINGA | 30/07//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELYKWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA | 27/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | YOHANA BRUNO SHAYO | NYUMBA | WILSON ELICHILIA MBOYA | BOKO | 22/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MUSSA MATHIAS SHIJA | NYUMBA | MUSSA MATHIAS SHIJA | UDINDIVU BAGAMOYO | 22/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | NYUMBA | LAMECK JOHN RUGIGA | KIBAMBA MBEZI | 26/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | LATIFA MOSHI MLANZI | NYUMBA | SALUMU OMARI AMIRI | MWANDEGE - MKURANGA | 27/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | OSCAR ELIAMINI CHUWA | NYUMBA | FLORA ELIAMINI CHUWA | MBAGALA KIZUIANI | 27/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ELISANTE BERNAD MRTA | NYUMBA | ELISANTE BERNAD MRTA | KIGAMBONI | 26/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | DICKSON CHRISTIAN NGEMELA | NYUMBA | DICKSON C. NGEMELA | KIMARA | 29/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | NYUMBA | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | TEGETA 'A' | 25/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | NEEMA FELIX MSIMAMI | NYUMBA | NEEMA FELIX MSIMAMI | LUGWADU MKOKOZI | 26/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA BAKARI BENDERA | NYUMBA | FATUMA BAKARI BENDERA | VIKAWE | 22/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SASI SELEMANI KITUNDU | NYUMBA | MWAJUMA SELEMANI KITUNDU | GOBA | 25/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | BERTHA DAMIAN WIKEDZI | NYUMBA | BERTHA DAMIAN WIKEDZI | GOBA | 25/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR. ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | BEATRICE PETER KESSY | NYUMBA | ALEXANDER MUSSA SINDOMA | PUGU | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA ATHUMANI MBARUKU | NYUMBA | EMELDA E. MPAGAMA | MALAMBA MAWILI | 29/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | VIWEGE MAJOHE | 22/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JUMA ALLY NGAWANAE | NYUMBA | JUMA ALLY NGAWANAE | MABWE PANDE | 25/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MUSSA INANO CHACHA | NYUMBA | HABIBU MUSSA MACHOROKO | MBAGALA KWA NYOKA | 27/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MOSES YARED CRY | NYUMBA | MOSES YARED CRY | ZAVARA BUYUNI | 25/07/2024 Kuanzia saa 4 asubuhi na Kuendelea |
| TEGETA | ANDREW SAMSON GESURURA | NYUMBA | ANDREW SAMSON GESURURA | BOKO | 25/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | YASIN MICKIDADI MICKIDADI | NYUMBA | SHAMSA SAIDI MOHAMED | MZINGA TOANGOMA | 27/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 19/07/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 16/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0714939933/0759648448/0715868000/0765999000/0714208208
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Majaliwa awaweka vigogo 'kitanzini' utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu,**
IRINGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza miradi yote inayojengwa kwa fedha za serikali ikamilike ndani ya mwaka huu na ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi na viongozi mbalimbali katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye Uwanja wa Mwembetogwa, mjini Iringa.

Alisema uimara wa serikali yoyote ni pamoja na kuwapo watumishi wa umma na kupitia wao, serikali inafuatilia mahitaji ya wananchi kwenye maeneo yote.

"Serikali yenu chini ya Dk. Samia Suluhu Hassan inaendelea kufuatilia mahitaji ya wananchi. Katika kufuatilia, tumezihusisha halmashauri za wilaya kote nchini kuhakikisha zinawafikia kwenye vijiji mlipo, mnaeleza matatizo mliyonayo na wao wanaratibu kwa kuanza utatuzi wa kero zinazowagusa kwenye maeneo yenu," alisema.

Waziri Mkuu pia alitoa fursa kwa naibu mawaziri na wabunge waliokuwapo kwenye mkutano huo ambao waliambatana naye kwenye ziara ya siku nne mkoani humo, kueleza miradi iliyotekelezwa na serikali katika mkoa huo.

Awali akizungumza na wananchi waliohudhuria mkutano huo kabla ya kumkaribisha Waziri Mkuu azungumze nao, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba alishukuru serikali kwa kupeleka fedha nyingi za miradi katika sekta mbalimbali zikiwamo za maji, afya, elimu, barabara, mawasiliano ya simu na nishati.

Akitoa mfano katika sekta ya miundombinu, Mkuu wa Mkoa alitaja baadhi ya barabara zitakazojengwa kwa kiwango cha lami zikiwamo za kutoka Ipogolo hadi Kilolo (Km. 33); Mafinga-Mgololo (Km. 80); mchepuo wa Mji wa Iringa Km 7.3 - (Iringa Bypass) na uboreshaji barabara ya Mlima Kitonga (Km saba).

"Pia tumepata Sh. bilioni 50 kupitia TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (wao wanahudumia mtandao wa barabara nyingi za vijijini)," alisema.

Kuhusu hali ya mawasiliano katika Mkoa wa Iringa, Serukamba alisema hadi kufikia Juni, 2024 ni vijiji 11 tu vilivyobaki bila kufikiwa na mawasiliano ya simu kulinganishwa na vijiji 22 kati ya 360 vilivyokuwa havijafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu mwaka 2021.

Alitaja vijiji hivyo 11 kuwa ni Ihimbo, Chogo, Ukami, Uhafiwa, Mpangatazara, Kitumbuka, Mwambao, Itimbo, Makota, Masisiwe na Mgowelo.

Kuhusu nishati ya umeme, Serukamba alisema serikali imetoa Sh. bilioni 71.05 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme katika mkoa wa Iringa ambapo hadi sasa vijiji vyote 360 vimepatiwa umeme.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, mkoani Pwani, Dk. Rogers Jacob (kulia), akikabidhi sehemu ya misaada ya vyakula na vifaa vya shule kwa Mkurugenzi wa Kituo cha kulelea watoto yatima Shalom, Lilian Mbise, katika Kata ya Msangani, iliyotolewa na watumishi wa halmashauri hiyo na Shirika la Elimu Kibaha mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Apandishwa kizimbani kwa mashtaka ya kulawiti mtoto

**Na Jumbe Ismailly,**
SINGIDA

MKAZI wa Mtaa wa Sabasaba, Kata ya Utemini Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Norasko Severine Haule (56), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Singida, akikabiliwa na mashtaka mawili, likiwamo la kulawiti mtoto wa kike mwenye umri wa miaka sita.

Mwanasheria wa Serikali, Carene alidai mahakamani huko kuwa katika shtaka la kwanza la kunajisi, mwezi Desemba mwaka jana, Mtaa wa Sabasaba, Manispaa ya Singida, Norasko alinajisi mtoto wa kike mwenye umri wa miaka sita (jina tunahifadhi).

Katika kesi hiyo Na. 10282 ya mwaka 2024, Mwanasheria wa Serikali Carene alidai kuwa Norasko alilawiti mtoto huyo mwezi Desemba mwaka jana, Mtaa wa Sabasaba, Manispaa ya Singida.

Baada ya mshtakiwa huyo kusomewa mashtaka dhidi yake alikana kutenda makosa hayo.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa shauri hilo umeshakamilika, hivyo kuomba kupangiwa tarehe nyingine kwa ajili ya kesi hiyo kuanza kusikilizwa.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Singida, Fadhili Ruvinga alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa Julai 22 mwaka huu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 20 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Siku hiyo ya uzinduzi ndiyo itakuwa siku ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari Mkoani Kigoma, Tabora na Katavi kwa siku saba hadi tarehe 26 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 20 Julai, 2024 hadi siku ya Ijumaa tarehe 26 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 27 Juni, 2024 na:

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**





Nipashe
# MWANZA
Jumatano Julai 10, 2024
TOLEO MAALUM



# Sifa 10 za Mwanza, zikinyambuliwa na RC kulikoni kinara nyuma ya Dar

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

UNAPOUTAJA Mkoa wa Mwanza, una wakazi 3.66, 872; wanaume milioni 1,802,183 na wanawake milioni 1,897,689, jumla yao, wa pili kitaifa nyuma ya Dar es Salaam, penye wakazi milioni tano na kadhaa.

Mwanza kuna wilaya na idadi ya wakazi ndani ya mabano, kuanzia zilizoko jijini; Nyamagana (394,834) na Ilemela (509, 687).

Zingine ni Buchosa (413,110), Kwimba (480,025), Magu (421,119), Misungwi (467,887), Sengerema (425,415) na kisiwa cha Ukerewe (387,815).

Sifa zingine tisa zinazoendana nazo ni; unapofika jijini Mwanza, kumezungukwa na milima ya mawe, nyumba zimejengwa huko, pia kuna mabonde yanayotengeneza vivutio aina yake kufika ngazi ya utalii, wageni wanapagawa nayo.

Pia, mkoa unazungukwa na Ziwa Victoria, kunakobeba utajiri samaki wanaolisha mkoa na nje, pia ikibaki ajira kuu mkoani.

Kuna la nne, mkoa huo wa Magharibi, ni kitovu cha biashara kimataifa, mataifa jirani Afrika Mashariki, kama Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ndio soko lao kuu la kununua bidhaa za ziwani, wakiwamo samaki sato na sangara, wenye thamani kubwa.

Hiyo inaungana na biashara ya 'mabondo', sehemu ya utumbo wa samaki, malighafi muhimu katika uzalishaji bidhaa za plastiki China na mataifa ya kiasia.

Aidha, ziwani kuna wasifu wa sita, mtu anapata mboga 'fresh' kutoka ziwani kwa gharama nafuu, samaki sato, sangara na dagaa wametapakaa kila kona.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Said Mtanda. **PICHA: MAKTABA**

Hilo linaendana na la saba, Soko la Kimataifa la Dagaa, jijini humo likibeba uchumi wa Kanda ya Ziwa, kuhalalalisha jiji hilo linaloundwa na wilaya za Ilemela na Nyamagana, ikishika nafasi ya pili nyuma ya 'kigogo' Dar es Salaam yenye wilaya tano.

Tena, jijini Mwanza kama zilivyo wilaya za Makete na Rungwe kupakanishwa na milima ya kihistoria Livingstone (Mtafiti David Livingtone), katikati yake kuna mawe ya kihistoria ya ukoloni, 'Mawe ya Bismark.'

Wasifu namba Tisa, ni upekee wa utitiri wa viwanda vya kuchakata samaki kuhudumia soko kubwa, wakiwamo wateja kigeni.

Kiutalii, Mwanza inabeba sifa ya 10, kuwapo kisiwa Sanane, nguzo mojawapo ya utalii mkubwa nchini.

### UCHUMI WAKE

Nguzo ya uchumi wake ni Kilimo na Mifugo, zinazochangia asilimia 75 ya pato la mkoa, watu wengi wakishi vijijini.

Eneo lake ni kilomita za mraba 25,233, chini ya nusu nchi kavu, kilomita za mraba 11,796 au asilimia 47, huku kilomita 13,437 (53%) ni majini, Ziwa Victoria.

Sekta nyingine zinazochangia pato lake, kwa mujibu wa Taarifa ya Maendeleo ya Mkoa ni: Biashara, Mawasiliano, Usafirishaji, Benki, Elimu, Afya, Kodi ya Pango, Uvuvi, Ujenzi, Madini, Umeme na Uzalishaji zote zikichangia asilimia nane.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, mkoa huo una wakazi milioni 3,669,872,

Mkuu wa Mkoa huo, Said Mtanda, anaelezea uchumi wao umekuwa ukiongezeka kila mwaka kulingana na ongezeko la uzalishaji kisekta mkoani.

Taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) 2021, inaeleza pato hilo limekuwa likiongezeka kutoka Sh. trilioni 8.5 mwaka 2017 hadi Sh. trilioni 12.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la shilingi trilioni 3.7 ambayo ni asilimia 67.

Kadhalika pato la wnanachi kwa mwaka limeongezeka kutoka Sh. 2.507,924 mwaka 2017 hadi Sh.3,301,349 mwaka 2022, sawa na ongezeko la Sh.793,425, ambayo ni asilimia 31.6 katika kipindi hicho.

Ongezeko hilo la pato la kila mwananchi, linaonyesha wakazi wa mkoa wa Mwanza, kiuchumi wamevuka kiwango cha umaskini uliokithiri, chini ya Dola Moja ya Marekani (Sh. 2687.73).

### SEKTA YA KILIMO, MIFUGO

Katika sekta ya kilimo upatikanaji wa chakula msimu wa ulaji mwaka 2022/23 mkoa ulilenga kulima hekta 451,529.35 za mazao muhimu ya chakula, zilizotarajiwa kutoa mavuno ya 1,098,094.

Katika kuboresha mifugo, taarifa ya mkoa inafafanua, mkoa umepokea madume bora ya mifugo aina ya Borani 39 kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, yaliyosambazwa kwenye vikundi 37 vya wafugaji wilaya ya Sengerema kwa ajili ya uzalishaji.

Pia kuna mradi wa vituo vinavyowajengea vijana uwezo, ujasiri wa kutumia taaluma walizopata vyuoni, kuwekeza sekta ya mifugo kuanzia Septemba 2022 ukiwa na vijana 88.

Kutokana na wengine kupata ajira hivi sasa kituo kimebaki na vijana 55 wanaume 39 na wanawake 16 ambao wanaendelea na unenepeshaji ng'ombe na kuwauza, faida inayopatikana inakuwa yao.

Mradi huo ulianza na ng'ombe 900 na hadi sasa inatajwa wameshauza 753, huku Sensa ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 2019/20, idadi ya mifugo mkoani Mwanza inakadiriwa kuwa 1,721,518; mbuzi 1,395,000, kondoo 604,674,

**INAENDELEA UK.12**



# Maboresho ya kimkakati MWAUWASA yanavyorejesha matumaini kwa wananchi

**Na Vitus Audax,MWANZA**

UJENZI wa Mradi mkubwa wa Mitambo ya kuzalisha Maji ya Butimba pamoja na maboresho ya kimkakati katika miundombinu ya Maji mkoani Mwanza yaliyotekelezwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) umetajwa kurejesha matumaini kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma ya Maji safi na salama.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso anauhakikishia umma kuwa Wizara haitorudi nyuma katika kuhakikisha dhamira ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani inatimia ambalo ndilo lengo kubwa la Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Sisi kama Wizara hatutokuwa kikwazo kwa Watanzania kupata Majisafi, salama na yenye kutosheleza, tutapambana muda wote kuhakikisha miradi inajengwa kwa ubora unaotakiwa na inakamilika kwa wakati ili wananchi wapate huduma," anasisitiza Aweso

Aidha Aweso anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Jijini Mwanza ambao anasema umeanza kutoa huduma na hivyo kupunguza adha ya maji iliyokuwepo katika baadhi ya maeneo.

Anabainisha kuwa uelekeo wa Serikali kupitia Wizara ya Maji ni kujenga miradi ya maji ya kimkakati kwa kutumia vyanzo vya maji toshelevu hususan katika maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji ili kufikisha asilimia 95 ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ya mijini na aslimia 85 kwa maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2025.

"Tunamshukuru sana Rais wetu, Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha na tumefanikiwa kutekeleza mradi huu mkubwa ambao tayari tumeanza kushuhudia matunda yake katika baadhi ya maeneo hasa ikizingatiwa kuwa changamoto ya maji kwa Jiji la Mwanza hapo awali ilikuwa ni kubwa," anasema Waziri Aweso.

## HALI YA UPATIKANAJI HUDUMA YA MAJI

Mkoa wa Mwanza unategemea chanzo cha Ziwa Victoria kupitia maji yanayozalishwa katika vituo vitano vya Capripoint, Butimba, Nyahiti, Nebuye, Busulwa na Ihelele kilicho chini ya KASHWASA.

Vituo hivyo vinahudumia Jiji la Mwanza (Nyamagana na Ilemela), Miji ya Magu, Nansio, Misungwi, Ngudu na Mji mdogo wa Kisesa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Neli Msuya anasema kwa Jiji la Mwanza, uwezo wa mitambo ya kuzalisha maji kwa siku ni lita milioni 90 kutoka Capripoint na milioni 48 kutoka Kituo kipya cha Butimba huku uhitaji ukiwa ni zaidi ya lita milioni 170.

Anasema kwa sasa huduma ya maji katika Jiji la Mwanza imeimarika kutoka mgao wa siku moja kwa Wiki kwa baadhi ya maeneo hadi siku tano kwa Wiki huku baadhi ya maeneo migao imeondolewa hasa baada ya kukamilika kwa mradi wa chanzo kipya cha maji Butimba.

"Ili kuimarisha na kuboresha zaidi upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Mwanza, Mamlaka inatekeleza miradi midogo ya matokeo ya haraka maarufu kama "quick win" ili kusambaza maji yaliyoongezeka na kufikia wananchi,"anasema Neli.

## UTEKELEZAJI WA MRADI WA CHANZO KIPYA CHA MAJI BUTIMBA.

Kabla ya ujenzi wa mradi wa Butimba, Jiji la Mwanza na viunga vyake lilitegemea huduma ya maji kutoka katika chanzo cha Capripoint ambacho kinauwezo wa kuzalisha takriban lita milioni 90 kwa siku wakati huo mahitaji yakiendelea kukua kutokana na ongezeko la idadi ya watu na shughuli za kiuchumi ikiwemo viwanda.

"Kwa kutambua hili, Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kujenga mradi mwingine mkubwa ambao utakwenda kupunguza adha ya maji iliyokuwa inawakabili wananchi wa Jiji la Mwanza," anasema Neli

Utekelezaji wa Mradi wa Chanzo kipya cha Maji Butimba unaotekelezwa na Serikali kupitia Programu ya Uboreshaji wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira yaani "Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN)" umetajwa kufikia asilimia 100 na kuanza kutoa huduma ya maji ya uhakika katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mwanza huku maboresho ya miundombinu katika baadhi ya maeneo yakiendelea ili kufikisha

INAENDELEA UK. II




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Said Mtanda akikagua mitambo ya uzalishaji maji katika mradi wa Butimba, kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA Neli Msuya akitoa maelezo juu ya utendaji kazi wake.



Mabomba ya makubwa ya usambazaji maji yakishushwa kwaajili ya kuanza kulazwa katika baadhi ya mitaa



# Maboresho ya kimkakati MWAUWASA yanavyorejesha matumaini kwa wananchi



Waziri wa Maji Jumaa Aweso akipokea taarifa kuhusu Mradi wa mkubwa wa Mitambo ya kuzalisha Maji ya Butimba

INATOKA UK. I

huduma hiyo katika maeneo yote lengwa.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba wa fedha kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kupitia LVWATSAN kwa lengo la kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza, Miji ya Bukoba na Musoma, miji midogo ya Misungwi, Magu na Lamadi.

Kaimu Mukurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Neli Msuya anasema, Miradi inayotekelezwa kupitia programu hiyo katika Jiji la Mwanza na Miji iliyotajwa hapo juu, inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank - EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Francaise de Développement - AFD).

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Neli Msuya anasema Mradi wa Usanifu na Ujenzi wa Chanzo Kipya cha Maji na Kituo cha Kusafisha na kutibu Maji Butimba, umegharimu zaidi ya Euro milioni 31.17 ambayo ni sawa na zaidi ya Sh. Bilioni 71.7 "Mradi huu umetekelezwa ndani ya miezi 33 na Mkandarasi M/s. SOGEA SATOM JV M/s. VINCI CONSTRUCTION GRANDS PROJECTS (VCGP) kuanzia Februari , Mosi, 2021," anasema Neli.

Aidha anasema Mradi huo umelenga kunufaisha wakazi zaidi ya 450,000 kutoka katika maeneo ya Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Buganda, Luchelele, Lwanhima, Sahwa, Fumagila, Kishiri na Igoma katika Jiji la Mwanza. Pia maeneo ya Bujora, Kisesa na Kanyama Wilayani Magu.

"Kazi kubwa tulionayo sasa ni kuboresha mfumo wa usambazaji maji ili haya maji yanazozalishwa yaweze kuwafikia wananchi na tayari kazi za ulazaji wa mabomba kwa awamu ya kwanza zimefanyika katika maeneo ya Buswelu, Luchelele, Kahama na Kisesa. Katika awamu ya pili ya mradi huu, tunaenda kujenga matenki ya kuhifadhia maji maeneo ya Kisesa, Buhongwa, Fumagila, Nyamazobe na Usagara", anasema.

Anasema mradi huo ulianza kwa majaribio ya awali ya kutoa huduma ya maji kati ya Septemba 15 na Oktoba mwaka jana (2023) na maeneo yaliyoanza kupata huduma ya maji ni maeneo ya Sahwa ya chini, Igoma, Kishiri, Ndofe, shamaliwa, Nyamhongolo Kisesa, Kanyama na Bujora ambayo hapo awali yalikuwa yakipata maji mara moja kwa wiki.

Maeneo mengine yanayopokea huduma ya maji kutoka Butimba ambayo hivi karibuni mtandao wa usambazaji maji utaboreshwa ni Nyegezi, Mkolani, Malimbe na Luchelele "Mradi umekamilika na tumeanza kutoa huduma kwa maeneo yote yaliyokusudiwa kupata huduma kutokea kwenye chanzo hicho kipya cha Butimba na tunamshukuru sana Rais wetu kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu ", anasema Msuya.

### WANENAVYO WANANCHI.

Baadhi ya Wakazi wa maeneo ya Igoma mkoani hapa, ambao kwa muda mrefu walikuwa wakisumbuka na upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama wameeleza kuwa kwa sasa huduma hiyo inapatikana saa 24 mara baada ya Mradi huo kuanza kutoa huduma.

"Tulizoea kukosa maji kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja na muda mwingine tunapata huduma kwa mgao mkali lakini kwa sasa tumesahau hali hiyo kwani maji yanatoka kwa kasi na kwa wakati wote,"alisema Said Alsalmi

Katika kuhakikisha huduma ya maji inawafikia walengwa wote kwa wakati hususani wale wanaohudumiwa na chanzo cha Butimba, upanuzi pamoja na ulazaji wa mabomba makubwa unaendelea ili kufanya huduma hiyo kuwa ya uhakika kwa wananchi wote.

Mkurugenzi Msuya anaeleza kuwa mtandao wa usambazaji maji katika eneo la Buhongwa wilayani Nyamagana mkoani hapa unaendelea kuboreshwa ili kuwezesha wananchi kunufaika na mradi wa Butimba.

"Hatua za muda mfupi, tunazoendelea nazo ni pamoja na kulaza mabomba makubwa ya usambazaji maji kwa awamu katika Mitaa mbalimbali hususani yenye changamoto ili kuboresha mfumo wa usambazaji,"anasema Msuya.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ng'washi, Thobias Simon anaishukuru MWAUWASA kwa jitihada zake za kuhakikisha huduma katika mitaa hiyo inaimarika. Alisema miongoni mwa jitiahada hizo ni pamoja na kutembelewa mara kwa mara na Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA na kukabidhiwa mabomba kwaajili ya kuendelea kuyalaza katika mitaa hiyo ili huduma iwe ya uhakika.

### MRADI WA USAMBAZAJI MAJI

Aidha Msuya anasema katika kuhakikisha wanaweka uwiano sawa wa usambazaji maji, Mamlaka hiyo inatarajia kutekeleza Mradi mkubwa wa usambazaji maji ambako yatajengwa matenki makubwa matano.

"Matenki hayo yatakuwa na ujazo wa jumla ya lita milioni 31, ambapo yatajengwa katika maeneo ya Buhongwa, Fumagila, Usagara, Nyamazobe pamoja na Kisesa ambapo yote hayo utekelezaji wake utaanza muda siyo mrefu"anasema Neli.

Kadhalika Mkurugenzi Neli anasema mbali na upanuzi wa chanzo cha Butimba na ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji, Mamlaka hiyo inaendelea na upanuzi pamoja na maboresho ya chanzo cha Capripoint ili kuhakikisha kila eneo la Mwanza linapata huduma toshelevu ya maji.

### WANANCHI WAMPA 'TANO' MKURUGENZI KWA HUDUMA SHIRIKISHI.

Baadhi ya wananchi na watumiaji wa huduma ya maji inayotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) wamempongeza Kaimu Mkurugezi Mtendaji wa Mamlaka hiyo Neli Msuya kwa kufanya huduma hiyo kuwa shirikishi wakati wote.

Diwani wa Kata ya Lwanhima jijini Mwanza, Marko Swalehe anasema Mkurugenzi huyo amekuwa akifanya ziara za mara kwa mara katika kata hiyo kushuhudia maeneo yenye uhitaji wa huduma na kusaidia kutoa suluhisho la haraka. Anasema hivi karibuni alifika katika kata hiyo na kukagua huduma kisha kuzungumza na viongozi ili kupata suluhisho la urejeshwaji wa miundombinu iliyoathiriwa na ujenzi wa barabara ya Igoma-Buhongwa.

"Nimekuwa nikishirikishwa kila mara kuhusu mipango inayohusu miradi ya maji na kuwa hatua zinazoendelea katika kata hiyo ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji kwa awamu ili kuboresha mifumo hiyo,"alisema Swalehe.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ng'washi, Kata ya Buhongwa jijini Mwanza, Thobias Simon anasema, Mkurugenzi Msuya amekuwa akihakikisha anafika katika maeneo yenye uhitaji na kuwasiliana na viongozi kuona namna ya kuongeza wigo wa usambazaji maji katika maeneo husika.

"Hivi karibuni amefika na kutukabidhi mabomba yatakayoimarisha mtandao wetu wa maji, tunampongeza kwa hili na pia kwa mipango ya utekelezaji ambayo alitudokeza kuwa wanaendelea nayo. Tunaahidi kuendelea kushirikiana naye katika kufanikisha adhima ya serikali ya kuhakikisha inamtua mwanamke ndoo ya maji kichwani,"alisisitiza.

Mkazi wa Nyakagwe, Deogratias Juma aliipongeza MWAUWASA kwa kuanzisha huduma mtandao ambayo inasaidia kupokea na kutatua changamoto za mifumo ya maji kwa haraka na ushirikishwaji.

"Kwa sasa hatupati shida kuwafuata watoa huduma ofisini bali unaandika tatizo lako kupitia kundi sogozi la Whatsapp ambapo mtoa huduma wa eneo husika anafika kwa wakati na kutatua tatizo lililopo bila gharama zozote, huduma hii ni msaada mkubwa kwetu kwani unaweza kuhudumiwa hata kama haupo nyumbani,"alisema Juma.

Alisema kuna muda maji yanakosekana katika makazi yao lakini wakijulisha watoa huduma kupitia platifomu hiyo wanakuta hitilafu zipo katika mifumo karibu na maeneo husika hivyo kuzifanyia kazi haraka tofauti na ilivyokuwa hapo awali.



Picha ya juu ikionesha Mradi Mkubwa wa Mitambo ya kuzalisha Maji ya Butimba





# TCB na mikakati kuirejesha thamani ya 'dhahabu nyeupe'

**Na Vitus Audax, MWANZA**

TASNIA ya pamba ina mchango mkubwa katika kupunguza umaskini nchini ambapo inatajwa kulimwa na wakulima wadogo zaidi ya 500,000 katika eneo la takribani hekta 400,000.

Zao hili lililopewa jina la dhahabu nyeupe hulimwa katika mikoa 17 (wilaya 56) ya Tanzania iliyogawanywa katika kanda mbili Kanda ya Magharibi inayoundwa na mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Shinyanga, Tabora, Singida, Katavi, Kagera, Kigoma, Dodoma, Manyara.

Aidha kanda ya Mashariki ambayo inaundwa na mikoa ya Morogoro, Tanga, Iringa, Kilimanjaro na Pwani huku asilimia 98 ya pamba yote nchini inazalishwa katika kanda ya Magharibi ikitajwa kuwa miongoni mwa mazao sita ya kimkakati nchini yakiwemo korosho, tumbaku, kahawa, mkonge na chai.

Asilimia 75 ya pamba ya Tanzania inatajwa kuuzwa nje ya nchi na kuliingizia taifa fedha za kigeni huku asilimia 25 ikitumika katika viwanda vya nguo vilivyopo hapa nchini.

### MAENDELEO SEKTA YA PAMBA.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Marco Mtunga anasema katika misimu mitatu iliyopita matumizi ya pembejeo yameshuhudiwa yakiongezeka mara dufu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa eneo la uzalishaji pamba kutoka mikoa 15 hadi kufikia 17

Pia anasema Msimu wa kilimo 2022/23 matumizi ya viuadudu yaliongezeka hadi kufikia chupa 11,714,000 na kiasi cha chupa 16,000,000 zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima msimu wa kilimo 2024/25. Jitihada kubwa inafanywa na Serikali na kwa zaidi ya miaka 4 sasa kila msimu maghala ya Bodi ya Pamba yanakuwa na akiba ya kutosha ili kutoa huduma hiyo mapema kwa wakulima. Msimu ujao wa kilimo 2024/2025 unaoanza Katikati ya mwezi Novemba wakulima watakaowahi kupanda pamba watahudumiwa kwa wakati ambapo tayari akiba ya chupa 5,000,000 zimeshanunuliwa na kuhifadhiwa katika maghala ya Bodi ya Pamba

Anasema kuwa usambazaji wa mbegu bora za pamba umeongezeka kutoka tani 15,000 kwa msimu hadi kufikia tani 22,486 kwa msimu ongezeko lililochangiwa na mabadiliko ya nafasi ya upandaji na ongezeko la wakulima.

Aidha, anasema mikakati inayoendelea katika Bodi hiyo ni kuhakikisha wanafikia lengo la kuzalisha tani milioni moja ifikapo 2025. Kuhusu maboresho katika huduma za ugani eneo ambalo linatajwa kuwa na changamoto kubwa kwa wakulima, Mtunga anasema, Bodi hiyo imekuwa ikifanya juhudi za makusudi kupunguza changamoto za maofisa kilimo kushindwa kuwafikia wakulima kwa kuwapatia vyombo vya usafiri pamoja na mafuta.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Marco Mtunga, akifundisha wakulima wa pamba Kanuni 10 za kilimo bora cha pamba.

Mtunga anasema Jumla ya pikipiki 290 zilisambazwa kwa maofisa kilimo na wagani katika mikoa 11 kati ya 17 inayozalisha pamba vilevile kutokana na uhaba wa wagani jumla ya wakulima wawezeshaji 5,000 wamepatiwa mafunzo ya kanuni 10 za kilimo bora cha pamba.

Anasema wakulima hao wanaitwa wakulima wawezeshaji ambao wapo wawezeshaji wawili kila Kijiji na Bodi imejipanga kuwapatia baiskeli msimu huu ili waweze kuwafikia na kuwaelimisha wakulima wenzao.

Anasema kupitia utafiti uliofanywa na Tasisi ya Kilimo Nchini (TARI) kwa kushirikiana na wataalam kutoka nchini Brazili na kuja na vipimo vipya vya upandaji wa Pamba, Bodi hiyo ilifanikiwa kuvitambulisha katika msimu wa kilimo 2021/22 vimeonesha dalili njema kwa kuongeza uzalishaji kutokana na ongezeko la idadi ya miche katika ekari moja ya pamba kutoka 22, 222 za awali hadi 44,444 ambapo tunao wakulima wanavuna kilo 2,000 kutoka katika ekari moja

Asilimia 70 ya wakulima kwa sasa wanapanda kwa kutumia vipimo vipya vilivyotambulishwa ( sm 60 kwa sm 30).

### MKATABA WA UTAFITI, MNYORORO WA THAMANI

Katika kuendelea kuimarisha kilimo cha pamba nchini Julai 20, 2023, Serikali ya Tanzania na Brazil zilisaini mkataba wa mradi wa utafiti wa mbegu ya pamba, usalama wa chakula na masuala ya lishe (BEYOND COTTONP ROJECT) wenye gharama ya Dola za Marekani 930,118 sawa na Sh bilioni 2.1.

Mkataba huo ulikuwa na lengo la kuimarisha utafiti pamoja na kuongeza thamani ya pamba hapa nchini, ambapo nchi ya Brazil pekee inachangia Dola za Marekani 629,700, TCB inachangia dola za kimarekani 289,022 huku shirikisho la chuo kikuu Campina Grande (UFCG) cha nchini Brazili kikichangia dola za Marekani 11,396.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania, Marco Mtunga anasema kuwa mradi huo utanufaisha kaya zaidi ya 8400 na kuimarisha tija katika uzalishaji pamba.

Aidha, mradi huo utakuwa dawa kwa changamoto za zao hilo kwani kuna tatizo la mbegu za pamba zilizopo kushambuliwa na magonjwa na wadudu. "Lakini utafiti huu utawezesha kupatikana kwa mbegu bora ambazo zitanufaisha wakulima wetu kupata tija kubwa na hivyo kuimarisha uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla, anasema Mtunga.

### MIKAKATI YA TCB KUINUA THAMANI YA PAMBA.

Katika kuhakikisha zao la pamba linazidi kukuzwa nchini, Bodi ya Pamba Nchini (TCB) yenye makao makuu yake mkoani Mwanza imeweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha kilimo cha zao hilo na kuwawezesha wakulima kurejesha ari ya kulima zao hilo ambalo sasa linawakwamua kiuchumi.

Kwa kuzingatia malengo ya Serikali ya kuongeza uzalishaji wa pamba, Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Pamba imeandaa mikakati mahsusi ya kuongeza tija na uzalishaji wa zao la pamba ambapo Bodi imelenga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka wastani wa tani 300,000 kwa mwaka hadi kufikia tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2025.

Mtunga anasema ili kufikia malengo hayo, Bodi ya Pamba Tanzania imeelekeza nguvu zaidi katika maeneo makuu matano ya kimkakati ambayo ni teknolojia za uzalishaji, elimu ya kilimo bora cha pamba, usajili wa wakulima, utafiti na huduma za ugani kuimarisha mnyororo wa thamani, kujenga mazingira rafiki kwa sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika zao hilo. Uwekezaji katika maeneo haya matano unatarajiwa kuleta matokeo chanya kwa tasnia ya pamba na sekta nzima ya kilimo.

Aidha anasema ili uzalishaji, tija na ubora wa Pamba uimarike suala la upatikanaji wa pembejeo ni la msingi sana na Bodi imekuwa na utaratibu wa kuhakikisha kuwa pembejeo zote muhimu kama vile mbegu na viuatilifu vinamfikia mkulima kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu, Mtunga anasema pamoja na mikakati hiyo, TCB kupitia Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba (CDTF) hugharamia shughuli za utafiti wa zao la pamba kupitia vituo vya utafiti wa kilimo TARI vilivyopo Ukiriguru-Mwanza na Ilonga Kilosa-Morogoro ambapo kwa msimu wa 2022/2023 Sh. milioni 426 zimetumika kufanya tafiti mbalimbali kupitia vituo hivyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Marco Mtunga anasema baada ya utafiti kuja na vipimo vipya vya upandaji ambavyo vimeonesha matokeo kwa kuongeza tija kwa mkulima, wataalam kutoka katika vituo vya utafiti Ilonga na Ukiriguru wapo katika juhudi za kuja na mbegu mpya ya pamba ambayo inatarajiwa kutatua baadhi ya changamoto zilizopo katika mbegu inayotumika sasa aina ya UKM08.

Vilevile Mtunga anataja Mradi wa Beyond Cotton ambao utekelezaji wake umeanza Julai 2022, ukiwa na lengo la kueneza teknolojia ya kuongeza thamani katika bidhaa zinazotokana na pamba.

Anasema katika kuhakikisha zao hilo linakuwa tunu ya kuongeza mapato kwa Taifa na kumuinua Mkulima TCB imeweka mkazo katika baadhi ya maeneo katika mradi huo ambayo ni pamoja na kuchakata miti ya pamba (cotton Stalk) ili kutengeneza nishati ya kupikia (briquettes), kuchakata nyuzi za pamba kwa kutumia teknolojia rahisi (handloom) ili kutengeneza na kufuma nguo za mkono kama vile sweta, vikoi, vitambaa na nyinginezo ambapo utekelezaji wake unaendelea.

### ELIMU NA UBORESHAJI HUDUMA ZA UGANI

Kuhusu Elimu ya kilimo bora cha pamba Mtunga anasema, suala hilo ni miongoni mwa majukumu ambayo Bodi imekuwa ikiyatekeleza kwa muda mrefu ili kuwezesha uzingatiaji wa kanuni kumi za kilimo bora cha pamba kwa wakulima waweze kufikia kiwango cha tija kinachokusudiwa kufuatia mabadiliko na utambulishaji wa teknolojia mbalimbali mpya katika uzalishaji wa zao la pamba.

Anasema Bodi imeendelea kutumia mbinu mbalimbali katika ufikishaji wa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wadau wake ikiwemo balozi wa pamba Aggrey Mwanri ambaye amekuwa akiendesha kampeni yenye lengo la kuongeza tija katika zao hilo ambayo ilianza msimu wa kilimo 2021/22.

Katika kuongeza tija msimu wa kilimo 2021/22 Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ilizindua kampeni maalum ya uongezaji tija kwa njia ya kutoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima ikimtumia Balozi rasmi wa zao la Pamba nchini Aggrey Mwanri.

Anasema, tangu kuanza kwa kampeni za balozi hadi leo mikoa yote 17 na wilaya zake 56 zinazozalisha pamba zimefikiwa na wakulima kupatiwa elimu ya kanuni 10 za kuzingatia ili kuwa na kilimo cha pamba chenye tija pamoja na kuongezeka idadi ya wakulima wapya wa pamba wanaohamasika kupitia kampeni hizo

Anasema mkakati na kampeni za balozi wa pamba ni endelevu katika kila msimu kufanyika kwa kuzingatia kalenda ya misimu ya kuanza kilimo cha pamba.

Anasema pamoja na hatua zilizochukuliwa kwa ujumla, kwenye zao la pamba katika msimu wa kilimo 2023/24, jumla ya Maafisa kilimo 280 waliajiriwa kwa kushirikiana na kampuni zinazonunua pamba. Kata 40 zilitumika kama eneo la majaribio ambapo kila kata ilipata Maafisa Ugani watano (5). Kata hizi zimeshuhudia kila kijiji kiliweza kupata Afisa Ugani ambaye aliwezeshwa usafiri, mafuta na hivyo kuweza kuwafikia wakulima kwa karibu zaidi.

Katika utekelezaji wa mpango huu yafuatayo yamebainika:

(i) Takwimu za idadi ya wakulima zinazotoka kwenye Halmashauri zina dosari ya kuwa ni wengi kuliko uhalisia hali inayopelekea matumizi

INAENDELEA UK. IV



# TCB na mikakati kuirejesha thamani ya ‘dhahabu nyeupe’

INATOKA UK. III

makubwa ya pembejeo
(ii) Eneo linalolimwa ni kubwa kuliko uhalisia;
(iii) Mahitaji ya pembejeo ni makubwa kuliko uhalisia;
(iv) Wakulima wamefurahia huduma iliyotolewa na Maafisa Ugani; na
(v) Tija imeongezeka katika vijiji vilivyoshiriki katika mpango huu wa kuboresha huduma za ugani.

Kwa kuzingatia tulichokishuhudia katika msimu wa kilimo wa 2023/24, jumla ya Maafisa kilimo 500 wataajiriwa katika msimu wa 2024/25 ili kupanua wigo wa utoaji huduma za ugani kwa ufanisi katika maeneo yanayolima pamba. Mtunga ameongeza kuwa hivi karibuni Serikali itaanza zoezi la usajili wa wakulima wa pamba nchi nzima ikiwa kama mojawapo ya njia itakayopatia ufumbuzi tatizo la kutokuwepo kwa taarifa na takwimu sahihi za wakulima wa pamba hivyo kuwezesha huduma zinazotolewa ziwafikie walengwa ambao ni wakulima wa pamba halisi.

Aidha anasema katika kuhakikisha wanawafikia kwa elimu wakulima wote wa pamba nchini ambao wamesambaa katika mikoa 17, wilaya 56, halmashauri 64, kata 600 na vijiji 2,200 wakikadiriwa kufikia 600,000, Bodi inatumia njia ya vyombo vya habari ili kuweza kuwafikia ikiwemo matumizi ya redio pamoja na televisheni.

Anasema Bodi imekuwa na utaratibu wa kuandaa na kurusha vipindi vya redio na televisheni vinavyotoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima katika vipindi tofauti kuzingatia kalenda ya kilimo cha pamba kuanzia uandaaji wa mashamba mpaka ununuzi na uuzaji wa pamba

“Matangazo pamoja na vipindi hivi vya elimu vimekuwa na mchango mkubwa kwa wakulima wa pamba kupata elimu ya kilimo bora cha pamba pamoja na kuweza kuongeza wakulima wapya ambapo baadhi ya wilaya ambazo hazikuwa zikilima pamba hapo kabla zimeanza kutambulisha zao la pamba kama mojawapo ya mazao yake ya kibiashara kuanzia msimu wa kilimo 2022/23.

### MATUMIZI YA NDEGE NYUKI KUDHIBITI WADUDU WAHARIBIFU WA PAMBA

Katika kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kilimo cha pamba, Mtunga anasema, Wakulima wengi wamekuwa wakipambana na wadudu waharibifu wa pamba kwa kutumia mbinu mbalimbali za upuliziaji ikiwemo vinyunyizi vya kubeba mgongoni au vinyunyizi mbeleko.



Afisa kilimo wa Bodi ya Pamba akitoa elimu ya kudhibiti wadudu kwa wakulima.

Ambapo matumizi ya vinyunyizi mbeleko yamekuwa ni changamoto kwa wakulima wenye mashamba makubwa kwani inawalazimu kutumia muda mrefu na nguvu kazi nyingi kunyunyizia pamba shambani

Anasema kufuatia hali hiyo ililazimu serikali kuona namna ya kukabiliana na changamoto hii kwa kuwahamasisha wakulima wenye mashamba makubwa na walio na utayari kulima mashamba makubwa waweekeze zaidi katika kilimo cha pamba kwa kutambulisha teknolojia ya upuliziaji kwa kutumia ndege nyuki au ndege zisizo na rubani.

Mtunga anasema katika msimu wa Kilimo 2022/23 serikali kupitia Bodi ya Pamba ilinunua ndege nyuki 20 kwa ajili ya shughuli ya unyunyiziaji viuadudu katika mashamba ya pamba. Ndege hizo zinatajwa kuwa na uwezo wa kunyunyiza ekari 15 hadi 20 za shamba la pamba kwa moja wa saa moja. Aidha katika msimu wa kilimo 2024/2025 Bodi inatarajia kuongeza ndege nyuki kutoka 20 hadi kufikia 60 ili kuongeza idadi ya wakulima na eneo litakalopata huduma ya upuliziaji viududu

### MATUMIZI YA ZANA ZA KISASA ZA KILIMO ; JEMBE LA PALIZI LA KUKOKOTWA NA WANYAMA KAZI NA TREKTA

Inaelezwa kuwa Wakulima wa pamba kwa asilimia 100 wanatumia njia ya palizi kama mbinu pekee kudhibiti magugu katika mashamba na kwa wastani palizi hufanyika kati ya mara 2 hadi 4 kwa msimu kwa kutumia jembe la mkono.

Aidha kwa kutumia jembe la mkono mkulima wanatajwa kulazimika kutumia watu sita hadi tisa kwa saa moja ili kupalilia eneo la ekari moja. Hali hii husababisha mkulima kuingia gharama kubwa katika uzalishaji na hivyo huathiri kipato chake.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Bodi ya Pamba ilitambulisha matumizi ya jembe la palizi linalokokotwa na wanyama kazi ili kumrahisishia mkulima shughuli nzima ya palizi na kumpunguzia gharama za uzalishaji.

Mtunga anasema hadi sasa Bodi hiyo imesambaza majembe ya wanyama kazi 2,000 kwa wakulima pamoja na kununua na kusambaza majembe 1,500 kwa wakulima wa pamba ili kuwafikishia wakulima wote wenye uhitaji.

“Aidha, kama ilivyo katika palizi pamba kwa miaka mingi imekuwa ikipandwa kwa kutumia jembe la mkono huku ikitumia watu takribani watano hadi tisa kwa saa moja kukamilisha upandaji kwenye eneo la ekari moja hali hii imekuwa ikiwafanya wakulima wengi kushindwa kulima mashamba makubwa kwa kuzingatia kuwa msimu wa upandaji wa pamba huenda sambamba na upandaji wa mazao mengine yanayotegemea mvua kupanda,”

“Bodi imekusudia kutatua changamoto hii kwa kutambulisha matumizi ya jembe la kupandia la kukokotwa na wanyama kazi ambalo litamwezesha mkulima kutumia nguvu kazi kidogo na muda mfupi katika shughuli ya upandaji. Tutanunua na kusambaza majembe 500 ya majaribio kwa wakulima wakubwa wa pamba kanda ya magharibi na kanda ya masharikí, anasema Mtunga.

Serikali kupitia wizara ya kilimo imekuja na ajenda mahsusi ya kuipaisha sekta ya kilimo kukua kwa takribani asilimia kumi (10%) ifikapo 2030, sambamba na kukifanya kilimo kibiashara badala ya kuishia kujikimu tu.

Sekta ndogo ya pamba inaenda sambamba na ajenda hii ya serikali kwa kuhakikisha kuwa pamba linakuwa zao la kuvutia wakulima na wadau wengi zaidi.

Mtunga amesema Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na wadau Msimu wa kilimo 2023/2024 ilinunua trekta 200 lengo ikiwa ni kuhamasisha wakulima kuongeza maeneo ya uzalishaji sambamba na tija katika zao la pamba ili kwenda sambamba na ajenda ya ukuaji wa sekta ya kilimo nchini. Mkakati huu ni endelevu ambapo katika msimu ujao wa kilimo trekta nyingine 200 zinatarajiwa kununuliwa kwa ajili ya wakulima wa pamba kupanua eneo la uzalishaji sambamba na kila wilaya kutenga maeneo ya kimkakati yatakayosimamiwa na halmashauri za wilaya husika kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Pamba

Mikakati tajwa ina lengo la kuongeza zaidi tija kwa mkulima wa pamba na kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa ni shughuli inayovutia kundi na rika tofauti kwa kuhusisha matumizi ya teknolojia na nyenzo mbalimbali kuendanana na mabadiliko ya sayansi teknolojia.

### UJENZI MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI

Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuzingatia kuwa kilimo hapa nchini kwa kiwango kikubwa kinategemea mvua, Mtunga anasema, Bodi ya Pamba inatarajia kuendesha mradi wa utengenezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yatakayotengwa kimkakati kufuatia uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamba kwa wilaya zitakazotambulishwa

Mkurugenzi Mkuu amesema kuwa mitambo ya uchimbaji mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji tayari imeshaagizwa na Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Pamba kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo 2024/2025

### MATUMIZI YA MBOLEA HAI KATIKA UZALISHAJI

Kilimo cha pamba kama kilivyo kilimo cha mazao mengine kinahitaji matumizi ya mbolea za kupandia na kukuzia ili kuongeza tija, uzalishaji na kipato kwa mkulima. Kwa tasnia ya pamba matumizi ya mbolea za viwandani bado yapo chini kutokana na uwezo mdogo wa kiuchumi wa wakulima wa pamba kujinunulia bidhaa hii. Wakulima wengi wanatumia mbolea ya samadi ambayo inapatikana kwa gaharama nafuu sana kupandia pamba kwenye mashamba yao.

Mkurugenzi Mkuu Mtunga amebainisha nia ya Bodi ya Pamba kuwa sambamba na wakulima kuongea tija kupitia uhamasishaji wa matumizi ya mbolea hai ya kukuzia pamba itakayoongeza kiasi cha mavuno kwa mkulima.

Mtunga anaendelea kuelezea kuwa katika msimu wa kilimo wa 2023/24 Bodi ya Pamba imeanza kutengeneza mbolea hai ambayo inatumia malighafi inayopatikana katika mazingira ya wakulima. Mbolea hii ambayo ni matokeo ya ushirikiano wa Tanzania na Brazil kupitia mradi wa “Cotton Victoria” imeonesha ufanisi mkubwa katika kuongeza idadi ya matunda na ukubwa wake. Katika msimu wa 2024/25 mpango uliopo ni kutengeneza mbolea ya kutosha ekari 1,000,000 ambayo itasambazwa kwa wakulima ili kuongeza tija. Gharama ya mbolea kwa ekari ni shilingi 7,500 hii inajumuisha kununua “micronutrients” kama boron, magnesium na zinc ambazo ni muhimu kwenye uwekaji matunda katika zao la pamba.

### MBEGU BORA ZA KUPANDA

Mkurugenzi Mkuu wa TCB anawakumbusha wakulima wote wa pamba nchini kuzingatia maelekezo ya wataalam ikiwa ni pamoja na matumizi ya mbegu bora ya za pamba inayojulikana kwa jina la UKMO8 ili kuwasaidia kufikia malengo yao katika kilimo hicho.

“Mbegu ni moja kati ya pembejeo muhimu inayopewa kipaumbele katika tafiti za kilimo zinazofanyika nchini. Mbegu mpya aina ya UKMO8 iliyogunduliwa mwaka 2008 na kuanza kutumika kikamilifu msimu wa 2018/19 ina sifa kubwa 5 ukilinganisha na mbegu nyingine zilizopo,”

“Mbegu hii ina uwezo wa kuzalisha zaidi ya kilo 1,200 kwa ekari huku ikiwa na uwiano mkubwa wa nyuzi ambaa ni asilimia 42 ukilinganisha na mbegu nyingine. Pamoja na mafanikio hayo, watafiti wamebaini kuwepo kwa kasoro kadhaa ambazo zitapatiwa majibu kwa kutambulisha mbegu mpya yenye ubora zaidi kwa wakulima wa pamba,” anasema Mtunga.

Anasema kuwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, kumezuka wadudu wafyonzao pamba ambao hapo awali hawakuwa tishio lakini kwa sasa wamekuwa ni tishio kubwa kwa ustawi wa zao la pamba na kuwa wadudu hao wamesababisha kuongezeka kwa matumizi ya viuadudu zaidi ya mara tatu na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji.

Mtunga anataja Suluhisho la muda mfupi la tatizo hilo kuwa ni pamoja na kutafuta aina za viuadudu ambavyo vinaweza kuua aina hizo za wadudu na suluhisho la muda mrefu kuwa ni watafiti kutafuta mbegu ambayo kwa asili itakuwa na uwezo wa kujilinda dhidi ya hao wadudu.

“Kama ilivyo mbegu hii ya UKMO8 ambayo ilipatikana baada ya kuzifanyia utafiti mbegu toka Ukiriguru Tanzania na mbegu toka nchi ya Mali, vilevile mbegu hii mpya inaendelea kufanyiwa utafiti kwa kuchanganya baadhi ya vinasaba vya mbegu za hapa nchini na mbegu nyingine kutoka Pakistan ambao ni moja kati ya nchi wazalishaji wakubwa wa pamba duniani,”

“Mbegu hii mpya inayofanyiwa utafiti itakuja na faida kuu tatu ikiwemo ukinzani dhidi ya wadudu wafyonzao, ustahimilivu dhidi ya ukame wa muda mrefu na mavuno mengi kwa mkulima na ubora wa nyuzi,” anasisitiza.

# Siri DCP Mutafungwa kuufanya Mkoa Mwanza shwari kona zote

## •Mkazi aipa nyumba yake Polisi

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

KATIKA safu ya kikosi kinachotumikia usalama wa raia na mali zao - Polisi, kuna jina maarufu, Naibu Kamishna wa Polisi Wilbroad Mutafungwa.

Si miaka mingi, alikuwa akishika Kikosi cha Usalama Barabarani kitaifa, sasa wasifu huo uko Kanda ya Ziwa kusimamia usalama wa makao makuu hayo ya kanda na utajiri kitaifa, jiji la pili kwa ukubwa kitaifa.

Mutafungwa, aliye mweledi kufafanua, anaorodhesha mbinu anazotumia kutunza usalama Mwanza, anadokeza baadhi ni; elimu ya umma, intelijensia, doria, madawati ya polisi na usalama shirikishi.

Katika kufanikisha, Mutafungwa anaiambia Nipashe katika mazungumzo maalum, kuwa wanatekeleza kwa vitengo vyake, baadhi ni: Usalama Barabarani, Upelelezi Polisi, Kikosi cha Mbwa, Farasi, Wanamaji na kawaida, huku akitaja staili ya viashiria kutokomezwa ushirikishaji wananchi, wakiwafichua wahalifu.

### VINAVYOMLETEA MAFANIKIO

Mutafungwa, anajinasibu kwa lugha 'amani na utulivu vimeshika namba moja mkoani,' akiorodhesha viashiria vyake, anaidokeza mojwapo mradi wa kiintelijensia, kila kata amepangiwa polisi, anayealimisha usalama jamii.

"Kuwafanya wananchi wawe karibu na jeshi la polisi, uimarishaji vikundi vya ulinzi shirikishi kila mtaa, vijiji, kata, kuhusishwa kampuni binafsi za ulinzi, kuzipa mafunzo stahiki ikiwamo elimu, kufanya doria za miguu, boti ziwani na magari kila siku," anafafanua.

Eneo lingine analitaja ni kuanzishhwa vikundi ulinzi shirikishi vya kata, sasa vinaleta tija mkoani, taarifa za uhalifu zinaendelea kutolewa kwa jamii wakitumia vyombo vya habari kama radio, televisheni, mikutano ya hadhara mijini na vijijini, kata na makundi mengineyo.

"Elimu imekuwa ikitolewa hadi kwa wanafunzi shule za msingi, sekondari, vyuo vidogo na vikuu, waendesha bodaboda, waganga wa jadi, madereva vyombo vya moto, mama lishe, wavuvi, walinzi kampuni binafsi, yakiwamo makundi maalum na watu wenye uhitaji," anasema.



Kamanda Wilbroad Mufafungwa. **PICHA: MAKTABA**

### POLISI NA JAMII

Mutafungwa, aliye mweledi kufafanua, anataja magumu yanayomkabili ni wananchi kujichukulia sheria mkononi, madai ya imani za kishirikina zinzotatuliwa kwa elimu, hata wananchi wanaiamini polisi.

Mutafungwa anakumbusha, kuanzishwa Kitengo cha Polisi Jamii, pia ushirikiano na wananchi, ina kazi ya kujenga mema kati ya makundi hayo, wananchi washiriki kutanzua changamoto za uhalifu kwenye maeneo yao.

Pia, anataja utoaji taarifa za kuwafichua wahalifu, uhalifu, viashiria vyake, mafunzo kwa vikundi vya ulinzi shirikishi, namna ya kujilinda, mbinu za kukamata wahalifu kupitia madawati ya uelimishaji ngazi za wilaya na mikoa.

Mkoani Mwanza, Mutafungwa anasema Polisi kupitia vitengo vyake, imeweka utaratibu wa kukutana na makundi ya wananchi, ikiwafanyia uwezeshaji mkubwa, ushawishi, elimu ya polisi jamii ili washirikiane, akijigamba 'inafanyika kwa weledi mkubwa.'

Anatumia mfano, katika ngazi za wilaya na mikoa, wanakutana na wenye maduka makubwa, kati na kawaida, kusikiliza changamoto zao za kihalifu kazini, hata wakazitafutia ufumbuzi.

Anaeleza madawati hayo yamepanua wigo wa kuelimisha viongozi wa vikundi shirikishi mkoani Mwanza, wakiwafikia viongozi wa Kanda ya Ziwa, kuweka mikakati ya kudhibiti mauaji, hasa yatokanayo na imani za kishirikina, akitaja vyanzo kama migogoro ya ardhi ni tatizo mojawapo.

Kundi la wafanyabiashara tiba asili, analitaja nalo limo katika makundi ya kuelimishishwa na dawati hilo, wawekezaji hao wakielezea yanayowakabili katika shughuli zao, wanapewa elimu ya madhara za ramli chonganishi zinazofanywa na baadhi waganga asili wasio waadilifu.

Mkakati wa kushirikisha jamii kuzuia na kutanzua uhalifu, umesaidia kupata undani wa changamoto zinazowakabili wananchi kutokana na jiografia ya mkoa, matokeo yake unafungua na kuwafichua wahalifu, pia uhalifu unaojumuisha matukio ya kikatili.

Lingine linatajwa ni kuongezeka doria na misako kwa washukiwa wa matukio wanaotiwa mbaroni, akisema wananchi wanaelewa tafsiri za jukumu ulinzi na usalama mkoa kuwa la kila mtu. Hapo anaweka darasa ligine la makundi ya wanawake, watoto pia vikongwe.

Polisi Mwanza, inayakumbuka mauaji ya wenye ualbino, ukatili waliofanyiwa kwa kukatwa viungo kupitia imani potofu kusaka utajiri, nayo Mutafungwa anayataja yamekomeshwa.

Anaeleza maeneo mengine ya ushirikina yanahusisha kilimo katika dira za kunufaika kwa ufugaji na uchimbaji madini, polisi ikielekeza nguvu kudhibiti uhalifu huo, akijinasibu njia inayotumika 'ni ya kiitelejensia.'

Lingine analitaja ni doria na operesheni kufanyika Ziwa Victoria, nchi kavu doria, ni vipaumbele vya Polisi Mwanza na jeshi hilo, akinena wahusika 'hawatoboi.'

Katika ulingo wake wa zamani, Usalama Barabarani, Mutafungwa anasema kwa miezi mitatu, Januari hadi Machi, wamepunguza ajali kutoka 16 mwaka jana, ikinganisha na mwaka huu 13.

### JINSIA NA WATOTO

Katika Dawati la Jinsia na Watoto, Januari hadi Machi Polisi imeendelea kutokomeza ukatili kwa wanawake na Watoto, ikihusisha wadau; asasi za serikali na binafsi.

Mutafungwa anataja takwimu za mwaka huu, matukio yamepungua kufikia 358 kutoka 495 yaliyoripotiwa mwaka jana, sawa na asilimia 27.6.

Anakiri imetoa hamasa kwa wananchi kuona umuhimu vituo vya polisi katika maeneo yao, hata kuwapo tukio mkazi wa kisiwa cha Gana, anatajwa kujitolea nyumba akaikabidhi kwa polisi, itumike kuwa kituo cha polisi kisiwani humo.

Anajumuisha kuwa mkoa Mwanza hadi sasa umepunguza makosa ya uhalifu kwa asilimia 33.21, ajali za barabarani na vifo kwa asilimia 18.7

# SIFA 10 ZA MWANZA, ZIKINYAMBULIWA NA RC KULIKONI KINARA NYUMA DAR

**INATOKA UK. 9**

nguruwe 171,355 na kuku 3,400,947.

### SEKTA YA VIWANDA

Mkoa wa Mkoa Mwanza, Said Mtanda, anasema katika Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Biashara 2023, viwanda vimegawanywa katika makundi manne; vidogo sana, vidogo, kati na viwanda vikubwa.

Anataja makundi hayo ni mtaji wenye wafanyakazi, Mwanza kukiwapo jumla viwanda 1,922; vikiwamo vikubwa 119, vya kati 183, vidogo 291, vidogo sana 1,329.

Anavitaja vuinahusu; samaki, vinywaji baridi, vyakula, kuchenjua na kusafisha madini, plastiki, mabati, kuchambua pamba, vyakula vya mifugo, kusindika nafaka, nguo, nyama, viwanda vidogo vinavyosindika viungo,na vya maziwa.

Mtanda anasema, mkoa huo fursa ya uchakataji na usindikaji bidhaa za ngozi zinazozalishwa katika Machinjio ya Nyakato jijini Mwanza, zikiharibika kwa kukosa teknolojia ya kuzihudumia.

### SEKTA BIASHARA

Ufafanuzi wake Mkuu Mkoa, kuna jumla ya biashara zenye leseni 29,606, kati ya hizo 28,937 zinatokana na mamlaka za serikali za mitaa na leseni 669 za kundi A, zinatolewa na sasai ya Brela kwa biashara.

Hapo inagusa taasisi na biasahra za fedha, madini, afya, elimu, maduka, uingizaji bidhaa kutoka nje ya nchi, kutoa bidhaa nje na mawasiliano.

Pia, anataja kuwapo masoko 77 mkoani, mengine yamejengwa kwa ubia wa wananchi kushirikiana na serikali, akifafanua ni idadi pungufu, kulinganisha na mahitaji, ilali wafanyabiashara wanaongezeka kila siku hususani kutoka kundi la machinga.

### SEKTA ELIMU

Katika sekta Elimu, Mwanza taarifa yake inafafanua, kuna Elimu ya Watu Wazima kuwainua walioacha shule kwa sababu mbalimbali, kukiwapo vituo 19 vyenye wanafunzi 485 wanaoendelea na masomo ya sekondari.

Vilevile kunatajwa vituo 12 vya ufundi stadi, vyene vijana 1847 waliomaliza elimu ya msingi na sekondari, wavulana 1,111 na wasichana 7,736, wanaosoma; ufundi seremala, chuma, uashi, kompyuta, umeme, ushonaji na upishi.

Pia, zipo programu kuboresha Elimu ya Sekondari na kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu.



## 1939 - 2024 - UWEKEZAJI MPYA BN. 18.6/-...

# Meneja Lugenge: Tunakarabati, kupanua Bandari Mwanza kushika biashara Victoria

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

BANDARI ya Mwanza Kaskazini, ni miongoni mwa Bandari kubwa sita zilizopo ziwani Victoria, chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Zingine zinajumuisha; Mwanza Kusini, Bukoba, Kemondo Bay, Nansio na Musoma.

Bandari hiyo ilijengwa mwaka 1939, zama za utawala wa kikoloni nchini, mahusus kwa ajili ya kuhudumia abiria na mizigo midogo, ikiunganisha usafiri wa reli kwa usafiri kuelekea mikoa ya Kagera, Mara na nchi jirani za Kenya na Uganda.

Katika sehemu ya Mwanza, kuna bandari kubwa mbili ambazo ni Mwanza Kaskazini na Mwanza Kusini, maalum kwa ajili ya kuhudumia shehena za mizigo.

Hivi sasa kuna upanuzi na uboreshaji Bandari ya Mwanza Kaskazini, kukidhi mahitaji ya huduma zinazotolewa na bandari hiyo, inayohudumia abiria na mizigo midogo.



Meneja Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kanda ya Ziwa Victoria, Erasto Lugenge (aliyevaa kofia na mavazi ya kazi), akiwa kazini. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

**UPANUZI UNAOENDELEA**

Meneja Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania (TPA), Kanda ya Ziwa Victoria, Erasto Lugenge, anaelezea upanuzi na uboreshaji Bandari ya Mwanza Kaskazini unaoendelea kufanyika mkoani Mwanza, akisema mamlaka hiyo iliingia mkataba na kampuni kutoka China, kufanya upanuzi na uboreshaji huo.

Anataja mkataba ulianza kutekelezwa rasmi Mei mwaka jana, ukiwa wa miezi miezi 18, yaani mwaka mmoja na miezi sita, kwa gharama ya shilingi bilioni 18.6.

Lugenge anasema, upanuzi na uboreshaji wake umelenga kukidhi huduma za uendeshaji bandari, ukizingatia kukua shughuli za kibandari, ambao baada ya kukamilika na kuanza kutumika utahudumia pia meli zingine kubwa zinazoendelea kutengenezwa na shehena za mizigo na abiria katika Ziwa Victoria.

Anasema, pia yapo maboresho mengine ya mradi katika Ziwa Victoria, eneo la kwanza lililokusudiwa kujengwa ni maegesho ya meli, ujenzi wa miundombinu ya barabara na taka ngumu, ujenzi jengo la abiria, jengo la ukaguzi wa abiria na mizigo na ujenzi uzio wa bandari.

Vilevile, anataja ujenzi wa miundombinu, mifereji ya maji, ujenzi wa kingo za Mto Mirongo na kuhamisha miundombinu ya reli pamoja na kuwekwa miundombinu ya umeme, ikiwamo maandalizi ya utekelezaji wake.

Wakati Meneja Lugenge akizungumza na Nipashe, katikati ya Aprili mwaka huu, akisema mkandarasi alishafikia asilimia 100 ya hatua hiyo, akifafanua alishaleta mitambo ya kufanya kazi eneo la mradi na utekelezaji wa awali katika maendeleo ya mradi kwa asilimia 37, ikiwa imeshapita zaidi ya asilimia 75 ya mwaka wakati huo, tangu mradi kuanza.

Anasema, hadi kufikia Machi 15, mwaka huu ikijumuisha miezi miwili ya maandalizi, ujenzi kwa jumla ulishafikia asilimia 64 ya muda uliopangwa katika utekelezaji huo wa miezi 18 na malipo yaliyotolewa kwa mkandarasi wa ujenzi hadi ni shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 13 ya gharama za mradi wote.

**CHANGAMOTO ZAKE**

Katika mradi huo, zinatajwa changamoto zilizojitokeza ni hali ya utegemezi katika shughuli za bandari na maboresho yanayofanywa na mkandarasi, pia uboreshaji ukizingatia kwamba huduma za bandari bado zinaendelea sanjari na utekelezaji wake.

Pia kuna mabadiliko usanifu wa baadhi ya miundombinu katika mradi kusababisha kupitiwa upya usanifu, mbali na uliofanywa awali.

Lingine, Lugenge analitaja ni katika upanuzi, haja ya kupata eneo la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa ghati la meli mpya inayoendelea kujengwa.

Unafafanuliwa ni ujenzi unaohusisha ghati mahususi kwa ajili ya kuegesha meli kubwa katika Bandari ya Mwanza Kusini, MV Hapa Kazi Tu, ili iendane na meli hiyo inayoendelea na kujengwa.

Vilevile kuna ufinyu wa eneo la mradi unaotajwa kusababisha kupunguza kasi ya utekelezaji wake, hata serikali mkoa wa Mwanza kulazimika kuisaidia TPA eneo la soko la kuuza samaki, ili kukabiliana na changamoto hizo.

Meneja huyo anataja kuongezeka kina cha maji katika Ziwa Victoria, ikisababishwa na mvua nyingi iliyokuwa inaendelea kunyesha (wakati huo), shughuli za kibinadamu nazo zikichangia kuongezeka kina hicho, vyote vikisababisha mradi huo kuchelewa kukamilika kwa wakati, mpaka katikati ya Aprili mwaka huu, ilikuwa nyuma kwa asilima 20.5.

**MAFANIKIO YALIKO**

Lugenge anasema, mkandarasi huyo ameanza utaratibu wa kuongeza mitambo ya kufanyia kazi, kuongeza wafanyakazi, ili atumike usiku na mchana ili bandari, ili kukamilisha mradi ndani ya muda uliopangiwa kimkataba.

Anasema TPA Kanda ya Ziwa, inaazimia kuboresha bandari Ziwa Victoria, ili kunufaisha wananchi na fursa zilizopo, kwani mradi ukikamilika utaweza kuleta manufaa anwai kwa wakazi wa Mwanza na mikoa jirani, wapate ajira za kutosha wananchi wanaozunguka eneo la bandari hiyo.

Suala la kuhudumia shehena na mizigo, anasema kuna matarajio yataongezeka kutoka tani milioni moja kwa mwaka na zitaongezeka maradufu, huku kusanyaji mapato na huduma za kijamii ukiboreshwa.

"Upanuzi huo na uboreshaji Bandari Mwanza Kaskazini, umelenga kuwaleta pamoja watoa huduma wote, taasisi zinazotoa huduma za kibandari kuwa sehemu moja, huduma zitarahisishwa na kuwafanya wateja kuwavutia kutumia bandari za Ziwa Victoria kwa ujumla," anasimulia Lugenge.

**MIKAKATI IJAYO**

"Mikakati iliyopo baada ya kukamilika upanuzi na uboreshaji bandari hiyo, mamlaka (TPA) imeweka mpango wake wa Mradi wa Mwaka 2024/25, kupanua tena, pia kuiboresha Bandari ya Mwanza Kusini, ambayo ni maalum kwa ajili ya shehena za mizigo," anasema Lugenge.

Ahadi zake Lugenge anasema, bandari hiyo itakuwa kivutio na kitovu cha huduma ya usafiri wa maji kwa mikoa mitano ya Kanda ya Ziwa na nchi jirani watakuwa wakizihudumia.

Nchi ambazo wamekuwa zinazohudumiwa shehena kupitia bandari za Ziwa Victoria, kwa asilimia kubwa Uganda na Kenya, ni kupitia bandari za Kisumu, akitaja zaidi taifa la Sudan Kusini.

Vilevile anaitaja Burundi na Rwanda, akinena wataendelea kunufaika na bandari hiyo ya Mwanza, akitoa wito kwa wafanyabiashara na wadau wote wa usafiri watumie fursa hiyo kuwekeza katika huduma za usafirishaji kwa njia ya maji.

Bandari zingine ndogo katika Ziwa Victoria, anazitaja ni pamoja na Mwigobelo mkoani Mara; Magarini na Kyakwikwi mkoani Kagera; Lushamba -Mwanza.

Pia anataja Bandari Kavu ya Isaka Shinyanga na Nyamilembe mkoani Geita.



Ujenzi wa upanuzi wa Bandari ya Mwanza Kaskazini ukiendelea, mafundi wakiwa kazini.



# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA MADARAKANI ILEMELA INAENDELEA KUSONGA, ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 65.2 ZAPOKELEWA

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni Miongoni mwa halmashauri nane zilizopo mkoani Mwanza, Manispaa ya Ilemela inayoundwa na Tarafa moja, Kata 19, Mitaa 171 ikiwa na Baraza la Madiwani lenye jumla ya madiwani 26 na Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk. Angeline Mabula imetajwa kuinuka mara dufu kimaendeleo katika miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.



Jengo jipya la Utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

Kuendelea kwa Manispaa yeyote kunategemea maboresho pamoja na ujenzi wa miundombinu mipya katika sekta muhimu za Afya, Elimu, Maji pamoja na barabara ambapo kwa kipindi hicho Ilemela, inatajwa kupokea zaidi ya Sh.bilioni 65.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi muhimu kwa maendeleo ya Wananchi fedha kutoka serikali kuu na mapato ya ndani ya halmashauri.

Mkurugenzi Halmashauri hiyo, Bi Ummy Wayayu anasema fedha hizo zilizopokelewa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia zimefanya mabadiliko makubwa ya kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kuwasogezea karibu wananchi huduma muhimu za Afya, Elimu, Maji na Barabara.

**ELIMU**

Sekta ya Elimu ni mojawapo ya eneo la muhimu katika kukuza maendeleo ya nchi pamoja na kuongeza idadi ya watu wanye ujuzi katika sekta mbalimbali ili kuendana na suala la kukua kwa sayansi na teknolojia.

Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa kulihutubia Bunge aliweka bayana dhamira ya serikali yake ya kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na kufanya mabadiliko ya Mitaala iliyopo ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mahitaji ya soko kitaifa, kikanda na kimataifa.

Ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia kumeshuhudiwa maboresho makubwa katika sekta ya elimu na utekelezaji wa kazi kulingana azma yake ya kuhakikisha elimu inakuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kutoa wahitimu wenye ujuzi na stadi.

Mkurugenzi Ummy anasema katika kipindi hiki, madarasa 207 mapya yamejengwa kikamilifu sambamba na kuyawekea viti na meza ndani, hali iliyowawezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza kusoma bila usumbufu wala kubanana.

"Kuanzia Machi 2021 hadi Machi 2024 chini ya Rais.Samia Suluhu Hassan Halmashauri imepokea zaidi ya shilingi billioni 65.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo huku Sh.bilioni 16.67 zikiwa ni kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu ya sekondari pekee,"anasema Ummy.

Hellen Mushi ni afisa elimu vifaa na takwimu divisheni ya Elimu Sekondari Ilemela anasema sambamba na madarasa hayo vilevile zimejengwa maabara za kisasa 11 zenye mahitaji yote muhimu ya kujifunzia kwa vitendo na kuwa matokeo yake tayari yameanza kuonekana kutokana na ufaulu ambapo Manispaa hiyo imeongeza ufaulu mara dufu ikiongoza kwa Mkoa wa Mwanza kwa kuwa na ufaulu mzuri.

"Tumefuta alama sifuri kwa shule saba lakini pia jitihada za kuondoa daraja la nne kwa wanafunzi wote zinaendelea na kwa kidato cha sita ufaulu umeongezeka hadi asilimia 99.87 na hakuna daraja sifuri, tutaendelea kutimiza wajibu wetu kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa mitaala pamoja na uendeshaji wa shule ikiwa ni kusimamia vizuri miundombinu ambayo imejengwa na kuhakikisha kwamba inakuwa kwenye ubora unaotakiwa katika vipindi vyote,"anasema Mushi.

Mwl. Mushi anasema pia kuna ongezeko la shule sita mpya ambazo zimesaidia kupunguza umbali ambao wanafunzi wengi wamekuwa wakitembea kutoka nyumbani kwenda shule.

Wakishuhudia manufaa ya ongezeko la shule sambamba na maboresho katika miundombinu ya elimu sekondari baadhi ya walimu, wazazi pamoja na wanafunzi wanataja hatua hiyo kuwa chachu ya kila mtoto kupata elimu bora.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Buzuruga, Mwl.Jamal Ally anasema kabla ya kujengwa kwa shule hiyo mpya ya Buzuruga zimekuwa zikitokea ajali kwa wanafunzi kutokana na kutumia muda mrefu barabarani lakini utekelezaji wake umekuwa suluhisho kwa tatizo hilo la muda mrefu.

Mwanafunzi shule ya sekondari Buzuruga, Miriana Leonard anasema shule hiyo imewaepusha na vishawishi walivyokuwa wakivipata hapo awali walipokuwa wakitembea kuitafuta shule ya sekondari Kangae iliyopo umbali kutoka maeneo hayo.

Mkazi wa Buzuruga, Getrude Richard anasema hapo awali watoto wao walikuwa wanakutana na vikwazo vingi njiani zikiwemo ajali za barabarani huku wengine wakidaiwa kuchomwa visu na wahuni nyakati za alfajiri lakini kwa sasa hali ni tofauti kutokana na huduma hiyo kusogea karibu yao.

Kwa upande wa Elimu Msingi, Afisa elimu vifaa na takwimu Mwalimu Johannes John ameeleza kuwa zimejengwa shule mpya Saba na kuwa kati ya shule hizo, mbili zimejengwa kwa mradi wa boost kwa gharama ya Sh.billion 1.5.

Kadhalika anataja matumizi ya zaidi ya Sh.milioni 155.8 kwa ajili ya ujenzi wa matundu 89 ya vyoo ambapo vimeongeza idadi ya matundu ya vyoo kufikia 2691, sambamba na utengenezaji wa madawati 18,573 yaliyofanya Halmashauri hiyo kufikisha madawati 22,545.

Mwl. John anaeleza kuwa kwa kipindi hicho wamepokea Sh.bilioni 2.7 kwa ajili ya elimu bila malipo. Ambapo yote kwa pamoja anayataja kuzaa matunda ya ongezeko la ufaulu kwa asilimia 95.6, uandikishwaji wa wanafunzi kwa madarasa ya awali na msingi darasa la kwanza kwa asilimia 100.

Akisimulia hali ya mazingira ya usomaji ya awali, Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Busenga, Chacha Mniko anasema ulikuwepo msongamano kubwa wa wanafunzi darasani hali iliyokuwa ikisababisha washindwe kuelewa lakini kwa saa hali ni tofauti kutokana na kuwa na madarasa pamoja na miundombinu ya kutosha.

**AFYA**

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Manipaa ya Ilemela ina watu 402, 175 huku idadi hiyo ikitajwa kuendelea kuongezeka kutokana na kuwepo kwa fursa za kimaendeleo na miundombinu ya uhakika.

Ongezeko la watu katika eneo husika linatajwa kuwa chanzo cha ongezeko la mahitaji mbalimbali ikiwemo huduma za Afya, Mkurugenzi Ummy anaeleza kuwa, kutokana na hali hiyo katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan huduma za Afya zimeborehwa mara dufu.

Mkurugenzi Ummy amesema kuwa katika kipindi hicho, Ilemela ilipokea zaidi ya Sh.bilioni 3.2 ambazo zimesaidia kufanya mabadiliko makubwa ukiwemo ujenzi wa Hospitali ya Wilaya , vituo vya afya, zahanati pamoja na maboresho ya miundombinu mingine muhimu ikiwemo manunuzi ya vifaa tiba, madawa n.k.

Ameendelea kufafanua kuwa Halmashauri imefanikiwa kuongeza Hospitali moja ya Wilaya ambapo mwanzo haikuwepo Hospitali ya Wilaya ikiwa na majengo 15 ambapo majengo mengine tayari yameanza kutumika kutoa huduma za kitabibu. Vilevile kuna ongezeko la vituo viwili vya Afya na kufanya Manispaa hii kufikisha vituo vya afya vitano, Zahanati 17 na nyingine tatu ambazo tayari zimeanza kutoa huduma,"

"Kwenye Hospitali ya Wilaya kuna huduma za X-rays pamoja na Utra sound, lakini pia kituo cha afya Karume na Buzuruga tumepewa mashine za X-rays mpya kwaajili ya kuwasaidia wananchi kwasababu hizi huduma zamani wananchi walikuwa wanapata tabu sana hadi waende Bugando au Hospitali ya rufani Mkoa, Sekou-Toure Seketure," amefafanua

Vilevile anasema kuwa wamepata vifaa tiba kwaajili ya kinywa na meno na wanaendelea na maboresho hivyo kumuahidi Rais Samia Suluhu Hassan kuwa watazidi kusimamia shuhuli zote ili wananchi waendelee kupata huduma.

Kwa upande wa watumishi tumepata watumishi zaidi ya 50 wapya kwa kipindi hiki na kufanya idadi ya watumishi kufikia 472 kwa hiyo tunashukuru kwa maboresho haya makubwa na tutazidi kuweka juhudi ili kupunguza au kumaliza kabisa vifo ya kina mama wajawazito na wototo.

Mkazi wa Kata ya Kayenze, Anastazia Makoye anasema, anaishukuru serikali kwa ujenzi wa kituo cha Afya katika eneo lao na kuwa kituo hicho kimekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa kata hiyo na kuwarahisishia upatikanaji wa huduma walizokuwa wakizifuata katika kituo cha Sangabuye hali iliyokuwa ikisababisha wajawazito kukosa huduma kwa wakati.

**MIUNDOMBINU**

Ubora wa miundombinu unachochea kukua kwa uchumi wa mtu mmoja moja na taifa kwa ujumla kutokana na kufungua mianya ya ajira pamoja na kufikika kwa maeneo muhimu. Katika Manispaa ya Ilemela inatajwa kufanyika kwa maboresho makubwa ya miundombinu pamoja na ujenzi wa mingine mipya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa hiyo Ummy Wayayu anasema kwa kipindi hicho zaidi ya Sh. bilioni 1.75 zimeelekezwa katika ukamilishaji wa jengo la Utawala la Halmashauri.

Ummy anasema kuwa pia zimepokelewa Sh.bilioni 13.79 kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa kimkakati wa stendi ya mabasi ya Nyamhongolo ambayo mpaka sasa imekamilika kwa asilimia 100 na inaendelea kutumika.

"Vilevile Sh.bilioni 5.39 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya TASAF, fedha nyingine zaidi ya Sh.bilioni 3.58 za upimaji wa ardhi maeneo ya Sangabui pia Sh.bilioni Moja imepokelewa kwa ajili ya fedha za msaada wa kibajeti," anasema Ummy.

Aidha anaeleza kuwa Halmashauri hiyo imepokea Sh.milioni 227.91 ikiwa ni fedha za mfuko wa jimbo kwaajili ya kuchochea maendeleo ndani ya Jimbo pamoja na Sh. bilioni 12.9 fedha za mapato ya ndani ambazo zinatekeleza miradi mbalimbali upande wa afya elimu, upimaji na ulipaji wa huduma za ardhi na maendeleo ya jamii pamoja na barabara.

Mkurugenzi Mtendaji Ummy anatoa shukurani zake za dhati kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuidhinisha na kutoa fedha hizo ambazo zimeisadia Manispaa hiyoo kukabiliana na kero mbalimbali za wananchi.

"Lakini pia kwa upande wa sisi Halmashauri tumeendelea na mikakati kwaajili ya kuendelea kukusanya mapato yetu ya ndani ili kuweza kuendelea kuchochea na kusimamia vizuri miradi ya maendeleo ambayo kwa namna moja au nyingine inaleta tija kwa wananchi wetu," anasisitiza Ummy.

Akizungumza kwa niaba ya baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ilemela, Mhe Renatusi Mulunga mbali na kumshukuru Rais Samia kwa fedha nyingi alizotoa katika Manispaa ya Ilemela anaeleza kufurahishwa utekelezaji wa haraka wa miradi ya maendeleo chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Niseme tu kuwa kazi ni nyingi na za kuonekana lakini nitoe rai kwa wakazi wa Ilemela, waendelee kuiunga mkono serikali katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi unazidi kufanyika na kuwa endelevu,"anasema Mulunga.

Aidha amewataka wananchi hao kuhakikisha wanaunga mkono juhudi hizo kwa kupeleka watoto wao wote na pia kuendeleza mausiano na walimu ili kujua maendeleo ya watoto wao na siyo kuwatelekeza tu shule bila kufuatilia maendeleo yao.



# RUWASA Mwanza ilivyowatua ndoo kichwani zaidi ya wananchi Mil.1.6

**Na Vitus Audax, MWANZA**



Mkurugenzi mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo kulia akiweka saini ya katika mkataba wa upanuzi mradi wa maji Lugeye wenye thamani ya Sh.bilioni 7.1 unaotarajiwa kuhudumia zaidi ya watu 80,000 katika Kata ya Lugeye na kuzalisha lita milioni 3 kwa siku, aliyesimama katikati ni wakili Gloria Chagewi mwanasheri wa RUWASA pamoja na wakandarasi kutoka kapuni ya ujenzi ya Monela Construction and co LTD watakaojenga mradi huo. **PICHA: VITUS AUDAX**

SAFARI iliyoanzishwa Julai, 2019 na serikali kupitia Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 ya kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuwa taasisi ya umma yenye jukumu la kujenga skimu za maji na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, imekuwa mkombozi sasa kwa wananchi zaidi ya milioni 1.645 sawa na asilimia 70 ya Wananchi waishio maeneo ya vijijini mkoani Mwanza.

Awali, kabla ya kuanzishwa majukumu ya RUWASA yalikuwa yanatekelezwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa (RSs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Majukumu hayo ni pamoja na kuhakikisha huduma za maji zinapatikana kwenye jamii za watu waishio maeneo ya vijijini, miji midogo na makao makuu ya wilaya.

Baada ya majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa (RSs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamishwa kwenda RUWASA, uwajibikaji wa Maofisa waliokuwa wanahusika na utoaji wa huduma ya maji ulihamishwa kwenda Wizara ya Maji kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

RUWASA imeingia kazini ikiwa na dhamia ya kutoa huduma ya majisafi na salama na kuhamasisha usafi wa mazingira kwa jamii iishio vijijini kwa kufanya usanifu, ujenzi, kusaidia uendeshaji wa matengenezo ya miundombinu na utoaji wa huduma kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya kiuchumi na kijamii shughuli zinazotekelezwa ipasavyo na Wakala huo mkoani Mwanza.

Hadi kufikia Juni, 2024 RUWASA umefanikiwa kuwatua ndoo kichwani wananchi waishio vijijini 1,645,061 sawa na asilimia 70 ya wananchi 2,337,573 waishio vijijini, mkoani Mwanza.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Mwanza wenye Wilaya nne na Halmashauri nane una jumla ya watu 3,699,872 ambapo kati ya hao 2,337,573 wanaishi maeneo ya vijijini.

**ANENAVYO MKURUGENZI MKUU**

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Nchini Mhandisi Clement Kivegalo akizungumza wakati wa utiwaji wa saini wa mikataba miwili ya ujenzi pamoja na upanuzi wa miradi ya maji katika Kata tatu za Lugeye, Lumeji na Misungwi zilizopo katika Wilaya ya Magu mkoani hapa yenye thamani ya Sh. Bilioni 8.4 kwaajili ya kuhudumia wananchi zaidi ya elfu themanini wa kata hizo na kumaliza changamoto ya maji kwa asilimia tisini alisema Mwanza ni miongoni mwa mikoa iliyopata kipaumbele cha kufikishiwa miradi mingi ya maji.

Anasema kwa nchi nzima serikali tayari imesaini miradi yenye thamani ya Sh.bilioni 800 kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini lakini kwa Mkoa wa Mwanza ni miradi ya zaidi ya Sh.bilioni 125.

"Kwa Mkoa wa Mwanza pekee hadi kufikia disemba 2022 tumesaini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 125 kwaajili ya miradi ya maji vijijini 43 ikiwa mingine tayari imekamilika na tayari inatoa maji ikiwa ni sehemu ya kutatua tatizo la upatikanaji wa maji na kumtua mama ndoo kichwani," alisema Kivegalo

**HALI ILIVYO MWANZA**

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Godfrey Sanga anaiambia Nipashe kuwa Wakala huo unahudumia Wilaya tano ambazo ni Magu, Kwimba, Sengerema, Ukerewe na Misungwi huku ukihudumia vijiji 514 kati ya 544 vilivyopo mkoani hapa huku vijiji 30 vikihudumiwa na Mamlaka za Maji.

"Kati ya vijiji hivyo tulivyonavyo, vijiji vilivyofikiwa na huduma ya maji ni 480, sawa na 88%, vilivyofikiwa na miradi ya bomba ni 251, vilivyofikiwa na visima ni 229 huku visivyofikiwa na huduma ya maji ni 34," anasema Mhandisi Sanga.

Akifafanua hali ya upatikanaji wa maji vijijini katika Wilaya tano zinazohudumiwa Mhandisi Sanga anasema, Wilaya ya Kwimba yenye wakazi 447,579 kati yao 322,257 wanapata huduma sawa na asilimia 72.



"Kwa Magu asilimia 75 wamefikiwa huduma ambao ni 273,297 kati ya 364,393, Misungwi watu 326,942 wamefikiwa na maji kati ya 447,867 sawa na asilimia 73, Sengerema watu 491,643 kati ya 746,665 wamefikiwa huduma sawa na asilimia 66,"

"Wilaya ya Ukerewe yenye wananchi 331,069 tayari wananchi 230,922 wamefikiwa na huduma ya maji sawa na asilimia 70 hivyo kwa muda huu kazi iliyofanyika ni kubwa kwa muda mfupi lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wote waishio vijijini kazi inayosimamiwa kikamilifu na Rais Samia Suluhu Hassan,"anasema Mhandisi Sanga.

Aidha Mhandisi Sanga anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhudumia Wakala huo mkoani Mwanza kwa kuendelea kuupatia fedha za utekelezaji wa miadi mbalimbali sambamba na kutoa ajira ili kuhakikisha wanakuwa na watumishi wa kutosha.

Anasema kwasasa Mkoa huu unaupungufu wa Watumishi 21 kati ya 95 wanaohitajika katika ofisi ya Mkoa na ofisi za Wilaya zinazohudimiwa na Wakala huo.

"Katika ofisi ya Meneja Mkoa uhitaji ni watumishi 17 ambapo waliopo mpaka sasa ni 15 tukiwa na upungufu wa watumishi wawili. Aidha katika Wilaya ya Kwimba uhitaji wa watumishi ni 15, waliopo ni Wanane huku ikiwa na upungufu wa Watumishi Saba,"

"Wilayani Magu tunao watumishi 10 mahitaji ni 15 tuna upungufu wa watumishi watano, Misungwi tunao watumishi wanane, mahitaji ni watumishi 15 huku ikiwa na upungufu wa watumishi saba,"

"Vilevile Sengerema tuna ziada ya watumishi watatu ambapo mahitaji ni 18 lakini wapo watumishi 21 na Ukerewe tunao upungufu wa watumishi sita ambapo tulionao ni tisa huku mahitaji yakiwa watumishi 15,"anasema Mhandisi Sanga.

**KUHUSU FEDHA ZILIZOPOELEWA 2023/24**

Meneja, Mhandisi Sanga anasema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 RUWASA Mkoa wa Mwanza ulipokea zaidi ya Sh.bilioni 31.185 ambapo kati ya fedha hizo walitumia Sh.bilioni 30.843 na kubaki na salio la Sh.milioni 351.9.

"Fedha hizo tumezipokea kutoka PforR zaidi ya Sh.bilioni 16.21 ambapo zimetumika Sh.bilioni 16.19 zikibaki zaidi ya Sh.milioni 19.665, fedha nyingine ni kutoka NWF zaidi ya Sh.bilioni 14.947, zimetumika zaidi ya Sh.bilioni 14.625 na kusalia Sh.milioni 332 fedha nyingine tulizozipokea ni kutoka OC ambazo ni zaidi ya Sh.bilioni 28,124 ambapo tumetumia zaidi ya Sh.bilioni 28,122 ambapo tumesalia na Sh.1,980.66,"anasema Mhandisi Sanga.

Aidha Mhandisi Sanga anasema katika kipindi cha mwaka 2023/24 wakala huo ulipanga kutekeleza miadi 74 katika Wilaya wanazozihudumia ikiwa na thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 146.315 ambapo kwa bajeti ya mwaka huo umepokea zaidi ya Sh.bilioni 30.658.

"Miradi hii ambayo inaendelea katika mwaka wa fedha ujao 2024/25 kwa Wilaya ya Kwimba tunao ujenzi wa miundombinu 15 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 23.971 na kwa mwaka huu bajeti ilikuwa zaidi ya Sh.bilioni 6.173, Magu miradi 10 yenye ghaama ya zaidi ya Sh.bilioni 17.017 bajeti ni zaidi ya Shbilioni 5.894,"

"Misungwi ni miradi 18 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 61.7 bajeti ilikuwa ni Sh.bilioni 3.071, Sengerema miradi 21 inayoghaimu zaidi ya Sh.bilioni 28.243 ambapo bajeti iliyopangwa ni zaidi ya Sh.bilioni 9.344 na Ukerewe ina miradi 10 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 15.377 ambapo bajeti yake kwa mwaka huu ilikuwa ni zaidi ya Sh.bilioni 6.174,"anasema Mhandisi Sanga.

INAENDELEA UK. 14



# RUWASA Mwanza ilivyowatua ndoo kichwani zaidi ya wananchi Mil.1.6

INATOKA UK. 13

### MIKAKATI 2024/25

Katika kuhakikisha wananchi vijijini wanaendelea kufikiwa huduma ya maji safi na salama na kufikia lengo la Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Maji la kumtua mama ndoo kichwani RUWASA inaeleza kuweka mikakati mbalimbali kuakisha lengo hilo linatimia mkoani Mwanza.

Meneja Sanga, anasema miradi 54 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 185.614 inataajiwa kuendelea kutekelezwa katika Wilaya zote tano zinazohudumiwa na Wakala huo kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambapo zaidi ya Sh.bilioni 20.4 imetengwa kwaajili ya miundombinu hiyo.

Mhandisi Sanga anasema mgawanyo wa miradi hiyo ni pamoja na Kwimba miradi 12 yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 11.569, ambazo zimepangiwa zaidi ya Sh.bilioni 2.207, Miradi Saba kwa Wilaya ya Magu yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 54.206 ambapo imepangiwa zaidi ya Sh.bilioni 3.828.

Kadhalika Mhandisi Sanga anasema katika Wilaya ya Misungwi ipo miradi 12 inayogharimu zaidi ya Sh.bilioni 66.9 na bajeti yake itakuwa zaidi ya Sh.bilioni 3.287, Sengerema miradi 15 ya zaidi ya Sh.bilioni 35.453 ikipangiwa zaidi ya Sh.biloni 7.06 na Ukerewe ikiwa na miradi minane yenye thamani ya Sh.bilioni 17.477 ambayo imepangiwa zaidi ya Sh.bilioni 4.02

Licha ya shughuli kubwa inayofanywa na Wakala huu kwa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Sanga anasema zipo changamoto kadhaa zinazohitaji ufumbuzi ili kuhakikisha wanafikia matokeo ya haraka.

Mhandisi Sanga anataja changamoto hizo kuwa ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa fedha za madai ya Wakandarasi baada ya kutekeleza kazi za ujenzi.

"Vilevile Miradi tuliyonayo ni mikubwa sana kuliko bajeti hivyo tunaendelea kupunguza idadi ya miradi mipya ili bajeti iliyopo na ijayo 2024/25 iweze kupunguza madeni ya mikataba inayoendelea,"anasema Mhandisi Sanga

Anaendelea kusema kuwa changamoto nyingine ni uchache wa Watumishi ngazi ya Mkoa na Wilaya kulinganisha na miradi mikubwa inayoendelea kujengwa pamoja na uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri.

### UENDELEVU WA MIRADI YA MAJI VIJIJINI

Meneja wa RUWASA Mwanza, Mkoa wa Mwanza Mhandisi Sanga anasema kwa ujumla Mkoa una idadi Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii vinavyokusanya mapato kupitia Mfumo wa Malipo Serikalini (CBWSO-GePG) 33 vyenye jumla ya wateja 47,096.

Anasema katika Wilaya hizo zipo jumla ya Skimu za Maji 130 ambapo kupitia CBWSO-GePG kwa kipindi cha Disemba 2023 hadi Mei 2024 zimekusanya zaidi ya Sh.milioni 703.7 ambazo zinatumika katika utunzaji na ukaabati wa miundombinu ya maji katika maeneo husika.

Kadhalika anasema kati ya fedha hizo zilizokuanywa zaidi ya Sh.milioni 573.2 zimetumika katika kipindi hicho na kubaki na salio la zaidi ya Sh.milioni 129.8



Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kwimba Mhandisi Godriver Gwambasa akikagua Mradi wa Maji wa Kijiji cha Izizimba 'B' uliopo wilayani Kwimba wenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 460 ambao unahudumia wananchi zaidi ya 3600.**PICHA NA VITUS AUDAX**

### MIKAKATI

Kuhusu mikakati ya RUWASA Mwanza, Mhandisi Sanga anasema kuwa wanaendelea kusimamia ukamilishaji wa miradi 65 inayoendelea ambapo ikikamilika itahudumia watu 726,287, na kuongeza asilimia ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijni kutoka 70% ya sasa hadi 86% ifikapo mwezi Juni 2025.

Vilevile wanataajia kufikisha huduma ya maji katika vijiji 34 visivyo na huduma pamoja na vijiji vyenye upungufu wa maji kwa kuchimba visima 35 kwa majimbo Saba ya uchaguzi, kusanifu na kuingiza kwenye mpango na bajeti ya kila mwaka.

Kadhalika Mhandisi Sanga anasema wataendelea kutoa elimu kwa CBWSOs juu ya Usimamizi, Uendeshaji na uendelevu wa skimu za maji vijijini hasa matumizi ya GePG.

"Tunaendelea kutenga ununuzi wa magari na pikipiki katika ujenzi wa miradi yetu inayoendelea, mfano tumeweka ununuzi wa gari moja katika mradi wa Ukiliguru - Sumve na gari moja kwenye mradi wa Kigongo ambayo yakipatikana yatapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya magari,"anasema Sanga.

### WANENAVYO WANANCHI

Kati ya vitu vinavyorudisha nyuma shughuli za kimaendeleo katika nchi zinazoendelea kama Tanzania ni pamoja na ukosefu wa huduma ya uhakika wa maji safi na salama hali inayowalazimu Wanawake na watoto kutumia muda mrefu kutafuta huduma hiyo katika vyanzo ambavyo siyo vya uhakika na si salama pia.

Baadhi ya wananchi wanaonufaika na huduma ya maji safi na salama kutoka katika vijiji vinavyo hudumiwa na RUWASA vikiwemo vijiji vya Nsola, Kisamba, Bubinza na Yichobela vilivyopo katika kata za Lubugu na Ichobela wilayani Magu mkoani hapa wanataja kufikishiwa huduma hiyo kuwa mkombozi wa maisha yao.

Wanaeleza hayo walipotembelewa na Nipashe na kutaja kuwa hapo awali walivyoteseka kupata maji kwaajili ya kutumia huku zaidi ya watu watatu wa vijiji hivyo wakielezwa kutafunwa na mamba wakati wakichota maji ziwa Victoria.

"Ili kupata maji tulikuwa tunalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa sita kwa mguu kuelekea ziwani na kuna vipindi tofauti wenzetu walivamiwa, kushambuliwa mpaka kufa na mamba walipoenda kuchota maji alfajiri ziwani," alisema Elizabeth Sahani mkazi wa Bubinza.

Elizabeth alieza kuwa kwa sasa wamepumizika na hali ngumu ya upatikanaji wa maji baada ya maji kuwafikia mpaka mlangoni kupitia miradi iliyotekelezwa na RUWASA katika vijiji vyao.

Nae Wase Zabron mkazi wa kijiji cha Kisamba alieleza hali upatikanaji wa maji katika kijiji hicho kuwa ngumu awali kutokana na wanakijiji kuchota maji katika madimbwi anayotumika kunyweshea mifugo huku maji hayo yakielezwa kutokuwa safi na salama.

"Muda mwingine tulilazimika kuamka usiku kwenda kuchota maji ili ikifika asubuhi tupate nafasi ya kuweza kufanya shughuli zetu nyingine za kilimo mapoja na shughuli nyingine za kiuchumi ambap hutua hii ilitugombanisha na waume zetu ambao hawakuamini mienendo yetu," Alieleza Mgreth John

Lucas Zabron ni Diwani wa kata ya Lubugu anaiambia Nipashe kuwa katika kata yake pamoja na kata jirani wamefanikiwa kufikishiwa maji kutoka miradi ya usambasaji maji iliyotengenezwa na RUWASA kwaajili ya kukidhi mahitaji ya wananchi hao.

Vilevile alisema maji hayo wanayapata kwa bili hasa wale waliounganisha kwenye nyumba zao pamoja na wengine ambao wanapata maji hayo kupitia vituo vya usambazaji wanapolipia kwa wastani wa Sh.30 kwa ndoo moja.

Aidha baadhi ya wananchi na viongozi wa CBWSO katika wilaya ya Misungwi na Ukerewe mkoani hapa wanaiomba serikali kuchukua hatua kali kwa watu ambao wamekuwa wakiharibu miundombinu ya maji kwa kukata mabomba na kuiba vifaa wakiisababishia hasara serikali wakati mwingine wananchi kukosa huduma ya maji.

Wameyaeleza hayo kwa nyakati tofauti wakizungumza na Nipashe kufuatia uandaaji wa toleo hili, ambapo Peter Paul ni Meneja wa chombo cha watoa huduma za maji ngazi ya jamii katika mradi wa maji vijijini wa Fela-Usagara (FEUWASA) analiambia Nipashe kuwa licha ya kupatiwa mradi huo bado kuna watu wachache wanaohujumu miundombinu yake kwa kukata na kutoboa mabomba wengine wakiiba baadhi ya vifaa.

Baadhi ya wananchi wanaonufaika na miradi ya maji katika wilaya za Misungwi, Kwimba Magu ,Sengerema pamoja na Ukerewe waliomba serikali kupitia RUWASA kuendelea kutoa elimu juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji ili viendelee kuwanufaisha sambamba na utekelezaji wa miradi ya maji.

"Hii miradi inatusaidia kupata maji safi na salama tofauti na awali tulikuwa tukitembea umbali wa kilometa tano kufuata maji ziwani ambayo hata hivyo siyo safi na salama, hivyo wakidhibiti hujuma hizo ndogondogo hatutokosa maji safi tena" alisema Rucia Jilala mkazi


Perepetoa Masele pamoja mwenzake wakazi wa kijiji cha Ichobela wakifurahia kupokea huduma ya maji safi na salama kutoka kwa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini RUWASA wilayani Magu katika moja ya kituo cha kuchoja maji kati ya vituo 13 vilivyopo katika kijiji hicho. Kwa ndoo moja ya lita 20 wanachota kwa wastani wa Sh.30 huku waliounganishiwa majumbani wakipata huduma hiyo kwa Sh.1500 kwa uniti moja. **PICHA NA VITUS AUDAX**

# Bugando iliyobeba dhana ya huduma bora za afya, miaka mitatu ya Rais Samia

**Na Vitus Audax, MWANZA**

HOSPITALI ya Rufaa ya Kanda ya Bugando ilifunguliwa rasmi Novemba 3, 1971 na Raisi wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere ikihudumia Mikoa nane ya kanda ya Ziwa na Magharibi, inayo kadiliwa kuwa na wakazi zaidi ya Milioni 22.

Bugando inamilikiwa na Kanisa Katoliki ambapo inaendeshwa kwa ubia na Serikali ya Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania.Hospitali hii ni ya pili kwa ukubwa nchini ikihudumia wastani wa Wagonjwa 1200-1400 kwa Siku na ina zaidi ya vitanda 1000,.

**HUDUMA ZITOLEWAZO.**

Bugando, imejikita katika utoaji wa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi katika nyanja za Tiba, upasuaji na huduma za afya Saidizi. Kwa upande wa huduma za tiba, hospitali imeendelea kutoa huduma ambapo kwa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan imehudumia jumla ya wagonjwa wa nje na ndani 654,862.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando, Dk. Fabian Massaga anasema miongoni mwa huduma zinazotolewa katika Hospitali hii ni pamoja na huduma za Tiba, matibabu ya figo, kisukari, magonjwa ya damu, magonjwa ya kuambukiza, njia ya chakula, ngozi pamoja na saratani.

Kuhusu huduma za upasuaji, Dk.Massaga anasema hospitali imejikita katika kufanya upasuaji wa kibingwa na kibingwa bobezi ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu imeendelea kutoa huduma hizo kwa kufanya jumla ya pasuaji 47,108 za wagonjwa.

"Tumefanya upasuaji maalumu wa Watoto ambapo zaidi ya wagonjwa 1493 wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa mbalimbali, vilevile katika upasuaji wa jumla umehusisha kubadilisha nyonga, upasuaji wa kinywa na meno,"

"Upasuaji mwingine ni pamoja na macho, koo, pua na masikio, upasuaji wa kifua na moyo, upasuaji wa ubongo, mishipa ya fahamu na mgongo, mfumo wa mkojo, upasuaji sanifu pamoja na matundu madogo,"anasema Dk.Massaga

Dk.Massaga anasema sambamba na huduma hizo, pia wameendelea na kutoa huduma bora za vipimo vya mionzi na maabara ambavyo vimerahisisha utolewaji wa huduma za haraka kwa wagonjwa kutoka maeneo mbalimbali.

Anasema miongoni mwa vipimo hivyo vya kisasa ni pamoja na Ultra sound, CT- SCAN, X-RAY, Mammography, Dental X-RAY, Intervational Radiology, Maabara ya uchunguzi wa vina saba pamoja na Maabara ya uchunguzi wa vivimbe ambavyo vimesaidia utolewaji wa huduma kufanyika kwa urahisi ndani ya kanda.

**UPATIKANAJI DAWA ULIVYOIMARIKA**

Dk.Massaga katika Hospitali hiyo hali ya upatikanaji wa dawa muhimu na maalum umezidi kuimarika hadi kufikia asilimia 96 ambapo dawa hizo zinatoka kwenye mapato ya ndani na kwa wazabuni mbali mbali.

Kadhalika anasema hospitali hiyo ina kitengo cha uzalishaji wa maji tiba ambacho kina saidia kupunguza gharama za hospitali katika kuagiza baadhi ya dawa ambazo ni ngumu kupatikana katika masoko, hususani hapa nchini.

Huduma za dharura katika hospitali ni muhimili muhimu kwa mstakhabari wa uhai wa mgonjwa, Dk. Massaga anasema kwa sasa huduma za dharura zimeendelea kuboreshwa hospitalini hapo hali inayosaidia kuokoa maisha ya wagonjwa wengi.

"Tunaishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kuboresha huduma za Dharura katika Hospitali hii kwa kununua gari la kisasa zaidi la Wagonjwa lenye thamani ya Sh.milioni 163, gari hili litasaidia kutatua changamoto kwa wagonjwa mbalimbali wa dharura na wakati wa majanga kutokana na uwezo wake wa kutoa huduma zote za dharura hata ikiwa nje ya hospitali,"anasema Dk.Massaga.

Aidha anaeleza kuwa kupitia fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na Serikali, hospitali imeweza kununua vifaa tiba katika idara ya dharura (EMD) ili kupunguza changamoto kwa wagonjwa wa dharura wanaopelekwa hospitalini hapo kila siku.

**MABORESHO YA KIMKAKATI KATIKA MIUNDO MBINU**

Mkurugenzi Dk.Massaga anasema katika kipindi cha miaka mitatu Hospitali hiyo imeshuhudia maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali katika miundombinu muhimu ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wakati na harasa hasa katika kipindi cha majanga ya kitaifa na kidunia kwa ujumla.

Anataja maboresho hayo kuwa ni pamoja na kuongeza vyumba vya wagongwa mahututi (ICU) ambavyo vilikuwa pungufu hospitalini hapo na kusababisha adha kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za uangalizi wa karibu sana akitolea mfano tatizo kubwa la kidunia la UVIKO-19.

"Kwa kuliona hilo Mhe. Samia Suluhu Hassan alitoa fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa vyumba vya ICU Sh. milioni 500 ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa ambao wamekua wakihangaika kutokana na upungufu huu,"amesema Dk.Massaga

Aidha anataja maboresho mengine kuwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la matibabu ya macho, ambalo limejengwa na hospitali hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Kwasasa tumeanza kuhakikisha huduma ambazo zilikuwa zinatolewa nje ya nchi, sasa zinapatikana hapa nchini kwa kutumia wataalam wetu. Jambo ambalo limekuwa faraja sana kwa wananchi ambao hawakuwa na uwezo wa kuwapeleka wagonjwa wao nje ya nchi, vilevile serikali imeweza kuokoa fedha nyingi kutokana na jengo hili la matibabu,"anasema Dk.Massaga





Dkt. Fabian A. Massaga
Mkurugenzi Mtendaji
Hospitali ya Rufaa ya
Kanda ya Bugando

Aidha anataja jumla ya bajeti ya ujenzi wa jengo hilo kuwa ni Sh. bilioni 3.7, ambapo wafadhili wametoa Sh. Bilioni 2.4, Hospitali ya Bugando wametoa Sh. bilioni 1.3.

**WODI YA SARATANI**

Vilevile Dk.Massaga anasema miongoni mwa maboresho ya kimkakati yaliyofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na ujenzi wa jengo la matibabu ya Saratani kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau mbalimbali.

Anasema Jengo hilo lina huduma zote za msingi kama vyumba vya madaktari, Maabara, uchunguzi wa mionzi, dawa, ultra Sound, kutunza kumbukumbu za mgonjwa na chumba cha wagonjwa maalum (VIP).

"Huduma zote muhimu zitapatikana katika jengo hili hali inayopunguza mizunguko kwa wagonjwa. Wodi ya saratani imesaidia kupunguza urasimu na adha kwa wagonjwa kusafiri kwenda Dar-es-Salaam (Ocean Road) na nchi za jirani kutafuta huduma na pia wagonjwa wanapata matibabu sahihi kwa wakati sahihi, kwa namna moja ama nyingine imepunguza vifo kwani wagonjwa wanahudumiwa kwa wakati,"anasema Dk.Massaga.

Vilevile Dk.Massaga anasema Hospitali hiyo imefanikiwa kujenga Mtambo wa kufua hewa ya oksijeni wenye uwezo wa kuzalisha mitungi ya Oksijeni 400 ambapo Hospitali hiyo ina tumia mitungi takribani 100 kwa siku, na kuwa Hospitali nyingine zitanufaika na mtambo huu.

"Ujenzi huu umegharimu Sh. milioni 272 kutoka katika mapato ya ndani ya Hospitali na gharama ya mashine zinatoka kwenye pesa za Uviko-19 ambazo ni Sh.milioni 600.

**BUGANDO ILIVYOMWAGA AJIRA KWA MAELFU.**

Dk.Massaga anasema Hospitali hiyo imetoa fursa za ajira kwa watu zaidi ya 2,068 ambapo kati yao watumishi zaidi ya 1200 wanalipwa na serikali ambapo pia serikali imefadhili watumishi 27 kimasomo katika ngazi mbalimbali za kibingwa na kibingwa bobezi.

"Hospitali inapenda kuishukuru serikali ya awamu ya sita kupitia wizara ya afya, kwa ufadhili wa wataalam katika kujiendeleza kimasomo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika sekta ya afya. Pia imeendelea kulipa mishahara kwa wafanyakazi wa taasisi kwa zaidi ya Sh.bilioni 21.073, fedha za madawa kutoka MSD ni zaidi ya Sh.milioni 734.8 pamoja na fedha za gharama za uendeshaji kutoka serikalini zaidi ya Sh.milioni 210.99,"anaema Dk.Massaga.

**KUBORESHWA KWA MAHUSIANO KATI YA TAASISI ZA DINI NA SERIKALI.**

Kuhusu mahusiano na serikali Dk.Massaga anasema, Hospitali hiyo inayomilikiwa na kanisa Katoliki Tanzania imeendelea kuwa na ushirikiano na serikali kwa kiasi kikubwa na ushirikiano huu umezidi kuimarika siku hadi siku.

"Mfano Rais Samia Suluhu Hassan alifanikiwa kuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho ya Jubilee ya Miaka 50 ya Bugando, na alizindua miradi mbalimbali ikiwemo Mashine ya MRI, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango alikuja kuzindua jengo la Saratani, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Kassim alizindua jengo la Macho,"

"Vilevile serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza imekua ikihamasisha na kutafuta wadau mbalimbali ili waweze kutoa msaada hasa katika ujenzi na maendeleo. Pia kubadilishana ujuzi katika sekta ya Afya, kama sehemu ya ushirikiano kati ya Serikali na Taasisi za Dini, Wataalam wetu wamekuwa wakibadilisaha ujuzi na madaktari wengine kutoka hospitali za serikali ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa - Muhimbili Orthopedic Institute (MOI), Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya pamoja na Hospitali nyingine," anasema Dk.Massaga.

Aidha Dk.Massaga anatoa wilo kwa wananchi kubadili mitindo ya maisha na kuondoa kasumba iliyojengeka kuwa Hospitali ni kwa ajili ya wagonjwa tu badala yake watambue kuwa kila mmoja ni mgonjwa na anahitaji uchunguzi mara kwa mara na kupata ushauri wa kitaalamu kwa ustawi wa afya yake.

**NENO KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

"Tunaishukuru, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya kuendelea kuwajali wananchi kwa kuboresha huduma za afya katika vituo vya Afya na hospitali za ngazi zote. Pia Hospitali inapenda kuishukuru serikali ya awamu ya sita kupitia wizara ya afya, kwa ufadhili wa wataalam katika kujiendeleza kimasomo ya ubingwa na ubobezi katika sekta ya afya,"anasema Dk.Massaga

# TFS inavyowekeza kimkakati kuyaona mapinduzi mazingira, uchumi Mwanza

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza, inatamka kubeba wasifu wa kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki kwa miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita.

TFS Mwanza, inajishughulisha na kuhifadhi misitu iliyopandwa, ya asili na nyuki kwa wilaya za Nyamagana, Ilemela, Misungwi, Magu, Kwimba, Sengerema na Ukerewe,

Pia, inataja kusimamia hifadhi za misitu ya asili minne zenye hekta 17,360: Kome (2,487), na Maisome (9,319) wilayani Sengerema; Sayaka Magu (5,421); Igwata, Kwimba (133).

Vilevile mashamba ya kupandwa mawili, Rubya (1,926) wilayani Ukerewe na Buhindi (21,880), wilayani Sengerema.

Shughuli kuu za TFS, ni kuhifadhi na kulinda misitu ya asili, kupanda miti katika mashamba ya serikali, kufuga nyuki, kukusanya mapato serikali, kuhudumia mazao ya mistu, nyuki, pia kuelimisha kuhifadhi misitu na nyuki.

Mhifadhi Mkuu wa TFS Kanda ya Ziwa, Bakari Mohamed, anayataja ni mafanikio, kimazingira, kiikolojia, uchumi na utamaduni.

Anaeleza ni faida zitokanazo na kulinda, kuhifadhi, kupatikana mvua sahihi, kukabili mabadiliko tabianchi, kupunguza hewa ukaa angani, joto la dunia na kuzuia mafuriko majini.

Mengine anayataja ni kuzuia vimbunga, kurutubisha ardhi, kuhifadhi vyanzo maji, viumbe hai na kuzalisha nishati, bidhaa za ujenzi, dawa asili, matambiko na ibada hifadhi za misitu kwa baadhi ya jamii.

Bakari anasema, TFS Mwanza wanaimarisha mipaka katika Hifadhi Kome, Maisome, Igwata na Sayaka, zaidi ya kilomita 7,411 mipaka zimehifadhiwa.

Pia anataja miche ya miti 21,700 imepandwa Hifadhi za Igwata na Sayaka wilayani Magu, kukiwapo mipango kitaalamu miaka mitano kuhifadhi misitu ya Maisome na Kome.

Anabainisha wavamizi msituni Sayaka, Maisome na Kome, wameshaondolewa kupisha uoto wa asili na ikolojia kurudi, wakiondolewa wananchi 120 wanaozunguka mistu hiyo.

Kwa mbadala, wamepewa elimu ya uhifadhi na ufugaji nyuki kwa wananchi wanaojihusisha na uvuvi, kwa walioruhusiwa kufanya shughuli zao hifadhini Maisome na Kome, wilayani Sengerema.

Vilevile kuna elimu ya uhifadhi na ufugaji nyuki kwa wafugaji wanaozunguka hifadhini Sayaka na wananchi wanaozunguka mashamba ya miti Rubya na Buhindi.

TFS mkoani Mwanza, inasimamia uendelezaji mashamba ya miti kupandwa Rubya na Buhindi, kunakozalisha miti aina Misindano inayotumika kujenga na kuunda samani.

Pia, ikitumika kuhifadhi ardhi, vyanzo vya maji na kukabili mabadiliko tabianchi, ikiwamo katika mashamba ya Rubya na Buhindi. Kila mwaka kunazalishwa miti yenye ujazo mita 60,000 na kuhudumia wateja 132 wa viwanda vya mbao.

Bakari anasema, hadi sasa TFS imechukua juhudi kuanzisha bustani za miti na program za upandaji miti, yenye vitalu saba vya miche wilaya za Nyamagana, Misungwi, Magu, Sengerema na Ukerewe, vikizalisha miche 1,500 kila mwaka.

Lengo analitaja ni kuwagawia wananchi bure wakapande katika maeneo yao, pia taasisi za umma na binafsi, kupanda pia maeneo ya wazi. vilima vya Mwanza na kurejesha miti kulikovunwa.

Miti huoteshwa vitaluni kuhifadhi mazingira, kuzuia mmomonyoko, kutunza vyanzo vya maji, kurejesha uoto asili na kulikoharibika.

Kuna miti inayokua haraka, Bakari anaitaja ni kuendeleza mashamba serikali Buhindi na Rubya, inayofaa kwa kilimo mseto, maji vizuri, miti ya matunda, mapambo pamoja na vivuli.

Anasema, TFS imefanikiwa katika miaka mitatu kuotesha miti 3,700,744, ikiwamo ya mbao, vivuli, kuni, nguzo, dawa, mapambo, matunda, parachichi, limao, fenesi, mapera mapapai na mapasheni.

Hiyo inaendana na kutolewa miche ya miti bure kwa wananchi na taasisi; miti ipatayo 1,795,423 imepandwa kwenye mkoani Mwanza, kwa kushirikiana na wadau wengine katika miradi ya kimkakati.

Mpaka sasa, zaidi miche ya miti 9,100 imepandwa katika mradi mkubwa wa chanzo cha maji Butimba jijini Mwanza, lengo ni kutunza mazingira ya chanzo hicho, TFS ikisisitiza jamii kuanzisha mashamba madogo kwa ajili ya nishati ya kuni, kilimo mseto na ufugaji nyuki.

Aidha, Bakari anasema wameshwa mashamba madogo ya miti hekta 48 na kupandwa miti hekta 42,080 katika shule za msingi na Chuo cha Ualimu Murutunguru, wilayani Ukerewe; pia wilayani Nyamagana na Misungwi.

**KUHUDUMIA WAFANYABIASHARA**

Kwa miaka mitatu, Bakari anasema TFS Mwanza imewatambua wafanyabiashara wa mazao ya mistu na nyuki 1,571, waliorahisishiwa huduma kwa mfumo wa kiteknolojia uitwao FReMIS (Forest Ressources Management Information System).

Anaueleza, unawarahisishia usajili, uvunaji na usafirishaji mazao mistu, hivyo wananchi au wadau wa mazao hayo, wanajirahisishia michakato wanayohitaji kutoka TFS.

Bakari anasema, wakala umekamilisha ujenzi wa ofisi ghorofa moja ya TFS Kanda Ziwa, wilayani Nyamagana jijini, sasa iko katika hatua kununua boti ya mwendokasi wilayani Sengerema ya doria kudhibiti uharibifu hifadhini, hasa visiwani Maisome na Kome, wilayani humo na kwingineko.



Kwaniaba ya Kamishna wa Uhifadhi TFS, Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Ziwa inakupongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta Mafanikio makubwa katika Kanda ya Ziwa kwenye Uhifadhi wa Misitu na Uendelezaji wa Rasilimali za Misitu na Nyuki zilipoko ndani ya Misitu ya asili na Misitu ya kupanda, pamoja na kuimarika kwa iikolojia katika misitu hiyo. Kazi uliyoifanya katika miaka mitatu kwenye sekta yetu ya misitu inadhihirisha utendaji kazi uliotukuka, hususan katika kuhimiza na kuelekeza utunzaji wa Misitu, Vyanzo vya Maji na Upandaji wa Miti na Utunzaji wa Mazingira kwa Ujumla.



## Waishi kwa hofu kisa kukithiri vitendo vya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

DIWANI wa Kata ya Jambiani, Salama Ali Hamad, amesema kukithiri kwa vitendo vya udhalilishaji kwa watoto kumeifanya jamii kuishi kwa hofu.

Aliyasema hayo alipozungumza na jamii katika mkutano wa kutoa elimu ya sheria ulioandaliwa na Jumuiya ya Wasaidizi wa Sheria Wilaya ya Kusini Unguja (SOPAU).

Alisema wazazi na walezi sasa hivi wamekuwa na hofu kubwa kuhusu watoto wao ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo hivyo ambavyo wahusika wakuu ni watu wao wa karibu katika familia wakiwamo wazazi.

Alisema mtoto amekuwa hayupo salama muda wote, jambo ambalo linawapa mashaka kinamama wakati wote kwa kuhofia vitendo hivyo.

Aidha, alisema kuna haja ya jamii kubadili mitazamo na kuhakikisha wanawalinda watoto wao ili wasifanyiwe vitendo vya udhalilishaji.

Hivyo, alisema kitendo cha SOPAU kutoa ni kizuri na kitawajenga kuwa na uwelewa juu ya madhara ya vitendo ambavyo watoto wao hufanyiwa.

Alisema kuwa upo udhalilishaji wa aina nyingi ambao hufanyiwa watoto na hata watu wazima, kwamba ili kuutokomeza wanahitaji kuwa na ushirikiano wa pamoja baina ya mama na baba pamoja na ndugu waliokaribu.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wenzake, Aviwa Juma, alisema watajitahidi kutoa ulinzi kwa watoto wao lakini hali za umaskini unachangia watoto wao kufanyiwa vitendo hivyo.

Hivyo, alisema mara nyingi watoto ambao wanadhalilishwa ni wale ambao wazazi wao hali zao za kimaisha ni duni.

Mjumbe wa SOPAU, Hija Ame, alisema wamekuwa na utaratibu wa kupita katika kila eneo kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali yanayowahusu yakiwamo ya udhalilishaji, migogoro ya ardhi, ndoa na talaka.

Alisema kuwa lengo la kufanya hivyo ni kutaka kuona kwa namna gani wananchi wanakuwa na uwelewa mzuri wa kufuatilia kesi zao ili waweze kupata haki zao pale linapotokea tatizo.

# Kilo 1,341 dawa za kulevya zateketezwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KILO 1,341 za dawa za kulevya zimeteketezwa visiwani Zanzibar na Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilisha kazi hiyo, Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo, Kanali Burhan Zubeir Nassor alisema dawa zilizoteketezwa ni heroin kilo 21, bangi kilo 1,265, mirungi kilo 30, na valium kilo 25.

Alisema mamlaka hiyo itahakikisha kwamba vielelezo ambavyo vimemaliza kesi katika vyombo vya usimamizi wa sheria wanaviteketeza ili kuzuia dawa hizo zisirudi kwenye jamii.

"Kiujumla kama mnavyofahamu kwamba Zanzibar ni kisiwa na zipo njia nyingi ambapo kijiografia zipo bandari bubu 370, hivyo tunapata ugumu sana katika mapambano haya, lakini tunawaomba wananchi ambao wanaishi katika bandari bubu watusaidie kutupatia taarifa za uingizaji wa dawa za kulevya, ili wanaouhusika tuwachukulie sheria kama ambavyo sheria inavyoelekeza," alisema.

Alisema kwa kupindi kirefu walikuwa hawajateketeza dawa hizo kulikochangiwa na sababu mbalimbali, kwamba dawa zilizoteketezwa ni za tangu mwaka 2018 hadi 2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, alisema serikali itaendelea kuteketeza dawa za kulevya kama ambayo sheria na kanuni zinavyoelekeza.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Sheha Mjaja Juma, alisema uteketezaji wa dawa za kulevya linasimamiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Uteketezaji wa Bidhaa ambazo Hazifai kwa Matumizi ya Binadamu ya Mwaka 1919 ambayo ilitayarishwa kwa mujibu wa Sheria namba 3 ya Mwaka 2015.

Hata hivyo, aliwatoa hofu wananchi kuwa uchomaji wa dawa hizo hautaathiri kiumbe chochote kwa sababu mazingira yanayochomewa yako salama kwa kuwa wametumia jiko maalum.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Machano Othman Said, aliishauri mamlaka husika kuhakikisha kuwa wanaziteketeza dawa hizo kila mwaka.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kupotea kwa vielelezo na kuipongeza mamlaka hiyo kwa kuweka umakini katika suala la uteketezaji wa dawa hizo ambapo taasisi mbalimbali zilishiriki.




Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana (katikati), akiwasha mshumaa kuzindua tamasha la siku tatu kwa ajili ya kuonesha maisha ya kiimani na mafundisho ya Krishna lililowaleta pamoja jamii ya Kihindu kutoka nchini kote, lililoandaliwa na kituo kikuu cha utamaduni na shughuli za kidini cha Shree Goverdhannathji Haveli, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita. Wengine ni Mwenyekiti wa kituo hicho, Yogesh Manek (kulia), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Watumieni maofisa kazi kusuluhisha migogoro kazini'

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa sekta binafsi wametakiwa kuwatumia maofisa kazi, ili kupata elimu ya kutosha juu ya masuala mbalimbali yanayohusiana na usuluhishi na migogoro kazini.

Wito huo umetolewa na Ofisa Kazi Msaidizi wa Kamisheni ya Kazi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Juma Khamis Juma, katika kambi maalum ya utoaji wa elimu juu ya masuala ya usuluhishi na migogoro ya kazi inayoendelea katika viwanja vya mnara wa mapinduzi, Muembe Kisonge, Wilaya ya Mjini.

Alisema endapo wafanyakazi hao watakuwa na uelewa wa kutosha itawasaidia kupata haki na stahiki zao ipasavyo.

Hata hivyo, alisema kuwa mwamko bado ni mdogo wa jamii kuitumia taasisi hiyo katika kupata ufumbuzi wa mambo mbalimbali ya usuluhishi na migogoro katika kazi jambo ambalo alilitaja linapelekea kukosa haki zao.

Alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha kamisheni ya kazi ili kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi katika sekta za umma na binafsi na kuhakikisha wafanyakazi wanapata haki zao.

Pia alisema kitengo hicho kinahimiza masuala ya mahusiano mema kazini, usalama na afya kushughulikia suala la ajira pamoja na utoaji wa elimu kwa waajiri na waajiriwa ndani ya jamii ili kuondoa migogoro katika kazi.

Msuluhishi na Mwamuzi wa migogoro ya kazi, kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi (DHU), Sisahau Rished Faki, alisema kitengo hicho kimeanzishwa chini ya Kifungu cha 72(1) cha Sheria ya Uhusiano Kazini Namba 1 ya Mwaka 2005 ili kuimarisha uhusiano katika maeneo ya kazi.

Aidha, alieleza kuwa kitengo hicho kilichopo ndani ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, chini ya Kamisheni ya Kazi kimesaidia kupunguza migogoro katika sehemu za kazi, kuleta ufanisi, amani na usawa miongoni mwa wafanyakazi na waajiri.

Alisema mlalamikaji anapaswa kuwasilisha mgogoro wa kuachishwa kazi ndani ya siku 14 kuanzia siku aliyoachishwa na ikiwa mgogoro ni tofauti na kuachishwa kazi unapaswa kuwasilishwa ndani ya siku 30 tangu mgogoro ulipotokea.

Aliongeza kuwa endapo mgogoro utapitwa na muda utawasilishwa kupitia ombi la kujaza fomu ya kufungua shauri lililo nje ya muda ambalo litaambatanishwa na hati ya kiapo.

Alibainisha kuwa kitengo hicho kinahakikisha migogoro ya kazi inasuluhishwa na kuamuliwa kwa wakati, uwazi na usawa ambapo takribani migogoro saba hupokelewa na kusuluhishwa kwa mwezi.

Aliitaja migogoro inayowasilishwa mara kwa mara ikiwamo ya kukatishwa kwa mkataba wa kazi visisvyo halali katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Kaskazini na Kusini Unguja.

Mmoja ya watu waliofika kupata elimu hiyo, Bakar Ali Haji alisema elimu hiyo imewasaidia kujua eneo sahihi la kupeleka changamoto zao za kazi na kuweza kupatiwa ufumbuzi.

Hata hivyo aliishauri jamii kutokupuuza kufika katika kambi kama hizo kwani wanaweza kupata elimu ya mambo mbalimbali itakayowasaidia kutatua changamoto zilizokuwa zinawakabili.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**PETER MAREALLE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S103/51** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BIHAWANA SECONDARY SCHOOL** mwaka 1978 na cheti cha chuo cha kilimo na mifugo chenye majina **PETER G.M.G MAREALLE** chenye usajili namba **AV 241** kilichotolewa na **CHUO CHA TENGERU** mwaka 1981. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/135568/2024 PHQ/DAR/KIN/135580/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HAPPINESS EDEN MATOI** anatangaza kupotelewa na vyeti vyake cha kidato cha nne chenye index namba **S0558-0018** kilichotolewa na balaza la mitihani kupitia shule ya secondari ya Mwanga mwaka 2014 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0134-0515** kilichotolewa kituo cha mtihani Old moshi mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Taarifa polisi: **PHQ/DAR/KIN/139517/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL .M. JOHN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0456-0086/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KINANGO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/KIL/HAI/3426/2023**

## ANATAFUTWA



**Mimi TEDDY JOSEPH MWAMI** wa nyaishozi Tegeta simu **# 0713450105,** namtafuta ndugu **Chano Mohamed Nunu** aliyeniuzia plot **#589 block G Tegeta mwaka 2000** anisaidie uhakiki wa mikataba kisheria nipate umilikishwaji kutoka wizara ya ardhi

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LAMECK MAJIGO MJUNGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye majina **INNOMAX COMPANY LIMITED** namba za usajili **MC840DBE** aina ya **HAOJUE.** Chassis No. **LC6PCJBJ8M0055637.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/7983/2024**

**KATIKA BARALA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 119 LA 2024**

**TACHI BOARD LIMITED MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**KILIMACITY INTERNATIONAL COMPANY LTD MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**KILIMACITY INTERNATIONAL COMPANY LTD POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**TACHI BOARD LIMITED** Amefungua/shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala. Shauri husika limepanga kutajwa tarehe 06/08/2024 Saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh.J.W.SILLAS Hivyo unamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 01 Mwezi 07 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11680 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late JUSTINE MACHUMU MAGAYANE Of NZUGUNI within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JESCA KATUSIME ELISA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 7, 2024

Dated at Dodoma this 21 Day of MAY, 2024.
Presented for filling this 7 day of JUNE, 2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri la Madai Na. 99/2024**

**Jina la mdai NKWABI MBOJE**

**Jina la mdaiwa LAMECK GIBSON KATORWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa : LAMECK GIBSON KATORWA WA GEITA**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai)**
**MADAI YA FEDHA TSHS 1,715,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 16 mwezi 07 mwaka 2024 saa2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 07 mwaka 2024

HAKIMU


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 745 700 710.***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA/ KITAIFA

# Ruto atia saini sheria mpya Tume Huru ya Uchaguzi

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, ametia saini mswada wa marekebisho ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) na kuwa sheria kamili.

Katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Kenyatta (KICC), miongoni mwa waliohudhuria ni viongozi wakuu wa upinzani kutoka muungano wa Azimio, Raila Odinga na Kalonzo Musyoka.

Hatua hiyo inakuja kufuatia maandamano yaliyofanywa na vijana nchini humo wanaojiita Gen - Z kumshinikiza Rais Ruto kutosaini muswada wa fedha 2024 na kumtaka kuharakisha mchakato wa uundwaji wa tume hiyo kwa mujibu wa katiba.

Mchakato wa uteuzi wa maofisa wa Tume ya Uchaguzi nchini Kenya unatarajiwa kuanza baada ya kiongozi huyo kuidhisha na kuwa sheria.

Ndani ya sheria hiyo, kutakuwapo nafasi ya Mwenyekiti na wajumbe huru watakaomba nafasi hiyo.

Pia wajumbe wawili watakaounda tume hiyo mmoja atatoka chama cha wanasheria wa Kenya na mwingine taasisi ya dini. Muswada huo ni mojawapo ya utekelezaji wa matokeo ya mazungumzo ya Kamati ya Kitaifa ya Majadiliano.

Katika hafla hiyo, viongozi wa serikali walikuwapo akiwamo Naibu Rais Rigathi Gachagua na Mwanasheria Mkuu wa serikali, Justin Muturi.

Wabunge kadhaa walioshuhudia tukio hilo muhimu ni Opiyo Wandayi, Naibu viongozi wa chama cha ODM, Hassan Joho na Wycliffe Oparanya.

***BBC.***



Wapalestina wakikimbia tena mji wa Gaza kuepuka mashambulizi mapya kutoka vikosi vya ya Israel juzi. **PICHA: AFP**

# Sudani Kusini yaadhimisha miaka 13 ya uhuru wake

**JUBA,** SUDAN KUSINI

SUDANI Kusini jana imeadhimisha miaka 13 tangu ilipotengana na Sudan na kuwa taifa huru.

Sherehe hizo zimefanyika wakati taifa hilo likiendelea kupitia changamoto mbalimbali ikiwamo vita vya wenyewe kwa wenyewe na migogoro ya kisiasa.

Katibu Mkuu wa chama tawala cha SPLM, amesema katika kipindi hicho Rais Salva Kiir, ameweka misingi ya maridhiano na kulijenga taifa hilo kwa pamoja.

„Kazi ambayo Rais Salva Kiir anafanya sasa ni kuhakikisha kuwa pande zote mbili zinazohusika na mapigano zimesitisha kupigana, hata hivyo kilichoko kwa sasa mapigano huko Sudan yamechangia sehemu kubwa matatizo ya nchi yetu.“ Alisema Ayuol.

Aidha, Regina Joseph Kaba katibu mkuu wa chama cha upinzani kinachoongozwa na Riek Machar, alisema hali ya umaskini imezidi kuimarika kiasi ambacho taifa hilo linaelekea kuanguka.

"Kabla ya uhuru hali ya umaskini ilikuwa asilimia 60, sasa imepanda na kufikia asilimia 80. Tunaelekea pabaya kiuchumi. Kiwango cha watu ambao hawajasoma kilikuwa asilimia 27 mwaka 2011 lakini sasa ni asilimia 32." Alisema.

***RFI***

# Rais Liberia apunguza mshahara wake

**MONROVIA,** LIBERIA

RAIS wa Liberia, Joseph Boakai, amepunguza mshahara wake kwa asilimia 40.

Kiongozi huyo kuanzi mwezi Februari baada ya kuapishwa kuwa rais, alikuwa akipokea dola za Marekani, 13,400, na kuanzia mwezi huu atalipwa dola 8,000.

Sawa na shilingi ya Tanzania, awali alilipwa milioni 35.57 na sasa atapokea mshahara wa milioni 21.2 kila mwezi.

Ofisi ya rais wa nchi hiyo, ilisema Boakai ana matumaini ya kuweka mfano wa utawala unaowajibika na kuonyesha mshikamano kwa Waliberia.

Mishahara ya serikali imekuwa ikichunguzwa vikali hivi karibuni huku Waliberia wakilalamikia kupanda kwa gharama ya maisha.

Takriban mtu mmoja kati ya watano anaishi kwa chini ya shilingi 2,500 kwa siku katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Hatua hiyo inafuatia ile ya mtangulizi wake, George Weah, ambaye alikatwa asilimia 25 ya mshahara wake.

Baadhi ya watu katika taifa hilo wamepongeza uamuzi huo, lakini wengine wanahoji kama kweli hatua hiyo inalingana na kujitolea kutokana bado anapokea marupurupu mengi.

***BBC***

## Makalla asema ujenzi wa barabara shule za ghorofa utabadili jiji la Dar

**Na Romana Mallya**

KATIBU wa NEC, Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, amesema ujenzi wa barabara unaoendelea zikiwamo zinazounganisha mitaa pamoja na shule za ghorofa za sekondari ni udhihirisho Rais Samia Suluhu Hassan kutaka kubadilisha Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, ameagiza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mnazi Mnazi, Halmashauri ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam uliosimama miezi miwili ukamilishwe kwa kasi.

Alitoa agizo hilo jana mkoani humo baada ya kutembelea shule hiyo kujionea ujenzi wa madarasa 20, ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya siku saba.

Makalla alisema amefurahi shule hiyo kuwekwa katika ratiba yake.

Alisema ujenzi wa madarasa mkoani humo ulikuwa unachelewa kutokana na ufinyu wa maeneo wakaamua kuondokana na madarasa ya mtawanyo na kujenga ya ghorofa.

"Mnazi Mmoja ni miongoni mwa shule za sekondari ambazo zinajengwa madarasa haya. Mkurugenzi umesema hapa fedha za ujenzi zipo za kutosha ila kwa kuwa mnatumia akaunti ya pamoja ya maendeleo, maelekezo yangu tukamilishe shule hii kwa kasi kubwa tutimize dhamira ya Rais Samia. Tunaamini wanafunzi bora tutawapata hapa Mnazi Mmoja.

"Ninaamini jengo hili likikamilika hapa pataheshimika na wewe Mkurugenzi endapo utafanikisha utaweka rekodi, hizo sababu mlizotoa zifanyieni kazi ili tukamilishe dhamira njema ya Rais Samia ya kuendelea kuboresha mazingira ya elimu na kutoa heshima ya ile Sh. bilioni 1.8 iliyotolewa na Rais Samia," alisema Makalla.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, Jomaary Santura, alisema shule hiyo inatarajia kukamilika mwezi Oktoba, mwaka huu na tayari Sh. milioni 540 zimeshalipwa.

Katika ziara hiyo, Makalla alitembelea mradi wa barabara za mtaa wa Mwanza na Kigoma, Jimbo la Ilala ambazo zitawekewa lami, mifereji na taa za barabarani.

Makalla alisema kila kona jijini humo kunatifuliwa na watu wapo kazini ikiwa ni ishara tosha kwamba, Rais Samia ameamua kuibadilisha Dar es Salaam.

# PRISONS YAACHA WANANE KWA MPIGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imetangaza kuachana na wachezaji wanane kwa mpigo wakiwamo walioisaidia timu hiyo kubaki Ligi Kuu.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari ya Klabu hiyo, imesema imeachana na wachezaji hao kwa sababu mbalimbali, lakini kikubwa ni kutaka kufanya maboresho makubwa ya kikosi cha kuelekea kwenye msimu mpya.

„Ilikuwa muda mzuri kuwa nanyi, tunawatakia kila la kheri huko mwendako," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Wachezaji waliopewa mkono wa kwaheri ni pamoja na aliyekuwa kipa namba moja, Yona Amosi, Meshack Suleiman, Batshi Mambote, Messi Atangana, Ibrahim Abraham, Hamisi Kisanga na Joshua Nyatini.

Prisons ambayo msimu uliopita ilimaliza Ligi Kuu ikiwa nafasi ya tisa na pointi zake 34, iko katika harakati za kujiimarisha kuelekea msimu ujao, ikiwa tayari imeshamtangaza Kocha Mkuu, Mbwana Makata.

Mwishoni mwa mwezi uliopita Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Ramadhani Nyamka, aliahidi kuisaidia kufanya usajili mzuri utakaoifanya kuwa na kikosi imara na cha kutisha.

„Nawapongeza wachezaji wa Prisons kwa sababu tulianza vibaya kidogo, lakini kwenye dirisha dogo tulifanya mabadiliko, kwa maana benchi la ufundi pia maingizo mapya kama matano hivi, yalisaidia kabisa kubadilisha kiwango cha timu na mmeona matokeo yake ni haya, Kilichosalia ni kufanya usajili mkubwa utakaoisaidia kufanya vizuri zaidi msimu ujao, tunataka sasa tuwe na timu yenye msuli wa kugombea Ubingwa wa Tanzania Bara" alisema.

## KVZ FC kufumua kikosi chake

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KLABU ya KVZ FC imesema inatarajia kufanya maboresho makubwa ya kikosi chake ili kupata timu ya ushindani kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Katika maboresho hayo timu hiyo tayari imetangaza kuachana na wachezaji 10 ambao walitumikia timu hiyo msimu uliopita.

Kati ya wachezaji hao, wachezaji wawili wametolewa kwa mkopo kutokana na viwango vyao kushuka hali iliyopelekea kukaa muda mrefu benchi bila kupata nafasi ya kucheza.

Wachezaji watatu wameuzwa lakini bado hawajaweka wazi timu walizokwenda wakati wachezaji watano wamewapa mkono wa kwa heri.

KVZ FC katika msimu uliopita ilishindwa kutwaa taji la Ligi kuu ya Zanzibar na kuambulia nafasi ya nne katika ligi hiyo yenye timu 16 licha ya hapo awali kutangaza nia ya kutwaa ubingwa.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha wa timu hiyo, Ali Mohamed Ameir alisema mpango wao mkubwa ni kuhakikisha wanaboresha timu hiyo ili kuanza msimu mpya kwa nguvu.

Alisema kulingana na ushindani uliokuwapo msimu uliopita, mipango yao ni kupata wachezaji bora na wenye viwango vya juu ambao wataweza kufanikisha malengo ya timu hiyo.

Alisema msimu iliopita ingawa walishindwa kutwaa ubingwa bado walipambana na kufanikiwa kumaliza katika nafasi ya nne.

"Maboresho ya kikosi chetu kwa msimu huu yatazingatia zaidi changamoto ambazo tumeziona kwa msimu uliopita," alisema.

Hata hivyo alisema anatarajia kuanza maandalizi yao mapema zaidi ili kupata timu yenye muunganiko katika kuelekea michezo ya Ligi Kuu ambayo bado Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) haijatoa kalenda yake ya msimu mpya.



Mshambuliaji mpya wa Yanga, Mzimbabwe Prince Dube (katikati), akiwa na wachezaji wenzake, Muivory Coast, Kouassi Yao (kulia) na mzawa Nickson Kibabage (kushoto) kwenye mazoezi ya ‚gym' jana. **PICHA: BINZUBEIRY**

# JKT TANZANIA YAANZA UKARABATI ISAMUHYO, MABENA ASHUHUDIA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya JKT Tanzania imeanza rasmi ukarabati wa uwanja wake, Meja Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam na kushuhudiwa na Mkuu wa Utawala wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali, Hassan Mabena.

Brigedia Jenerali huyo alifanya ziara hiyo juzi kwenye uwanja huo kujionea ukarabati wake kwenye uwanja ambao unatumiwa na timu ya mpira wa miguu, JKT Tanzania iliyopo Ligi Kuu Tanzania Bara, na timu ya soka wanawake, JKT Queens.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema lengo la ukaguzi ni kuangalia maendeleo kwenye uwanja huo unaomilikiwa na Jeshi hilo ambalo limeamua kufanyia maboresho makubwa, hasa eneo la kuchezea 'pitch', kujengwa majukwaa ya mashabiki kuuzunguka uwanja wote.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Masau Bwire, amesema kuwa mradi huo ukikamilika, Meja Jenerali Isamuhyo, utakuwa moja ya viwanja bora nchini kwa jinsi plani ya ujenzi inavyoendelea.

"Tumeshaanza kuufanyia maboresho uwanja wetu, tunataka kuufanya uwe moja ya viwanja bora sana nchini na hilo linawezekana ukarabati tunaofanya ni wa kuweka majukwaa, ili wadau, wapenzi na mashabiki wetu waje kutazama soka ndani ya uwanja kwa starehe, soka ni burudani, hatutaki watu waje waanze kusimama wengine wanawazuia wenzao mbele kuona mechi, hapana..., tunataka kila mmoja awe amekaa, tena kwenye kiti ambacho atakuwa amestarehe, huku akiwa anaangalia mchezo kwa raha mustarehe," alisema Masau.

Ujenzi wa uwanja huo uliotumiwa na JKT Tanzania kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, unakuja baada ya baadhi ya mashabiki kulalamikia kuwa uwanja huo bado haujawa kwenye ubora unaotakiwa hasa eneo la kuchezea.

## ZISIKUPITE

### EDERSON ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kupokea ombi kutoka Saudi Arabia kumnunua mlinda mlango Ederson na wanataka zaidi ya pauni milioni 30 kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ambaye anahusishwa na klabu ya Al-Nassr. (***Sportsport***)

### MASON AWANIWA MARSEILLE

MARSEILLE ina uhakika wa kuwashinda Lazio kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood baada ya klabu hiyo ya Serie A kutoa pauni milioni 17 kwa mchezaji huyo wa miaka 22. (***Mail***)

### PAQUETA AWEKWA SOKONI

KLABU ya Famengo ilianza mawasiliano na West Ham kuhusu usajili wa mchezaji wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, Lucas Paqueta na klabu hizo mbili ziko katika hatua za awali za mazungumzo. (***Globo***)

### WILLIAMS ANUKIA BARCA

BARCELONA inaongoza mbio za kumsajili winga wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams, huku Arsenal na Chelsea wakikabiliwa na hatari ya kumkosa mchezaji huyo. (***Football Insider***)

### CUCURELLA AMSHAWISHI WILLIAMS

MLINZI wa Chelsea, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 25, amesema anajaribu kumshawishi mchezaji mwenzake wa Hispania, Nico Williams ajiunge na The Blues, wawili hao wapo kwenye kikosi cha nchi yao kwenye Euro 2024. (***Sport***)

### YORO AWINDWA

MLINZI wa Lille, Leny Yoro anataka kuhamia Real Madrid na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 18 anasubiri klabu kuafikiana, wakati Liverpool na Paris St-Germain ziko tayari kunyakua iwapo dili hilo litasambaratika. (***Fabrizio Romano***)

### MATTY AOTA MBAWA

MLINZI wa kulia wa Aston Villa, Matty Cash huenda asijiunge na AC Milan licha ya ripoti zinazomhusisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mwenye umri wa miaka 26 na klabu hiyo ya Serie A. (***Birmingham Live***)

### CANCELO NA BARCA

KLABU ya Barcelona ina nia ya kumsajili Joao Cancelo wa Manchester City baada ya beki huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 30 kucheza kwa mkopo katika klabu hiyo ya Hispania msimu uliopita. (***SportsMole***)

### KOOPMEINERS ATAKIWA JUVE

JUVENTUS inataka kuimarisha safu yao ya kati kwa kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 26, Teun Koopmeiners. (***La Gazzetta dello Sport***)

### LUSALE AWINDWA MAN UTD

KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili kinda mwenye umri wa miaka 16 kutoka Slovakia, Samuel Lusale kutoka Crystal Palace. (***Moror***)

### DOMINIC BASI TENA

USAJILI wa Newcastle United wa mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, umegonga mwamba baada ya Magpies kushindwa kumuuza mshambuliaji wao, Callum Wilson. (***Telegraph***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ODEGAARD ANA UHAKIKA WA MATAJI ARSENAL

**LONDON,** England

### Anaona watarejea wakiwa na nguvu zaidi baada ya huzuni ya...

MARTIN Ødegaard ana imani Arsenal "itazawadiwa kombe" msimu ujao na ameapa kuwa wanaweza kurejea wakiwa na nguvu zaidi baada ya huzuni ya msimu uliopita.

Kikosi cha Mikel Arteta kiliweka rekodi mpya za klabu katika enzi ya Ligi ya Kuu England kwa kupata ushindi katika michezo 28 ya Ligi Kuu na kufunga mabao 91 lakini bado walishindwa kutwaa ubingwa huku Manchester City ikitwaa taji lao la nne mfululizo kwa tofauti ya pointi mbili.

Arsenal wameanza maandalizi yao ya msimu wa 2024-25 mbele ya klabu nyingine huku wachezaji tisa ambao hawajahusika katika michuano ya Euro au Copa América -- wakiwamo Ødegaard, Ben White na Jurriën Timber -- walijiunga na wafanyakazi wa klabu katika jiji la Marbella nchini Hispania kwa kambi ambayo inaangazia hali zote mbili na kuruhusu wakati wa kupumzika na wanafamilia.

"Tuliweka historia kama tulivyozungumza hapo awali na lazima tujivunie mambo hayo," alisema Ødegaard.

**"Haikutosha kushinda na ndivyo tulivyotaka kufanya. Sote tulihisi kukatishwa tamaa kwa kuwa karibu sana. Lakini katika soka, ni alama ndogo. Ni rahisi kuangalia mchezo mmoja lakini lazima uangalie kwa msimu mzima na tena ni alama ndogo. Hatukuwa na msimamo wa kushinda.**

"Tunajua tunaweza kuimarika, tunajua tunakwenda kuwa bora zaidi. Hilo ndilo tunalofanyia kazi kwa sasa. Ni alama ndogo tu, maelezo madogo kwenye mchezo na jinsi ya kukabiliana na msimu mrefu. Karibu sana, lakini tutarudi kwa nguvu zaidi nina hakika.

"Nadhani ni rahisi kupata motisha kwa sababu sote tunataka kushinda, sote tunataka kitu kimoja na sote tunasukumana kwa nguvu kila siku - wafanyakazi, wachezaji, mashabiki, kila mtu anasukuma upande mmoja.

"Nadhani ni kuhusu kufanya mambo hayo madogo kila siku ili kuwa bora kidogo na mwishowe nina uhakika itazawadiwa na kombe."

Arsenal itaelekea Marekani baadaye mwezi huu kwa michezo dhidi ya Bournemouth, Manchester United na Liverpool.

# MWAMUZI MTATA KUAMUA ENGLAND, UHOLANZI




**DORTMUND,** Ujerumani

UEFA imemteua mwamuzi ambaye hapo awali alikiri upangaji matokeo na ambaye uadilifu wake ulitiliwa shaka hadharani na Jude Bellingham kwa mechi ya nusu fainali ya Euro 2024 dhidi ya Uholanzi.

Felix Zwayer atasimamia pambano la leo Jumatano huko Dortmund licha ya kufungiwa kwa miezi sita mwaka 2005 baada ya kupokea hongo ya euro 300 kutoka kwa ofisa mwingine, Robert Hoyzer.

Uchunguzi wa 2005 uligundua kuwa Zwayer alikubali hongo ili kuipendelea klabu ya Ujerumani ya Wuppertaler SV katika mechi yao dhidi ya Werder Bremen Mei 2004.

Bellingham alirejelea tukio hilo katika mahojiano baada ya mechi mwaka 2021 baada ya Borussia Dortmund kufungwa 3-2 na Bayern Munich katika mchezo mkubwa wa Bundesliga.

Kiungo huyo wa kati wa England aliyeichezea Dortmund wakati huo alisema: “Unaweza kuangalia maamuzi mengi kwenye mchezo.

“Unampa mwamuzi, ambaye amepanga mechi kabla, mchezo mkubwa zaidi nchini Ujerumani. Unatarajia nini?”

Bellingham baadaye alipigwa faini ya Euro 40,000 kwa maoni yake ambayo yalikuja baada ya Dortmund kunyimwa penalti.

# Alcantara atangaza kustaafu soka

**MADRID,** Hispania

THIAGO Alcantara ametangaza kustaafu soka la kulipwa.

Kiungo huyo wa zamani wa Barcelona, Bayern Munich na Liverpool aliona mkataba wake Anfield ukimalizika msimu huu wa majira ya joto, licha ya huduma yake kutakiwa Saudi Arabia, ameamua kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 33.

“Siku zote nitakuwa tayari kurudisha kile nilichopewa na ninashukuru kwa wakati ambao nimefurahia,” aliandika Thiago kwenye mtandao wa kijamii.

“Asante, mpira wa miguu. Na kwa wote walionisindikiza na kunifanya kuwa mchezaji bora.

“Tutaonana hivi karibuni, Thiago.”

Mkurugenzi Mtendaji wa Bayern, Jan-Christian Dreesen alitoa pongezi kwa Mhispania huyo, ambaye alicheza mechi 235 katika klabu hiyo kati ya 2013 na 2020.

“Kwaheri Thiago, ilikuwa heshima,” Dreesen alisema katika taarifa yake.

“Thiago alikuwa sehemu ya timu yetu kwa miaka saba, na ilikuwa pamoja naye kwamba tulishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2020.

Pep Guardiola alisema: ‘”Asante sana kwa wakati mzuri pamoja. Tunakutakia kila la kheri kwa maisha yako yajayo. Nafasi katika timu yetu ya magwiji itahifadhiwa kila wakati.”

Katika mechi 235 alizochezea Bayern, Thiago aliweza kucheza mechi 100 akiwa na Barcelona na nyingine 98 akiwa na Liverpool, huku majeraha yakionekana kumtatiza kiungo huyo wa zamani katika kipindi cha mwisho cha maisha yake ya soka huko Anfield.



# Greenwood sasa kutua Marseille

**MANCHESTER,** England




MANCHESTER United ipo kwenye mazungumzo na Marseille kuhusu mkataba wa kudumu ambao utamwezesha Mason Greenwood kuondoka Old Trafford, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alicheza kwa mkopo nchini Hispania msimu uliopita akiwa na Getafe, akifunga mabao 10 katika mechi 36 alizoichezea timu hiyo ya LaLiga, lakini alitakiwa kurejea United kwa ajili ya mazoezi ya kujiandaa na msimu ujao kutokana na mkataba wake kuwa bado na miezi 12.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba Greenwood alikuwa kwenye uwanja wa mazoezi wa United, Carrington.

Greenwood hajaichezea United tangu kusimamishwa na klabu Januari 2022 baada ya kukutwa na tuhuma za ubakaji na unyanyasaji, huku Polisi wa Greater Manchester wakithibitisha kuwapo kwa “picha na video za mitandao ya kijamii zilizotumwa na mwanamke akiripoti matukio ya ukatili wa kimwili.”

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mara moja alishtakiwa kwa jaribio la ubakaji, kujihusisha na shambulio lililosababisha madhara halisi ya mwili kwa tarehe ya kesi iliyopangwa Novemba 2023, kabla ya mashtaka yake kufutwa.

Licha ya kufutwa kwa mashtaka dhidi ya Greenwood, mchezaji huyo hajarejea uwanjani kwa United akiwa na klabu hiyo badala yake ameamua kutafuta timu mpya.

Getafe walikuwa wakitaka kumsajili Greenwood kwa mkataba wa kudumu kufuatia mafanikio yake ya mkopo msimu uliopita, lakini vyanzo vimesema kwamba United inataka angalau pauni milioni 20 ambazo wameshindwa kulipwa.

Juventus, Atlético Madrid na Lazio zote zina nia ya kutaka kupata mkataba wa kudumu kwa Greenwood, lakini timu ya Ufaransa ya Marseille sasa imeibuka kuwa mstari wa mbele huku chanzo kikiiambia ESPN kwamba timu hiyo ya Ligue 1 imewasilisha ofa thabiti na mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea.

Katika hatua hii, ada na masharti ya mpango wowote hayajafichuliwa.

HABARI MICHEZO

# SIMBA YATANGAZA RASMI KUACHANA NA KANOUTE

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Simba jana imetangaza rasmi kuachana na kiungo wake, Sadio Kanoute baada ya mkataba wake kumalizika klabu hapo.

Kanoute alijiunga na Simba msimu wa 2021/2022 akitokea kwenye klabu ya Al Ahly Benghazi ya nchini Libya na kusaini mkataba wa miaka mitatu uliomalizika hivi karibuni.

Hata hivyo, siku moja kabla ya kutangaza kuachana na Kanoute, uongozi wa klabu hiyo ulitangaza kumsajili kiungo mzawa, Yusuph Kagoma ambaye sasa anakwenda kuchukua nafasi ya Kanoute kwenye kikosi hicho.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema uongozi wa klabu hiyo unaendelea kukiimarisha kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi na mshindano ya kimataifa watakayoshiriki.

„Tunamshukuru sana Kanoute kwa muda wote aliokuwa akiitumikia klabu yetu, mchango wake ni mkubwa mno na Wanasimba wataukumbuka," alisema Ahmed.

Aidha, alisema bado wanaendelea na usajili na hivi karibuni watatangaza mchezaji mwingine waliomsajili kwa ajili ya kuitumikia klabu hiyo.

„Simba ya msimu ujao itakuwa ya moto, tunataka kurudisha heshima yetu, tunataka kurudisha ufalme wetu na ndio maana unaona unafanyika usajili wa nguvu," alisema Ahmed.




Mchezaji Rafi Ayub (katikati) wa Timu ya Vijana Kids ya Kitunda jijini Dar es Salaam, akimiliki mpira huku akizongwa na wenzake wakati wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dube: Nataka kushinda makombe

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI mpya wa klabu ya Yanga, Prince Dube, amesema anaamini anaweza kushinda mataji akiwa na mabingwa hao watetezi.

Nyota huyo jana aliungana na wachezaji wengine kuanza maandalizi yao kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili, Dube aliyejiunga na Yanga akitokea Azam FC, alisema lengo lake ni kuona anashinda taji la Ligi Kuu msimu ujao na kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa.

„Nipo tayari kutoa mchango wangu kwenye timu, naamini naweza kutwaa mataji nikiwa na Yanga... tumeanza maandalizi na nitahakikisha najituma kwa ajili ya timu," alisema nyota huyo raia wa Zimbabwe.

Alisema Yanga ina wachezaji wazuri na wenye uzoefu hivyo ana uhakika kama watajituma wanaweza wakatetea tena ubingwa wao wa Ligi Kuu.

Kabla ya kujiunga na Yanga, Dube alikuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi cha Azam kabla ya kuomba kuondoka ndani ya timu hiyo na kujiunga na Yanga.

Dube pia alikuwa akiwindwa na klabu ya Simba kabla ya kuamua kumwaga wino kuwatumikia mabingwa hao wa nchi.

# Kundi la pili Simba kuondoka leo

INATOKA UK. 24

mu, mchezaji atapimwa na kifaa hicho, akionekana ana kilevi mwilini hatoruhusiwa kuingia kambini na hapo atakuwa amefanya makosa mawili, moja ni kutokuwa kwenye kituo chake cha kazi, lakini pia kuhesabiwa kuwa ni mlevi, hivyo atakumbana na adhabu kali ambayo itaainishwa baadaye," alisema mtoa taarifa huyo huku pia wachezaji wenye tabia ya ugomvi nao watakumbana na adhabu kama hiyo.

Pia katika kikao hicho kilichokutanisha Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Ushauri, wachezaji na baadhi ya wafanyakazi wa klabu hiyo, wametakiwa kuvaa nguo rasmi wakati wakiwa kambini ambazo ni zile zenye nembo ya wadhamini na ile ya klabu.

# Yanga yaanzia 'Gym' ikimtangaza Andambwile

INATOKA UK. 24

itakuwa ni moja tu, tukishinda tutachukua kombe letu, kabla ya mechi hiyo tutakuwa na wiki tatu za kunoa visu vyetu vizuri, na nadhani hilo litakuwa kombe letu la kwanza, tena tutalichukua nje ya nchi," alisema Kamwe.

Wakati hayo yakiendelea, klabu hiyo jana mchana imemtangaza mchezaji Aziz Andambwile akitoka Singida Fountain Gate.

Kiungo huyo mkabaji ambaye ni mzawa, alikuwa akiichezea Mbeya City, kabla ya kujiunga na Singida Big Stars mwaka 2022.

Usajili wa mchezaji unakuja siku moja, baada ya Simba kumsajili kiungo mkabaji kutoka klabu hiyo hiyo, Yusuph Kagoma.

Habari zinasema awali Yanga ilimhitaji Kagoma, lakini ilizidiwa kete na Wekundu wa Msimbazi na baadaye kuamua kumgeukia Andambwile.

**"Tunashukuru, tumefanya usajili mzuri, tumesajili wachezaji bora na kutengeneza kikosi bora cha ushindani ndani na nje ya nchi, hatukuwa na kelele kwa sababu wachezaji tuliotaka kuwasajili safari hii ni wakubwa ambao tungeenda kwa kelele tungewapoteza, watu walikuja kushtuka mwishoni tumeshamaliza mchezo," alitamba Kamwe.**

Michezo
Nipashe Jumatano Julai 10, 2024

Odegaard ana uhakika wa mataji Arsenal
UKURASA 21



# Kundi la pili Simba kuoondoka leo Dar

Litajumuisha wachezaji na viongozi, kwenda kuungana na wengine nchini Misri, watovu wa nidhamu kukiona...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

KUNDI la pili la wachezaji na viongozi wa klabu ya Simba linaondoka nchini leo kwenda Misri kuungana na wengine waliotangulia tayari kwa maandalizi ya msimu mpya.

Awali baadhi ya wachezaji na benchi la ufundi waliondoka nchini juzi kuelekea katika mji wa Ismailia watakapoweka kambi ya wiki tatu kabla ya kurejea nchini kwenye kilele cha tamasha la kila mwaka la 'Simba Day'.

Akizunguma na Nipashe, Ofisa habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema baada ya kundi hilo la pili kuondoka sasa wataanza rasmi maandalizi yao chini ya kocha mpya Fadlu Davids aliyetangazwa na Simba hivi karibuni kuchukua mikoba ya kocha Benchikha aliyeachana na Simba.

„Sasa kikosi chetu kitakuwa kimekamilika tayari kwa maandalizi ya chini ya benchi jipya la ufundi, lakini golikipa wetu Ayoub Lakred naye ataungana na timu Misri akitokea kwao Morocco," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kazi sasa imebaki kwa benchi la ufundi kuandaa timu tayari kwa mikikimikiki ya Ligi Kuu pamoja na mashindano ya kimataifa ambapo Simba itashiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika hatua nyingine, klabu hiyo imeweka mikakati ya kuwapima kilevi wachezaji wake wote watakaokuwa wakiingia kambini.

Habari zilizopatikana katika kikao kilichofanyika wiki hii kwenye hoteli moja pembeni ya Bahari ya Hindi, Dar es Salaam kilichoongozwa na Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu hiyo, Mohamed Dewji, pamoja na mambo mengine, kilisisitiza nidhamu kwa wachezaji pamoja na uwajibikaji ili kuipa mafanikio timu hiyo uwanjani.

Mmoja wa waliokuwa kwenye kikao hicho amesema, wachezaji wa timu hiyo walitangaziwa kuwa meneja mpya wa timu atakabidhiwa kifaa maalum kinachoweza kupima kama mchezaji ataingia kambini akiwa amelewa na kama itakuwa hivyo basi atazuiliwa kuingia kambini."

„Huu ni mkakati mpya wa kutengeneza timu ambayo ina wachezaji wenye nidha-

INAENDELEA UK. 23




Kiungo mpya wa klabu ya Yanga, Clatous Chama akiwa kwenye jezi ya timu hiyo baada ya kutangazwa rasmi jana kujiunga na timu hiyo akitokea Simba. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Yanga yaanzia 'Gym' ikimtangaza Andambwile

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga jana kimeanza rasmi maandalizi ya mashindano msimu ujao, huku klabu hiyo ikitamba kutwaa taji la kwanza nchini Afrika Kusini kwenye michuano ya Kombe la Toyota.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema wachezaji wapya na wa zamani waliosajiliwa wameshaanza kuwasili na itachukua muda wa siku tatu kukamilisha idadi ya wote waliosajiliwa kwa msimu ujao.

Amesema kwa siku ya kwanza wale waliowasili walipimwa afya na kuanza mazoezi ya kujenga miili yao na kuwa na pumzi zoezi ambalo litaendelea kwa wachezaji wote watakaowasili.

„Tulianza asubuhi kucheki afya zao na baadaye mazoezi ya fiziki yaliyofanyika kwenye 'gym' pale Gymkhana, Kocha Mkuu Miguel Gamondi na benchi lake la ufundi wote wameshaingia, wachezaji wengi wameshaingia, wapya na wa zamani, wote wanaonekana kuwa na furaha, hii inaleta picha kuwa tutakuwa na msimu mwingine mzuri," alisema Kamwe na kuongeza kwa siku tatu watakuwa na kazi ya kupokea wachezaji zoezi ambalo litaisha leo Jumatano.

„Tuna siku tatu hizi za kuripoti, kupima afya na mazoezi ya utimamu wa mwili, baada ya hapo tutakuwa na nafasi nzuri ya kutangaza 'programu' nzima ya Yanga kwenye maandalizi ya msimu ujao," alisema.

Akizungumzia ziara yao waliyoalikwa kwenda Afrika Kusini kwa ajili ya mechi ya Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini katika mchezo utakaochezwa Julai 28, Uwanja wa Bloemfontein, alisema itakuwa ni fursa nzuri kwao kutwaa taji la kwanza msimu ujao kabla ya hata michuano mingine haijaanza.

„Niwaambie tu watu kuwa mechi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >